# KUCHUNGUZA MABADILIKO YA KASIDA VISIWANI ZANZIBAR BAADA YA MAPINDUZI NA WAKATI WA SOKO HURIA

**OTHMAN SULEIMAN HAMAD**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA MASHARTI YA SHAHADA YA UZAMILI YA (M.A KISWAHILI - FASIHI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2017**

# UTHIBITISHO

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma kazi hii na anapendekeza kuwa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kukubali kupokea tasnifu hii: "**Kuchunguza Mabadiliko ya Kasida Visiwani Zanzibar Baada ya Mapinduzi na Wakati wa Soko Huria"** na kwamba nimeridhika kuwa tasnifu hii imefikia kiwango kinachotakiwa na inafaa kuhudhurishwa kwa utahini wa shahada ya uzamili (M. A Kiswahili – Fasihi) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

……………………….……………..

Prof. Emmanuel Mbogo

(Msimamizi)

……………………….……………..

Tarehe

# HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote ile ya Tasnifu hii kama kutoa sehemu ndogo ya tasnifu hii, kielektroniki au njia nyegine yoyote ile bila ya idhini ya Muandishi wa Tasnifu hii au kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

**TAMKO**

Mimi, **Othman Suleiman Hamad**, nathibitisha kuwa kazi hii ni yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada hii au nyengine yoyote.

………………………………………..

Saini

…………………………………….

Tarehe

# TABARUKU

Ninatabaruku Tasnifu hii kwa familia yangu. Nawatakia maisha mema hapa duniani na zaidi huko akhera. Nawaomba wawe watu wema kwa wanaemjua na wasiemjua.

## SHUKURANI

Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyeenzi Mungu Muumba wa mbingu, ardhi na vilivyomo kwa kunijaalia uhai, uzima na kunipa uwezo wa kuufanya utafiti huu, kuandika na kuikamilisha kazi hii. Pili napenda kuwashukuru wote waliochangia kwa namna moja au nyengine kukamilika kwa kazi hii. Hata hivyo si rahisi kuwataja wote kwa majina, ila ninapenda kuwashukuru wote nitakaowataja na ambao sitowataja kwa mchango wao wa kuifanikisha kazi hii.

Shukurani za pekee ziende kwa msimamizi wangu, Prof. Emmanuel Mbogo, kwanza kwa kunishawishi kuedelea na masomo haya, pili kwa kukubali kuwa msimamizi wangu, na tatu kwa moyo wake wa kunihimiza kufanya kazi kila alipohisi kuwepo kwa uzorotaji na namna fulani ya kusita sita na kuchelewesha kazi. Yeye alikuwa kwangu ni mshauri, muelekezaji na mwalimu alienikosoa kwa busara na hekima kubwa kila ilipobidi kukosolewa na kuelekezwa. Cha kumlipa mimi sina, lakini sitoacha kumuombea dua kwa Mwenyeenzi Mungu amzidishie moyo wa upendo na ampe nguvu aweze kuendelea kuwa hazina kubwa yenye kutegemewa kwa manufaa ya sasa na ya baadae, kwani yeye ni bahari isiyokauka. Hivyo wataweza kunufaika wengi wa enzi hizi a zijazo.

Aidha ninaushukuru uongozi mzima wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa kunisimamia na kuniongoza. Daima walikua mbele kunielekeza na kunishauri juu ya njia bora ya kufanikisha hadi kazi yangu hii kufikia hatua hii. Pia ninawashukuru wanafunzi wenzangu kwa mchango mkubwa walionipa wakati wa kufanya kazi hii ngumu. Naomba niwataje kwa majina ambao ni Mwalimu Mohamed Soud Juma, Bi Mwan-jabu Makame Ali, Bi Jina Ali Kombo na Mwalimu Ali Hassan Ali. Msaada

wao ulinitia ari na shauku wa kuikamilisha kazi yangu. Walikua wakinikumbusha wajibu wangu kuendelea na kuikamilisha kazi yangu hii.

Pia shukurani zangu za dhati zimuende Mwalimu (Ustadh) Ali Douch Seif wa Al-Madrasatul Qamariyyah kwa kuniwezesha kuikamilsha kazi yangu kwa kunipatia msaada wa kuwapata wahojiwa hasa walimu na wanafunzi wa mad-rasa. Pia nawashukuru wahojiwa wangu wote waliokubali kupoteza muda wao kujaza madodoso au kufanya mahojiano nami hadi kupatikana kwa data zilizohitajika.

Shukurani zangu maalum ziwaendee wazazi wangu wapendwa; kwanza baba yangu marehemu Bwana Suleiman Hamad Hamad na mama yangu Hadia Hamad Juma, kwa mapenzi yao, malezi mema na huruma kubwa kwangu zilizopelekea kunilea kwa uangalifu mkubwa na kunisomesha hadi kufikia elimu ya juu katika uhai wao. Namuomba Mwenyeenzi Mungu amrehemu baba yangu na amlaze mahala pema peponi. Na mama yangu ampe uhai wenye mafanikio na akimfisha amfishe kifo chema na amsamehe madhambi yake. Aamin

Nitakua mwizi wa fadhila na mchawi wa shukurani kama nitaacha kumshukuru mke wangu mpenzi Bi Laila Mshenga Mohamed na mtoto wangu mpendwa Ashraf Othman Suleiman kutokana na ustahamilivu wao mkubwa waliouonesha muda wote niliokuwa nikiwakoseha haki zao walizostahili kutokana na harakati za kufanya utafiti na uandishi wa kazi hii ngumu na yenye kuhangaisha fikra na akili.

Mwisho, nawashukuru watu wote waliotajwa na wasiotajwa kwani kwangu itakua ni vigumu kuwataja wote waliotoa msaada katika kazi hii. Nawashukuru niliowataja kwa niaba ya nisiowataja. Nyote nawaambieni Ahsanteni sana.

## IKISIRI

Utafiti huu una lengo la Kuchunguza Mabadiliko ya Kasida kwa kuchunguza fani na dhamira. Utafiti huu una malengo manne ambayo ni kubainisha kasida mbalimbali zilizosomwa katika kipindi cha baada ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kipindi kilichoshughulikiwa ni kuanzia miaka ya 1970 na wakati wa soko huria na maendeleo ya sayansi na teknolojia, kuanzia miaka ya 1990-2016, kuainisha vipengele vya fani vilivyotumika katika awamu hizo mbili, kubainisha dhamira za kasida katika awamu hizi mbili na kubainisha mabadiliko ya kifani na kidhamira kasida katika kipindi cha awamu mbili. Ili kufikia lengo kuu lililokusudiwa, mbinu za utafiti zilizohusika ni hojaji, usaili na kushiriki katika matukio ya usomwaji wa kasida. Nadharia mbili zilizoongoza utafiti huu ni nadharia ya umuundo na nadharia ya sosholojia ya fasihi na sampuli iliyotumika ni watu mia moja, kati ya hao hamsini wanawake na hamsini wanaume. Kwa upande wa matokeo ya utafiti, mtafiti aligundua kwamba kuna mabadiliko katika kasida. Mabadiliko hayo yanajitokeza katika fani na dhamira zake. Matumizi ya vifaa vya kisasa vya muziki kama vile kibodi, vinanda, nai na vipaza sauti vimebadilisha mtazamo wa kasida baada ya maendeleo ya sayansi na teknolojia. Soko huria limezifanya kasida ziwe ni biashara kuliko kushughulika na dini. Mtafiti amependekeza mambo kadhaa kwa watafiti wajao na jamii wayatupie macho na kuyafanyia kazi. Miongoni mwa mapendekezo hayo ni kuwaomba watafiti na wahakiki kujadili na kutilia mkazo uandishi wa tanzu hizi za kasida kama vinavyofafanuliwa vipengele vyengine. Walimu na wanafunzi wa mad-rasa wazingatie malengo ya kasida ili zibaki katika uhalisia wake, pia jamii zijali, kuheshimu na kuzingatia mipaka ya usomaji wa kasida

## MAELEZO YA BAADHI YA MISAMIATI ILIYOTUMIKA

| **Neno** | **Maelezo** |
|---|---|
| Tumwa | Mtume Muhammad (S.A.W) |
| Habiballah | Kipenzi cha Allah |
| Rasulillah | Mtume wa Allah |
| Rabiul-awal | Mwezi wa tatu wa Kiislamu (mfunguo sita) |
| Chumwa amini | Mtume muaminiwa |
| Suduri | Moyo |
| Rabbi | Mola mlezi |
| Sallu aley | Rehema ziwe juu yake |
| As-habu | Wafuasi wa Mtume katika zama zake |
| Muhajiri | Waislamu waliohama Makka na kuhamia Madina |
| Answari | Waislamu wa Madina waliowapokea muhajirina pamoja na Mtume (S.A.W) |
| Mukhtari | Aliyechaguliwa |

# YALIYOMO


**UTHIBITISHO** ..................................................................................... **ii**

**HAKIMILIKI** ..................................................................................... **iii**

**TAMKO** ..................................................................................... **iv**

**TABARUKU** ..................................................................................... **v**

**SHUKURANI**..................................................................................... **vi**

**IKISIRI** ..................................................................................... **viii**

**MAELEZO YA BAADHI YA MISAMIATI ILIYOTUMIKA**.......................... **ix**

**ORODHA YA MAJEDWALI** ............................................................ **xvi**

**ORODHA YA VIAMBATANISHI** ........................................................ **xvii**

**SURA YA KWANZA**.............................................................................. **1**

**UTANGULIZI** ..................................................................................... **1**

1.1 Utangulizi ..................................................................................... 1

1.2 Usuli wa Mada ..................................................................................... 1

1.3 Tatizo la Utafiti ..................................................................................... 7

1.4 Malengo ya Utafiti ..................................................................................... 8

1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti ..................................................................................... 8

1.4.2 Malengo Mahususi ..................................................................................... 8

1.5 Maswali ya Utafiti..................................................................................... 8

1.6 Umuhimu wa Utafiti..................................................................................... 9

1.7 Mipaka ya Utafiti ..................................................................................... 9

1.8 Vikwazo Vya Utafiti na Utatuzi Wake.................................................... 10

1.8.1 Upatikanaji wa Marejeleo ya Kutosha .................................................... 10

1.8.2 Upatikanaji wa Watafitiwa ........................................................................ 10

1.9 Hitimisho ........................................................................................................ 10

**SURA YA PILI ......................................................................................... 11**

**UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA NADHARIA ............. 11**

2.1 Utangulizi ........................................................................................................ 11

2.2 Utalii wa Kazi Tangulizi ................................................................................... 11

2.3 Kasida kwa Jumla ............................................................................................ 12

2.4 Historia fupi ya Kasida ..................................................................................... 12

2.5 Kasida na Uhakiki ............................................................................................ 14

2.6 Maana ya Dhana Mbalimbali ........................................................................... 14

2.7 Kipengele cha Nadharia ................................................................................... 15

2.8 Maelezo ya Dhana Muhimu .............................................................................. 17

2.9 Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi ..................................................................... 17

2.9.1 Nadharia ya Umuundo ..................................................................................... 20

2.10 Hitimisho ........................................................................................................ 21

**SURA YA TATU ........................................................................................ 23**

**MBINU NA NJIA ZA UTAFITI ................................................................ 23**

3.1 Utangulizi ........................................................................................................ 23

3.2 Mbinu Na Njia Za Utafiti ................................................................................ 23

3.2.1 Aina ya Utafiti ................................................................................................. 23

3.2.2 Eneo la Utafiti ................................................................................................. 24

3.2.3 Walengwa wa Utafiti ....................................................................................... 24

3.2.3.1 Ufafanuzi wa Aina ya Watafitiwa .................................................................. 25

3.3 Mbinu za Usampulishaji wa Data .................................................................... 26

3.3.1 Uteuzi Nasibu Kutegemea Fursa ........ 26
3.3.2 Uteuzi wa Sampuli wa Kimakusudi ........ 27
3.4.1 Sampuli za Data ........ 27
3.5 Mbinu za Ukusanyaji wa Data ........ 28
3.5.1 Mbinu ya Mahojiano ya Ana kwa Ana ........ 28
3.5.2 Mbinu ya Upitiaji wa Machapisho ........ 29
3.5.3 Mbinu ya Kushiriki katika Matukio ........ 29
3.6 Vifaa/ Zana za Utafiti ........ 30
3.6.1 Kinasa Sauti (Tepurekoda) ........ 30
3.6.2 Kompyuta ........ 31
3.6.3 Hojaji ........ 31
3.6.4 Matini ........ 32
3.7 Vyanzo vya Data ........ 32
3.8 Mpango Wa Utafiti ........ 32
3.9 Hitimisho ........ 33
**SURA YA NNE ........ 34**
**UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ........ 34**
4.1 Utangulizi ........ 34
4.2 Uwasilishaji na Uchambuzi wa Kasida ........ 34
4.3.3 Kasida za Wakati wa Msiba ........ 40
4.3.4 Kasida za Nadhiri ........ 41
4.4.2 Kasida Zinazosomwa Katika Sherehe Mbalimbali ........ 47
4.4.3 Kasida za Dua ........ 49
4.5 Uchambuzi wa Data ........ 50

4.5.1 Uchambuzi wa Data katika Vipengele vya Fani Baada ya Mapinduzi ....... 50
4.6 Matumizi ya Lugha ..... 60
4.7 Hitimisho ..... 62
4.8 Uchambuzi wa Data katika Vipengele vya Fani wakati wa Soko Huria.... 62
4.8.1 Miundo ya Kasida ..... 62
4.8.1.1 Vina na Mizani ..... 62
4.8.2 Mitindo ya Kasida ..... 66
4.8.3 Mtindo wa Kutumia Nafsi ..... 67
4.8.3.1 Nafsi ya Kwanza Wingi ..... 67
4.9 Matumizi ya Lugha ..... 67
4.9.1 Matumizi ya Tamathali ya Semi ya Sitiari ..... 68
4.9.2 Matumizi ya Ishara ..... 69
4.9.3 Matumizi ya maneno ya Lugha ya Kiarabu ..... 69
4.9.4 Matumizi ya Tash-hisi ..... 70
4.9.5 Matumizi ya Mubalagha ..... 71
4.10 Hitimisho ..... 71
4.11 Uchambuzi wa Data katika Vipengele vya Maudhui katika Wakati wa Baada ya Mapinduzi ..... 72
4.11.1 Uchambuzi wa Dhamira katika Kasida ..... 72
4.11.2 Kuwa na Tabia Njema ..... 72
4.11.3 Umoja na Mshikamano ..... 75
4.11.4 Utekelezaji wa Ahadi ..... 75
4.11.5 Wasia ..... 76
4.12 Hitimisho ..... 77

4.13 Uchambuzi wa Data za Dhamira Wakati wa Soko Huria .......................... 77
4.13.1 Umuhimu wa Kutenda Haki katika Jamii ................................................ 77
4.13.2 Sifa za Mtume.......................................................................................... 81
4.13.3 Kuwa na Tabia Njema .............................................................................. 82
4.13.4 Utekelezaji wa Ahadi ................................................................................ 83
4.13.5 Kuwaheshimu Wazazi ............................................................................... 84
4.13.6 Umuhimu wa Malezi Bora ........................................................................ 85
14 Hitimisho .......................................................................................................... 86
4.15 Uchambuzi wa Data Zilizokusanywa Maskanini...................................... 87
4.15.1 Njia za Ukusanyaji wa Data Zilivyofanikisha Lengo ............................... 88
4.15.2 Aina za Kasida ........................................................................................... 88
4.17 Dhamira za Kasida ....................................................................................... 92
4.18 Mabadiliko Katika Kasida ........................................................................... 95
4.19 Upungufu wa Ukamilifu wa Utafiti ............................................................ 99
4.19.1 Kasida nyingi hutumia lugha ya Kiarabu ................................................. 99
4.19.2 Baadhi ya Kasida Zilizosomwa na Watafitiwa Zilikuwa Fupi Mno........... 99
4.20 Hitimisho ..................................................................................................... 99
**SURA YA TANO ..........................................................................................101**
**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ................................................................101**
5.1 Utangulizi .......................................................................................................101
5.2 Muhtasari wa Tasnifu ....................................................................................101
5.3 Matokeo ya Utafiti .........................................................................................103
5.4 Nadharia za Utafiti .........................................................................................103
5.5 Mapya ya Utafiti ............................................................................................104

5.6 Hitimisho ........................................................................................105

5.7 Mapendekezo ....................................................................................106

**MAREJELEO ......................................................................................108**

**VIAMBATANISHI ...............................................................................113**

## ORODHA YA MAJEDWALI


Jedweli Na. 3.1: Aina na Idadi ya Watafitiwa ...................................................... 25

Jedweli Na 4. 1: Orodha ya Wahojiwa ................................................................ 87

Jedweli Na 4.2: Watafitiwa Wazee Wanaoeleza Aina za Kasida .......................... 88

Jedweli Na 4.3: Walimu wa Mad-Rasa Wanaozieleza Aina za Kasida ................ 89

Jedweli Na 4. 4: Wanafunzi wa Mad-Rasa Wanaoeleza Aina za Kasida ................ 90

Jedweli Na 4.5: Waandishi wa Habari Wanaoeleza Aina za Kasida ..................... 90

Jedweli Na 4.6: Walimu wa Mad-Rasa Wanaoeleza Vipengele vya Fani Katika Kasida ........................................................................................ 91

Jedweli Na 4.7: Wanafunzi Wanaoeleza Vipengele vya Fani katika Kasida ......... 92

Jedweli Na 4.8: Wazee Wanaelezea Vipengele vya Fani Katika Kasida ............... 92

Jedweli Na 4. 9: Walimu Wanaoeleza Dhamira za Kasida .................................... 93

Jedweli Na 4.10: Wanafunzi Wanaoeleza Dhamira Za Kasida................................ 94

Jedweli Na 4.11: Wasikiliza Wanaoeleza Dhamira za Kasida................................ 94

Jedweli Na 4. 12: Walimu wa Mad-Rasa Wanaoeleza Mabadiliko Ya Kasida ........ 96

Jedweli Na 4.13: Wanafunzi wa Mad-Rasa Wanaoeleza Mabadiliko ya Kasida...... 96

Jedweli Na 4.14: Waandishi wa Habari Wanaoeleza Mabadiliko Katika Kasida..... 97

Jedweli Na 4.15: Wazee Wanaoeleza Mabadiliko katika Kasida ............................ 97

Jedweli Na 4. 16: Wasikilizaji Wanaoeleza Mabadiliko katika kasida .................... 98

## ORODHA YA VIAMBATANISHI

Kiambatanishi A: Muongozo wa Maswali ya Usaili kwa Ajili ya Wanafunzi wa Mad-Rasa ....................................................................113

Kiambatanishi B: Muongozo wa Maswali ya Usaili kwa Ajili ya Walimu wa Mad-Rasa ....................................................................115

Kiambatanishi C: Muongozo Wa Maswali Ya Usaili Kwa Ajili Ya Wasikilizaji Wa Kasida ....................................................................117

Kiambatanishi D: Muongozo Wa Maswali Ya Usaili Kwa Ajili Ya Waandishi Wa Habari ....................................................................119

Kiambatanishi E: Muongozo wa Maswali ya Usaili kwa Ajili ya Wazee ..............121

Kiambatanishi F: Faharasa ya Kasida ....................................................................124

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Utangulizi

Utafiti huu una malengo manne ambayo ni kubainisha kasida zilizosomwa baada ya Mapinduzi ya Zanzibar na wakati wa Soko Huria, kuainisha vipengele vya fani vilivyotumika na vinavyotumika katika awamu hizo mbili, kubainisha dhamira za kasida zilizosomwa Baada ya Mapinduzi na Wakati wa Soko Huria na kubainisha mabadiliko ya kifani na kidhamira yaliyoingia katika kasida katika kipindi kilichotajwa. Sura hii inatoa taarifa juu ya usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, vikwazo vya utafiti na utatuzi wake.

## 1.2 Usuli wa Mada

Kasida ni miongoni mwa tungo za Kidini zinazohusishwa na Uislamu. Tungo za kasida katika jamii ya Kiislamu zimeanza zamani zikiwa na hali tafauti. Fasihi hii imekuwa ikihusisha watu wa jinsia na rika mbalimbali. Fani hii ni muhimu sana kwa Waislamu pia kwa jamii ya Wazanzibari kwa kuendeleza na kustawisha kitanzu hichi cha tungo za kishairi ndani ya fasihi simulizi.

Mazigwa (1991), amenukuliwa na Nussu (2012), mwanafasihi huumba lugha katika hali ya kuvutia na kuiweka madoido ya kila namna ili iweze kuwavutia wasikilizaji na wasomaji wake. Mwanafasihi huweza kuandika au kusimulia kwa njia ya nyimbo mambo ambayo yanafanywa na wanajamii. Mambo hayo yanaweza kuishawishi jamii kuona mambo mema na mabaya yanayotendwa na baadhi ya wanajamii kuwa

kama kero na kuyakemea kwa njia ya nyimbo kwa lengo la kuyaondoa au kuyadumisha yale yanayoonekana kuwa yanafaa kudumishwa. Chacha (1993), akimnukuu Abdalla (1976), fasihi huchimbuka na kuendelea kuishi kutokana na jamii. Anaendelea kufafanua kuwa, fasihi yoyote iwayo hupata uhai wake, miongozo yake na hata maudhui yake kutokana na hali halisi ya kiutamaduni, ya kisiasa na kiuchumi ya jamii hiyo.

Hapa Zanzibar, kasida zimekuwa ni sanaa maarufu sana katika shughuli za jamii. Kasida zina mvuto wa aina yake kwa washiriki au hadhira yake. Uzuri wake huonekana zaidi pale msomaji wake anapoonesha utaalamu wake katika kughani, kuzipangilia vizuri sauti wakati anaposoma na mpangilio mzima wa beti na mishororo katika utungaji wake. Fani na ufundi unaotumika katika kasida humsaidia msomaji kuyavuta na kuyateka mawazo na fikra za hadhira yake. Salum (2007).

Wataalamu wengi wanaelezea fasili ya neno kasida katika maandishi yao kwa uwazi. BAKIZA (2010), wanafafanua kasida ni shairi aghlabu lenye maudhui ya kumsifu Mtume Muhammad (S.A.W), kuusia au kufunza maadili mema. TUKI (2004), nao wanafafanua kuwa shairi ni utungo wa kisanaa wenye mpangilio maalum wa lugha ya mkato katika usemi, maandishi au wimbo unaoeleza wazo au mawazo, hisi au tukio juu ya maisha na ambao hufuata utaratibu wa urari na muwala maalum unaoheshimu na kuzingatia kanuni za utunzi wa mashairi unaohusika.

TUKI (2005), wameeleza kasida ni tungo maalum za kumsifu Mtume Muhammad (S.A.W) zinazosomwa wakati wa Maulid. Maulid ni kisomo maalum ambacho huelezea kuzaliwa kwa Mtume Muhammad (S.A.W) na maisha yake aliyoishi hapa

duniani. Kasida nyingi kama kasida ya Burudai na Hamziyyah zimetungwa kwa lengo la kumsifu Mtume Muhammad (S.A.W) pamoja na maisha yake aliyoishi hapa duniani.

Kasida nyengine maarufu katika historia ya kasida ni *Utenzi wa Mwanakupona*. Mdee na Mbogo (1985), wameeleza kuwa utungo huu wa Mwanakupona ni zao la fasihi ya kimwambao iliyoathiriwa na kupata utomvu wa uhai wake kutokana na utamaduni wa kimwambao ulioghoshiwa na maadili ya Ki-islam katika karne ya kumi na tisa (19). Maudhui ya tungo hizo yanaelezea dhima ya mke kwa mume wake katika jamii ya kiupwa huku maadili hayo yakiegemezwa na kuhalalishwa na dini ya Kiislamu. Kasida zilitokana na tungo za kishairi za Kiarabu hata kabla ya kuja kwa Mtume Muhammad (S.A.W) kuukamilisha Uislamu. Ushairi huu ulifika Afrika Mashariki baada ya ujio wa Waarabu katika nchi zetu.

Abobakar (2013), anaeleza kuwa Waswahili walichanganyika na Waarabu na kutokea kuunga udugu wa damu baina yao. Lugha za Kiswahili na Kiarabu zina historia ndefu sana kiasi kwamba hati za mwanzo kabisa katika kuandikia Kiswahili zilikuwa ni hati za Kiarabu-Kiswahili. (Abdulazizi (1992), Abdul-latif (1998). Kihore (2003), ananukuliwa na Abobakar (2013), anaeleza kuwa ushairi katika Kiarabu umeitwa kioo cha kweli cha maisha Uarabuni. Mashairi ya Kiarabu yanaoneshwa kuwa yalianza kabla ya Uislam. Nicholson (1969), anafafanua kuwa, kabla ya kuanza Uislamu (500-622 A.D) haya mashairi yalikuwa yameshafikia ukamilifu wa kisanaa unaofanya ushairi ufikiriwe ulianza mapema mno.

Wamitila (2003), anafafanua kuwa, utungo huu unaotokana na washairi wa Ki-arab, Ki-ajemi, Ki-turki na Ki-urdu. Anafafanua kuwa maudhui ya tungo hizi huwa ya

kimakumbukizi, kimaombolezo, kisifa au hata ya kitashtiti. Mifano mizuri ya kasida ni tungo zinazosimulia maisha na miujiza ya Mtume Muhammad ziitwazo kasida za Burudai na Hamziyya.

Mutiso (2005), anaifafanua kasida ya Hamziyyah, alieleza kuwa kasida hii ni maarufu sana katika ulimwengu wa fasihi ya dini ya Kiislamu na Waswahili huikariri wakati wa sherehe za Maulid ya Nabii Muhammad au wanapocheza Twali la Ndiya.

Hashil (1986), katika kasida yake ya "Mola alivyomjaza, Muhammad muangaza" amejaribu kuonyesha dhima za kasida za kumsifu Mtume Muhammad (S.A.W) kwa kuandika

Mwili wake umejaza, Macho yake yashangaza,
Mtume mwenye ijaza, Ujumbe atekeleza,
Amefanya miujiza, Sote anatushangaza,
Molla alivyomjaza, Muhammad muangaza.

Kasida zimeanza miaka mingi iliyopita. Wanahistoria wanatafautiana kuhusu tarehe hasa ya kuanza kwake. Wako wanaoamini kwamba, kasida zilianza pale Mtume Muhammad (S.A.W) alipohama katika mji wa Makkah na kuhamia Madina. Wakati huo watu wa Madina waliojulikana kwa jina la Answaar walijipanga katika mistari mirefu huku wakisoma kasida maarufu ya Tw'alaa L'badru ili kumkaribisha mgeni wao mtukufu katika mji wao. Wanahistoria wengine wanaamini fani hii ilianza karne nyingi za nyuma kabla ya Uislamu kukamilishwa na Mtume Muhammad (S.A.W) katika fasihi ya Kiarabu. Mutiso (2005), anafafanua kuwa, kinyume na vile

wanavyofikiri watu wengi, fani ya kasida ni ya kale sana katika fasihi ya Kiarabu na ilikuwapo hata kabla ya Mtume Muhammad (S.A.W), nabii wa mwisho wa Uislamu. Mulokozi (1996.113), anathibitisha kwamba, Uislamu ulileta mtazamo mpya na mpana zaidi kuhusu dunia na maisha na uliwaunganisha Waswahili na jumuiya pana ya umma wa Kiislamu duniani. Hivyo Waswahili nao walianza kushiriki katika utamaduni na taaluma za kilimwengu zilizokuwa zikifahamika wakati huo kupitia lugha ya Kiarabu.

Kwa upande wa kasida za Kiswahili nazo zimeanza miaka mingi iliyopita. Kasida hizo ni miongoni mwa mambo ya kale katika fasihi Simulizi ya Mswahili. Zipo kasida nyingi za zamani zilizoandikwa kwa Kiswahili kwa kutumia hati za Kiarabu. Mfano wa kasida hizo ni ile ya Hamziyyah iliyoandikwa na Aidarus. Mutiso (2005), alipokuwa anaichambua kasida hii alieleza, Kasida ya Hamziyyah ni moja wapo ya kazi za mwanzomwanzo kutungwa kwa Kiswahili cha zamani ambapo hata maneno mengine hayatumiki tena. Lugha ya Kiswahili ilianza hapo zamani, iliandikwa kwa hati za Kiarabu-Kiswahili. Mulokozi (1999), aneleza kuwa, lugha ya Kiswahili ilianza kuandikwa kwa hati za Kiarabu-Kiswahili labda katika karne ya kumi (10) au kabla.

Hata hivyo ujio wa maendeleo ya Sayansi na Teknolojia ulimwenguni kumeathiri sana fasihi katika nyanja mbalimbali ikiwamo uwanja wa kasida. Kihore na Chuwa (2004), wamefafanua kuwa, utamaduni wa kigeni ambao unazidi kuingia kwa kutumia Sayansi na Teknolojia utazidi kuziingilia jamii zetu. Kuingia kwa Sayansi na Teknolojia katika jamii zetu bila shaka kumeathiri fasihi zetu katika nyanja tafauti za kifani na kimaudhui.

Pamoja na umuhimu na mchango wake mkubwa katika jamii hii, kasida hazijafanyiwa utafiti wa kutosha hapa Zanzibar. Mtafiti ameona ni bora kuzifanyia utafiti kasida ili kuzichunguza na hatimaye kugundua kunga ambazo kasida imezifikia. Pia, mtafiti amekusudia kuchunguza vipengele vya fani na dhamira vinavyotumika katika utungaji na uwasilishwaji wake. Chacha (1992), anaeleza kuwa kazi za fasihi hujumuisha vipengele mbalimbali vya fani na maudhui na kuwa ushuhuda na ufafanuzi wa jamii. Senkoro (1972), anazidi kufafanua kuwa viko vipengele vingi vya fani katika ushairi. Amevitaja vipengele hivyo kuwa ni tamathali za semi, vina na mizani, umbo na muundo, misemo na nahau, methali, matumizi ya fumbo na tambo, mitindo, taswira, ishara, kejeli na dhihaka.  Kwa hivyo, mtafiti atachunguza fani na dhamira zililiyomo katika kasida kwa kuvichunguza na kuvichambua vipengele mbalimbali vya dhamira na fani vilivyotumika.

Kasida ni miongoni mwa vitanzu vya ushairi simulizi. Hupatikana katika kitanzu cha nyimbo katika fasihi hii. Utafiti na uhakiki wa kasida umefanywa na watafiti mbalimbali katika vipengele tafauti. Miongoni mwa watafiti waliotafiti kasida ni Salum (2007). Yeye aliangalia Nafasi ya Kasida za Kiswahili kwa Jamii ya Wazanzibari. Hata hivyo, hakutafiti wala kuchunguza mabadiliko ya kasida katika awamu mbili za maendeleo ya jamii hiyo ambazo mtafiti wa utafiti huu anakusudia kuzitafiti.

Utafiti huu umefanywa kwa lengo la kuchunguza mabadilko ya kasida kifani na kidhamira katika awamu mbili ambazo ni baada ya Mapinduzi ya Zanzibar na wakati wa soko huria. Mtafiti amechagua awamu hizi mbili kwa sababu katika kipindi hiki kuna mabadiliko makubwa ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni yaliyotokea

katika jamii. Kwa hivyo, utafiti huu umechunguza mabadiliko ya kasida katika awamu hizo kifani na kidhamira.

## 1.3 Tatizo la Utafiti

Zanzibar ni sehemun yenye maingiliano makubwa ya watu kutoka kila pembe ya dunia kwa muda mrefu. Maingiliano haya yameongezeka kutokana na maendeleo ya utandawazi duniani. Momanyi, Njogu na Mukuthuria (2012), wamemnukuu Mrikaria (2005).

Wamefafanua kuwa utandawazi ni upanukaji wa kina kirefu zaidi na usambazaji wa masafa marefu wa uhusiano miongoni mwa jamii, mintarafu, uhalisia wa maisha kuanzia yale ya ustawi wa jamii hadi yale ya harakati za kujikimu kiuchumi, kiutamaduni, kiulinzi, kibiashara, kiuwekezaji, kimawasiliano, na kiutandawazi, pamoja na jamii kuvamiwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Tatizo ni kukua kwa maendeleo ya sayansi na teknolojia na kuathiri sana kasida. Fani na dhamira za kasida zimekua zikibadilika kila uchao. Mtafiti ameamua kufanya utafiti huu ili kuchunguza ni mabadiliko gani yaliyotokea katika kasida kwa kuchunguza mabadiliko hayo katika kipindi cha baada ya Mapinduzi ya Zanzibar na wakati wa Soko Huria.

Kwa ujumla, mtafiti ameona ni bora kuchunguza kasida zimepata mabadiliko gani. Kwa kufanya hivyo ataweza kubaini endapo fani na dhamira za kasida zimebaki kama zilivyokua. Haya yatapatikana kwa mtafiti kukusanya kasida zilizosomwa katika awamu tofauti za kihistoria katika matukio mbalimbali na kuzichambua.

## 1.4 Malengo ya Utafiti

### 1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti

Utafiti huu ulichunguza mabadiliko ya kasida katika awamu mbili, ambazo ni baada ya Mapinduzi ya Zanzibar (1970-1990) na wakati wa Soko Huria (1990-2015) ili kubaini mabadiliko yanayojitokeza katika fani na dhamira katika vipindi hivyo.

### 1.4.2 Malengo Mahususi

Utafiti huu una malengo mahususi manne yafuatayo:

(i) Kurikodi na kubainisha kasida zilizosomwa katika kipindi cha awamu mbili zilizotajwa.

(ii) Kuainisha vipengele vya fani vilivyotumika na vinavyotumika katika awamu hizo mbili.

(iii) Kubainisha dhamira mbalimbali za kasida katika awamu mbili zilizotajwa

(iv) Kubainisha mabadiliko ya kifani na kidhamira yaliyoingia katika kasida katika vipindi vya awamu mbili za maendeleo ya watu wa Zanzibar.

## 1.5 Maswali ya Utafiti

(i) Je ni kasida gani zilisomwa baada ya Mapinduzi na wakati wa Soko Huria?

(ii) Ni vipengele gani vya fani vinavyojitokeza katika fasihi ya kasida katika awamu hizi mbili?

(iii) Je ni dhamira zipi zinazojitokeza katika kasida katika awamu mbili zilizoainishwa?

(iv) Jee, ni mabadiliko gani ya kifani na dhamira yanayojitokeza katika kasida za Kiswahili katika awamu mbili zilizoainishwa?

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu baada ya kukamilika unategemewa kuwa na umuhimu mkubwa hasa katika nyanja zifuatazo. Kwanza utasaidia kubainisha dhamira mbalimbali katika awamu mbili, yaani baada ya mapinduzi na wakati wa soko huria.

Pili, utasaidia kuziainisha aina mbalimbali za kasida zinazosomwa katika maisha ya kila siku.

Tatu, utasaidia kuyabaini mambo yanayofaa na yasiyofaa katika kasida kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia ulimwenguni.

Nne, utasaidia kugundua vipengele mbali mbali vya kifani na kidhamira vinavyojitokeza katika kasida ili kusaidia kuzifanya kasida ziwe bora zaidi kwa manufaa ya jamii.

Tano, ripoti ya utafiti huu itatumika kama ni marejeleo kwa watafiti wengine watakao jishughulisha na mada zinazolingana na mada hii.

## 1.7 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kuchunguza mabadiliko yaliyofikiwa na kasida hapa Zanzibar. Utafiti huu ulichunguza kasida za Kiswahili ingawa ziko kasida za lugha tofauti. Utafiti huu haukujishughulisha na kuchunguza athari za kasida katika jamii bali ulichunguza mabadiliko yake katika kipindi cha soko huria. Pia ulichambua vipengele vya fani kama vile miundo, mitindo na lugha na dhamira ili kubainisha mabadiliko katika kasida. Mtafiti alijikita katika kipindi hiki kwani ni kipindi cha mabadililko ya kisiasa na kiuchumi yaliyopelekea mabadiliko ya kijamii Zanzibar.

## 1.8 Vikwazo Vya Utafiti na Utatuzi Wake

Hornsby (2000), anatoa maana ya kikwazo kuwa ni hali au tukio au kitu chengine ambacho kitamfanya mtafiti apate ugumu katika kufanya au kulifikia jambo. Vikwazo vya utafiti ni jumla ya mambo yote ambayo kwa njia moja au nyengine yanasababisha utafiti usifanikiwe kwa kiwango kifaacho. Katika kukamilisha utafiti wake mtafiti alikukutana na vikwazo vifuatavyo:

### 1.8.1 Upatikanaji wa Marejeleo ya Kutosha

Zanzibar bado hakujawa na maktaba za kutosha zenye marejeleo ya kutosha yaliyomwezesha mtafiti kusoma na kufahamu vyema kuhusu mada yake. Mtafiti ili kutatua tatizo hili alijitahidi kutafuta marejeo kwenye intaneti na mitandao mengine. Pia alisafiri mara kwa mara ili kujisomea maktaba zilizopo huko Dar es Salam ili kukamilisha kazi yake kwa wakati uliofaa.

### 1.8.2 Upatikanaji wa Watafitiwa

Watafitiwa wengi ni watu ambao hawakujua umuhimu wa utafiti. Kwa sababu hiyo watafitiwa wengine hawakushiriki vyema katika kutoa data zilizohitajika kwa muda uliotakiwa. Mtafiti alijitahidi kutoa elimu kwa watafitiwa juu ya umuhimu wa utafiti huu kwa jamii katika kuziendeleza kasida kwa manufaa ya jamii.

## 1.9 Hitimisho

Katika sura hii ya kwanza, vipengele vilivyokusanywa ni pamoja na usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, lengo kuu la utafiti, malengo mahsusi, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na mwisho vikwazo na utatuzi wake. Sura inayofuata itachunguza utalii wa kazi tangulizi na mkabala wa nadharia.

# SURA YA PILI

# UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inahusu utalii wa machapisho ya kazi tangulizi zilizopata kufanyiwa utafiti ambazo zilizungumzia mada inayofanana au kukaribiana na mada iliyofayiwa utafiti. Kazi zilisomwa na kupembuliwa. Upembuzi huo ulizingatia vipengele vilivyohusu maana ya kasida, maana ya maulidi, nadharia mbalimbali, historia ya kasida, vipengele vya fani na dhamira za kasida, na sehemu ya mwisho ni hitimisho. Pia kipengele cha mkabala wa nadharia kimeonyeshwa na kuchambuliwa katika sura hii. Mtafiti alizisoma kazi hizo ili kupata taarifa juu ya mada anayoitafiti. Taaluma aliyoipata mtafiti ilimuongoza katika kufanikisha utafiti wake.

## 2.2 Utalii wa Kazi Tangulizi

Creswell (2009), anaeleza utalii wa kazi tangulizi ni uchaguaji na ufupishaji wa utafiti kuhusu mada. Anaendelea kueleza kuwa, hutoa muundo na kuonesha umuhimu kwa kulinganisha matokeo na utafiti mwengine. Mtafiti huhitajika kusoma kazi mbalimbali zinazohusu mada yake ili kugundua watafiti na waandishi watangulizi wameandika nini kuhusu mada anayoifanyia utafiti. Mtafiti amejisomea maandishi mbalimbali na vyazo vyengine vya taarifa kama vile mitandao ili kuzichunguuza na kuzisoma pamoja na kuzihakiki kazi mbalimbali zinazohusu utafiti wake. Mtafiti amesoma vitabu, majarida, masimulizi, makala na ametembelea vyombo vya habari pamoja na mitandao inayohusu mada yake. Katika kazi hizi ameona mifumo ya uandishi wa utafiti, kanuni za uandishi, mpangilio wa utafiti na

kapata taaluma mbalimbali zinazohusu utafiti wake. Kazi alizozitalii na kuzisoma mtafiti zilimsaidia katika kukamilisha utafiti wake.

### 2.3 Kasida kwa Jumla

Katika sehemu hii mtafiti alisoma kazi tangulizi kuhusiana na mada ya utafiti wake ambayo ni kuchunguza mabadiliko ya kasida. Lengo ni kugundua watafiti waliotangulia wamezungumzia mambo gani kuhusiana na mada ambayo utafiti huu unakusudia kuitafiti. Utanzu huu ni miongoni mwa sanaa za zamani na watafiti wengi wameufanyia utafiti. Mutiso (2005:5) anaeleza tukiipitia kasida ya Hamziyyah tunapambana na maneneo mengi ya zamani ya Kiswahili. Maneno haya hayapatikani katika makamusi ya kisasa. Zipo kasida zilizotungwa na kusomwa tokea wakati wa Mtume Muhammad (S.A.W) labda katika karne ya saba au nane. Kutokana na ukweli huu ni dhahiri kuwa, kuna umuhimu wa sanaa hii kufanyiwa utafiti ili kugundua mabadiliko yaliyotokea ndani yake kwa kuchunguza miundo na vipengele vyengine vya fani pamoja na dhamira zake. Mtafiti aliwahoji na kuzungumza na watu wa rika mbalimbali ili kupata habari za kina kuhusu utanzu huu. Taarifa hizo zilimsaidia kuihuisha na kuifanya kazi hii iwe bora zaidi.

### 2.4 Historia fupi ya Kasida

Wapo watafiti kadhaa waliowahi kutafiti na kuandika kuhusu kasida kwa shabaha na madhumuni mbalimbali, miongoni mwao ni Mutiso (2005), ambae ameandika kuhusu kasida ya Hamziyyah. Ameeleza kuwa kasida hii ni miongoni mwa kazi za mwanzoni za fasihi ya Kiswahili. Amefafanua mambo mbalimbali kama vile historia ya utenzi huo huku akiwataja waandishi wake. Maandishi ya muandishi huyo

yalimsaidia mtafiti kuelewa asili na historia ya kasida za Kiswahili ulimwenguni. Anaendelea kuelezea lengo la kasida hiyo kuwa ni kumsifu Mtume Muhammad (S.A.W).

Mulokozi (1999) amezitafiti *Tenzi Tatu za Kale* ambazo ni utenzi wa Fumo Liyongo wa Muhamed Kijumwa, Al-Inkishafi wa Sayyid Abdalla bin Ali na Utenzi wa Mwanakupona wa Mwanakupona binti Mshamu. Tenzi hizi zinasemekana kuwa zilitumika kama kasida katika shughuli mbalimbali za kijamii. Mwandishi ameeleza historia ya tenzi hizo na umuhimu wa kila moja katika jamii. Katika kitabu chake ameandika na kufafanua jinsi fasihi ya Kiswahili ilivyokuwa katika miaka ya nyuma katika karne ya kumi na sita (16) na kumi na saba (17). Mawazo yake yalimsaidia mtafiti kuelewa fasihi za mwanzo za Kiswahili na mambo iliyoyazungumzia ikiwamo kasida. Mtafiti mwengine aliyejihusisha na kasida ni Salum (2007), ambaye aliandika kuhusu nafasi ya kasida za Kiswahili kwa jamii ya Wazanzibari. Amefanya utafiti wake akiwa katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA). Katika tasnifu yake, pamoja na mambo mengine amezitaja kasida mbalimbali ikiwamo kasida za zamani za Hamziyyah, Burduai na utenzi wa Rasul-Ghuli. Pia anafafanua nafasi ya kasida za Kiswahili kwa jamii ya Wazanzibari. Utafiti huu ulimsaidia mtafiti kuendelea na lengo lake la utafiti kwani alipata kuona na kufahamu pengo la maarifa lililoachwa na mtafiti. Hii ni kwa sababu mtafiti huyu ameonyesha nafasi ya kasida za Kiswahili kwa Wazanzibari lakini hakueleza maendeleo ya kasida wala hakujihusisha na mabadiliko ya kifani na kidhamira katika sanaa hii. Pia mtafiti huyu hakuchambua vipengele vya fani wala vya dhamira katika utafiti wake. Hashil (1986), na Sengo (2010), wameandika kasida mbalimbali za kumsifu Mtume

Muhammad (S.A.W) pamoja na kufunza maadili katika jamii. Kasida hizi ni muongozo mzuri katika kufanikisha utafiti huu kwani zimeonesha baadhi ya maudhui ya kasida. Pia mtafiti alipata mifano halisi ya kasida ambapo zilimsaidia kukamilisha kazi yake kwa sababu kasida walizoziandika zimempa muongozo wa kuona miundo yake na kubaini fani iliyotumika na dhamira zilizomo.

## 2.5 Kasida na Uhakiki

Kasida ni sanaa ya zamani ambayo kwa kiasi kikubwa inahusishwa na dini ya Kiislamu. Utafiti na uhakiki kuhusu sanaa hii umefanywa na wataalamu kadhaa. Miongoni mwa wahakiki waliojishughulisha na uchunguzi na uhakiki wa kasida ni Mutiso (2005), alieichambua kasida ya zamani iliyojulikana kama kasida ya Hamziyyah. Kasida hii iliandikwa kwa hati za Kiarabu zikisomeka kwa lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, kasida za Kiswahili hazijafanyiwa uhakiki wa kutosha hapa Zanzibar. Wataalamu wengi wamejishughulisha na uchambuzi wa kasida za kale tu na huku kasida zinaendelea kutungwa na kusomwa kila siku katika jamii zetu. Mtafiti anatarajia utafiti huu utatoa mchango kwa watafiti na wahakiki wa kazi za fasihi kuitupia jicho la karibu sanaa hii na kutambua mabadiliko yake ili iweze kuwa bora zaidi.

## 2.6 Maana ya Dhana Mbalimbali

BAKIZA (2010), TUKI (2004), na TUKI (2005), wanatoa fasili ya dhana zinazohusu mada hii ya utafiti. Dhana zenyewe ni kama kasida, maulid na nadharia.. Wanafafanua kuwa, kasida ni tungo maalum zinazosomwa kwa lengo la kumsifu Mtume Muhammad (S.A.W) katika sherehe za maulid. Wanaeleza kuwa maulid ni

kisomo maaalum ambacho hueleza kuzaliwa kwa Mtume Muhammad (S.A.W) pamoja na maisha yake aliyoishi hapa duniani. Maana walizozitoa wataalamu hawa ni muhimu katika utafiti huu ingawa zina upungufu. Kasida zimekuwa na maana pana zaidi, ambapo pia, hutumiwa na jamii katika kufunza maadili na mambo mema mbalimbali. Pia, kasida zinatumka kama sanaa inayoburudisha katika sherehe mbalimbali za kijamii kama vile harusi na hata sherehe za kiserikali kama ufunguzi wa miradi ya maendeleo katika jamii.

TAKILUKI (1981), wanagusia misingi ya nadharia za fasihi, pia wanaeleza historia ya fasihi na jinsi inavyokuwa katika nyanja mbalimbali. Wanafafanua kuwa, fasihi hufuata mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi na kijamii katika jamii inayohusika. Mawazo na fikra za wataalamu hawa ni muhimu sana katika kumuwezesha mtafiti kuukamilisha utafiti wake kwa, sababu wametufafanulia fasili ya dhanna mbalimbali zitakazotumika katika utafiti wake.

## 2.7 Kipengele cha Nadharia

Hornsby (2000), anaeleza maana ya nadharia kuwa ni mpangilio wa mawazo ambayo yanatarajiwa kuelezea sababu ya kutokea au kuwapo kwa kitu fulani. Njogu na Chimerah (1999), wanagusia kipengele cha nadharia katika uhakiki wa kazi za fasihi. Wanafafanua kuwa, nadharia inatusaidia kuona uhusiano baina ya matukio na wahusika au matumizi ya lugha na maana ya kile tunachokisoma na tunachokisikia. Nadharia zinatoa mwangaza na kuweka wazi kilichojificha katika kazi za fasihi. Mawazo ya wataalamu hawa ni muhimu kwani yalimsaidia mtafiti kupata ufafanuzi na uchambuzi juu ya umuhimu wa kutumia nadharia zinazofaa katika kukamilisha

kazi yake. Ingawa waandishi hawa hawakueleza chochote kuhusu mabadiliko ya kasida Zanzibar, lakini mawazo yao yalimsaidia mtafiti kwa upande wa uchaguzi wa mkabala wa nadharia unaofaa katika utafitit wake. Mawazo ya watafiti hao yalimuwezesha mtafiti kuchagua na kutumia nadharia zilizoendana na utafiti wake kwani si kila nadharia inaweza kutumika kwa kila utafiti. Mtafiti anahitajika kuchagua nadharia inayofaa kutokana na mada na malengo ya utafiti wake.

Ntarangwi (2004), Wamitila (2002), Wamitila (2004), wao wamezifafanua nadharia mbalimbali kama vile nadharia ya sosholojia, nadharia ya umuundo na nadharia ya Kimarx. Nadharia hizo zinaeleza mambo mbalimbali zikiwamo sababu zinzosababisha mabadiliko katika jamii ambazo huwa ni mabadiliko na maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Senkoro (1987), anaeleza fasihi ilibadilika kulingana na mabadiliko ya mifumo. Anataja mfumo wa ujima, kipindi cha ushujaa, mfumo wa kitumwa, kimwinyi, kijamaa na mfumo wa kibepari. Senyamanza (2015), anagawa vipindi vya mabadiliko kulingana na maendeleo ya jamii. Anagawa awamu ya kabla na wakati wa ukoloni, kipindi cha uhuru miaka ya 1960 hadi 1967, kipindi cha Azimio la Arusha miaka ya 1967 hadi 1987 na kipindi cha mfumo wa Soko Huria kuanzia 1988. Wanandharia wanazichambua nadharia hizo kwa kina na kueleza umuhimu wake katika fasihi. Mawazo ya wataalamu hawa yalimpatia mtafiti mwangaza mzuri wa kuelewa na kuchambua mkabala wa nadharia ambao ni sehemu muhimu katika utafiti huu. Katika kazi zao amezigundua nadharia nyingi, amezisoma na kuzifahamu vyema. Mtafiti amepata nafasi ya kuzichagua chache ambazo ameona zinaweza kumsaidia katika kukamilisha kazi yake. Pia wataalamu hawa wanaeleza historia na wanachambua kazi zinazofanywa na nadharia hizo. Uchambuzi wa kazi

zao utamuwezesha mtafiti kuchagua nadharia zinazoendana na utafiti wake kama vile nadharia ya sosholojia ambayo inachambua vipengele vya maudhui katika kazi za fasihi na nadharia ya Kimuudo ambayo inatumika kuchambua vipengele vya fani. Nadharia ya kisosholojia ilimsaidia mtafiti katika kuchambua vipengele vya maudhui kama vile dhamira na nadharia ya umuundo ilimsaidia kuchunguza vipengele vya fani ambavyo ni muundo, mtindo na lugha katika utafiti huu. Nadharia hizo zilimsaidia mtafiti kwani zimechambua maendeleo ya fasihi katika jamii katika nyanja za kisiasa, kijamii, kiutamaduni na kiuchumi. Mabadiliko katika kasida yamesababishwa na maendeleo ya jamii ya kisiasa na kiuchumi kama inavyofafanuliwa katika nadharia ya sosholojia ya fasihi. Mtafiti aliyatumia mawazo yao kuchunguza mabadiliko ya kasida Zanzibar katika awamu zilizotajwa.

## 2.8 Maelezo ya Dhana Muhimu

Wamitila (2004), anaeleza fasili ya dhanna ya nadharia kuwa ni mawazo, dhana au maelezo yanayotolewa kueleza hali fulani, chanzo chake, muundo wake, utendakazi wake na muingiliano wake wa ndani na nje. Wamitila (2003:161) anafafanua kuwa nadharia ni sayansi au sanaa inayohusika na kanuni za kijumla na mikabala fulani au hata kanuni fulani zinazotumiwa katika uchunguzi wa suala fulani. Katika utafiti na uchunguzi wa kazi za fasihi, zipo nadharia mbalimbali ambazo zinaweza kutumika kuchunguza na kuchambua kazi za fasihi. Hapa mtafiti alichunguza na kuchambua nadharia tafauti na hatimae kuchagua zilizomfaa katika kukamilisha kazi yake.

## 2.9 Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi

Miongoni mwa waasisi wa nadharia hii ni Mmarekani Adam Smith mnamo mwaka 1970. Mwananadharia huyu anaeleza kwamba, nadharia hii imejikita zaidi katika

kuangalia uhusiano wa mwanadamu na mazingira yake. Maherey (1978), Eaggleton (1983), kama walivyonukuliwa na Wamitila (2003), wanaeleza kuwa, wahakiki wa kisosholojia wanaamini kuwa, kazi ya kifasihi inadhibitiwa na muundo wa kijamii, kiuchumi na kisiasa. Pia wahakiki hawa wanaamini kuwa, jinsi wasomaji wanavyoipokea, kuitathmini na kuihukumu kazi fulani huathiriwa pia na mazingira ya wasomaji hao kiwakati na kimahali. Msokile (1992), anaendelea kufafanua kuwa nadharia ya sosholojia huikabili kazi ya fasihi kwa kuangalia jinsi inavyohusiana na mazingira ya kijamii. Nadharia hii inaamini kuwa uhusiano wa kazi ya kifasihi na jamii ambayo kazi hiyo imeandikwa ni muhimu sana. Anaendelea kufafanua kuwa, sanaa haijengwi katika ombwe, ni kazi ya mwandishi katika mazingira na wakati maalum akiwajibika kwa jamii inayomuhusu ambayo ni sehemu yake muhimu. Msokile (1993.4), anazidi kufafanua kuwa mkabala huu kimsingi hutawaliwa na imani kuwa uhusiano kati ya kazi ya kifasihi na jamii ambayo kwayo kazi hiyo imeandikwa ni muhimu sana. Mhakiki wa kisosiolojia au kihistoria huiweka kazi yake katika ulimwengu wa kijamii na halafu huelezea uhusiano uliopo kati yake. Kama uhusiano ni mdogo basi tathmini juu ya ubora ama udhaifu hufuata. Mazingira ya jamii ndio huweza kubadili maudhui ya kazi ya fasihi.

Nadharia hii ilitumika katika utafiti huu kwa sababu kasida zinazosomwa hutegemea maendeleo fulani ya kiuchumi na kijamii katika jamii inayohusika. Chacha (1992), akimnukuu Abdalla (1976), anaeleza kwamba, hakuna fasihi hata moja ulimwenguni ambayo imechimbuka na kuendelea kuishi katika ombwe tupu. Fasihi yoyote iwayo itakuwa imeupata uhai wake, miongozo yake na hata maudhui yake kutokana na hali ya kiutamaduni, kisiasa na kiuchumi ya jamii hiyo iliyochimbukana nayo. Senkoro

(1988), anasisitiza kuwa fasihi hupata uhai wake kutokana na hali halisi za jamii kama vile za uchumi, siasa na utamaduni kwa jumla. Anaeleza kuwa misingi na mikondo ya historia ya jamii huipa fasihi umbo kimaudhui na kifani, huipa uhai na welekeo. Kwa mfano tukiangalia usomwaji wa kasida kabla ya mapinduzi tutaona kuwa ni tafauti na usomwaji wake baada ya mapinduzi na wakati wa soko huria na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Hii ni kwa sababu katika kipindi hiki jamii hii imepata maendeleo ya kisiasa, kijamii kiutamaduni na kiuchumi.

Mabadiliko haya ya kijamii na kiuchumi yamebadilisha mifumo ya fasihi katika jamii. Pia ilitumika kwa sababu, kasida ni miongoni mwa mambo ya kijamii na kidini ambayo huendelea kutokana na maendeleo ya jamii, kwa hivyo zinategemea sana mazingira ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Nadharia hii ilimsaidia mtafiti kuchunguza dhamira zilizomo katika kasida. Udhaifu wa nadharia hii ni kuwa, huchunguza maudhui tu katika kazi za fasihi wala haijihusushi na vipengele vya fani. Nadharia hii imetumiwa na watafiti mbalimbali. Miongoni mwa watafiti hao ni Makallo (2014), ameeleza kuwa kazi ya mwanasosholojia ni kuielewa jamii ambapo huangalia uhusiano wa jamii katika mienendo yao ya kila siku.

Kwa hivyo, mtafiti wa utafiti huu anategemea kuangalia mienendo na mazingira ya jamii ya Wazanzibari ambayo imeleta mabadiliko na maendeleo mballimbali katika kasida katika awamu mbili zilizotajwa katika utafiti huu. Nadharia hii haitasaidia katika uchambuzi wa vipengele vya fani katika kazi hii. Hivyo mtafiti alitumia nadharia ya umuundo ambayo ilichambua fani ili kuweza kuchambua vipengele hivyo kwa urahisi.

### 2.9.1 Nadharia ya Umuundo

Wamitila (2003), anaieleza nadharia ya umuundo kuwa hutumiwa kuelezea aina ya uhakiki ambayo inachunguza kaida zilizopo katika uundwaji wa kazi fulani. Ukuaji wa nadharia ya uumundo inahusiana na isimu kwa kiasi kikubwa. Mawazo ya mwanaisimu wa ki-Swizi, Ferdinand de Saussure yalikuwa na athari kubwa katika ukuaji wa nadharia hii. Umuundo ulizagaa zaidi katika miaka ya 1950. Mtazamo wa isimu kama mfumo au muundo unaathiri uhakiki wa kimuundo na inaiona kazi ya kifasihi kama muundo. Umuundo unatilia mkazo kwenye muundo wa kazi ya fasihi.

Wafuasi wa umundo wanaamini kuwa kazi ya fasihi haina urejelezi wa nje. Kutokana na urejelezi huu kazi hiyo inaishia kutufanya tuiwazie hali yake ya lugha. Maoni yao ni kuwa neno halihitaji urejelezi ili lipate maana. Mkabala huu huiangalia lugha kama mfumo unaojitosheleza. Mfumo huu hautegemei kusudi la msemaji au wa wasemaji (muandishi au waandishi). Ulimwengu wa nje au wa kiurejelezi au hata mfasiri hauna mchango mkubwa katika kuzaa maana ya kazi. Umuundo humpuuza muandishi katika uhakiki wake ili kufichua au kuweka wazi mfumo au harakati za kiuashiriaji ambazo zinatokea katika kazi hii. Mulokozi (1989), anafafanua kuwa umuundo ni nadharia inayojibainisha kwa kuangalia ujumla wa uhusiano wa sehemu moja kwa nyengine katika kufanya kitu kizima. Katoa mfano wa muungano wa maneno katika kuunda sentensi.

Kwa wahakiki wa kimuundo viashiria vina maaana na uzito mkubwa kuliko viashiriwa. Hii ina maana kuwa mhakiki wa kimuundo anaelekea kuvutiwa zaidi na jinsi maana inavyozushwa au kukuzwa kuliko na maana yenyewe. Hata hivyo wana umuundo hawaimuliki maana ya kazi kama wanavyofanya wanauhakiki mpya.

Umuundo unatilia mkazo miundo ya kiuashiriaji katika kazi ya kifasihi. Mkabala huu hupuuza masuala yanayohusiana na yaliyomo na maudhui ya kazi fulani. Kwao kazi ya kifasihi huwa ni udhihirishaji wa muundo wa kijumla. Udhihirishaji huu hua ni aina moja tu ya mawezekano mbalimbali. Nadharia hii huweka mkazo mkubwa kwenye unasibishi wa maana. Maana nasibishi ya neno ni maana inayohusishwa na neno hilo wala sio kile kinachorejelewa. Nadharia hii ni bora katika kuangalia miundo mbalimbali ya kazi za kifasihi. Udhaifu wa nadharia hii ni kwamba, nadharia hii hushughulikia vipengele vya fani tu na haijihusishi na vipengele vya maudhui.

Mtafiti alitumia nadharia hii katika kutafiti na kuchambua vipengele mbalimbali vya fani ambavyo havitaweza kushughulikiwa na nadharia ya sosholojia ya fasihi. Ilimsaidia mtafiti kuchambua vipengele vya nje visivyokuwa vya dhamira. Nadharia hii ya umuundo itashirikiana na ile ya sosholojia ambayo itahusika na kuchunguza maudhui ya kazi ya kifasihi. Kwa vile utafiti huu utahusisha uchunguzi wa fani na dhamira, mtafiti ilimlazimu atumie nadharia zote mbili ili kukamilisha kazi yake kwani hakuna nadharia hata moja kati ya hizi mbili iliweza kumfikisha mtafiti katika lengo lake.

## 2.10 Hitimisho

Katika sura hii ya pili mtafiti amechambua kwa kina maandishi yaliyoandikwa na watafiti na wahakiki wa kazi za fasihi tangulizi yanayohusiana na mada ya utafiti. Ambapo waandishi tangulizi wamegusia maana ya kasida, historia ya kasida, uhakiki wa kasida, vipengele vya fani na dhamira, mchango na athari za utandawazi katika fasihi. Na mwisho wa sura hii ufafanuzi wa mkabala wa nadharia zilizotumika katika

utafiti huu ulijadiliwa na kuonesha ni kwa kiasi gani ulivyoweza kufanikisha lengo la utafiti huu. Sura inayofuata itaonesha mbinu na njia za utafiti zilizotumika.

# SURA YA TATU

# MBINU NA NJIA ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inahusu kipengele cha mbinu na njia za utafiti ambazo zilitumika katika ukusanyaji na uchambuzi wa data. Mbinu mbalimbali zilitumika kama vile mbinu za kutumia miongozo ya usaili, matini, mahojiano, hojaji na kushiriki katika matukio yaliyoambatana na usomaji wa kasida. Pia sura hii imefafanua aina ya utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, usampulishaji, vifaa vya utafiti na vyanzo vya data. Mbinu hizi na njia zimemsaidia mtafiti katika kufanikisha malengo ya utafiti.

## 3.2 Mbinu Na Njia Za Utafiti

Mbinu na njia za utafiti ni utaratibu anaoutumia mtafiti ili kumuwezesha kufikia lengo lake. Mwaipopo (1999: 67), anaeleza mbinu za utafiti kuwa ni ule mpango ambao data hukusanywa, uteuzin hufanywa na data huchambuliwa na kutafsiriwa. Kwa hivyo ni kazi ya mtafiti kuteua mbinu na njia bora za utafiti kulingana na mada anayoifanyia utafiti pamoja na malengo ya utafiti huo ili aweze kukusanya data kwa urahisi. Mtafiti katika kufikia lengo lake alitumia mbinu mbalimbali za utafiti kama zifuatazo.

### 3.2.1 Aina ya Utafiti

Utafiti huu ni utafiti wa kusoma tatizo “case study”. Kothari (2004:113) anaeleza kuwa mbinu hii inajumuisha uchunguzi makini na kamili wa jamii, ikiwa ni mtu mmoja, familia, taasisi, kikundi cha kiutamaduni au hata jamii nzima. Anafahamisha kuwa mtafiti anaweza kuchukua taasisi moja ya kijamii au zaidi kwa ajili ya utafiti

wake. Mbinu hii ilitumika kwa sababu mtafiti alichunguza tatizo moja tu ambalo ni maendeleo ya kasida katika jamii ya Wazanzibari inayohusika katika vipindi vilivyoteuliwa.

### 3.2.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika Zanzibar, katika kisiwa cha Unguja, Mkoa wa Mjini Magharibi katika Wilaya ya Magharibi. Katika eneo hili hupatikana watu kutoka sehemu mbalimbali za hapa visiwani na maeneo mengine kwa sababu ni eneo lenye waislamu wengi, ni eneo linalofikika kwa wepesi, pia wasomaji na wapenzi wengi wa kasida hupatikana katika eneo hilo. Shughuli nyingi zinazohusisha usomaji wa kasida hupatikana katika eneo hili. Ni rahisi kwa mtafiti kulifikia eneo hili kwani ni eneo linalofikika kwa urahisi. Pia ni eneo ambalo watafitiwa wanaweza kupatikana kwa urahisi. Kwa hiyo ilikua ni rahisi kwa mtafiti kukamilisha kazi yake kwa kuwapata walengwa wa utafiti kwa wakati uliotarajiwa.

### 3.2.3 Walengwa wa Utafiti

Walengwa wa utafiti huu ni walimu wa madrasa, wanafunzi wa madrasa, wazee, wapenzi wa kasida na waandishi wa habari wa vyombo vinavyojishughulisha na uandaaji na urushaji wa vipindi vya kasida. Watafitiwa hawa waliweza kutoa taarifa zilizohitajika katika utafiti huu. Watafitiwa ni sehemu ya jamii ya watu au vitu fulani iliyochaguliwa ili itoe taarifa zitakazokuwa kiwakilishi cha jamii nzima, Kothari (2009). Katika utafiti huu, watafitiwa walikuwa ni wazee waliojishughulisha na kasida, walimu wa mad-rasa, wanafunzi wa mad-rasa, waandishi wa habari wa vyombo vinavyojishighulisha na kasida na wapenzi wa kasida. Mtafiti aliwatumia watafitiwa wa rika na jinsia zote ili kurahisisha upatikanaji wa data za matukio na

nyakati mbalimbali kwa urahisi na uhakika zaidi. Watafitiwa hawa walikuwa 100 na waliteuliwa kama ifuatavyo.

**Jedweli Na. 3.1: Aina na Idadi ya Watafitiwa**

| Namba | Aina Ya Watafitiwa | W'ke | W'me | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Wazee | 10 | 10 | 20 |
| 2. | Walimu Wa Mad-Rasa | 10 | 10 | 20 |
| 3. | Wanafunzi Wa Mad-Rasa | 10 | 10 | 20 |
| 4. | Waandishi Wa Habari | 10 | 10 | 20 |
| 5. | Wapenzi Wa Kasida | 10 | 10 | 20 |
| **6.** | **Jumla** | **50** | **50** | **100** |

### 3.2.3.1 Ufafanuzi wa Aina ya Watafitiwa

(i) Wazee walisaidia kupatikana kwa data za miaka iliyopita kwa mfano miaka ya thamanini. Hii ni kwa sababu wao ndio walioishi katika wakati huo na ndio wenye data za uhakika za wakati huo kuliko vijana ambao hawakuishi katika wakati huo.

(ii) Walimu wa mad-rasa hujishughulisha katika utungaji, usimamizi wa usomaji wa kasida na hata uwasilishaji wake. Waliweza kutoa taarifa juu ya matukio yanayowasukuma kutunga kasida tafauti katika wakati tafauti na matukio tafauti.

(iii) Wanafunzi wa mad-rasa ndio wasomaji wakubwa wa kasida katika hafla na matukio mbali mbali. Walieleza kasida wanazozisoma zinakua na miundo gani na dhamira gani zinayokusudiwa kufikishwa kwa jamii katika nyakati tafauti.

(iv) Waaandishi wa habari wa vyombo mbalimbali hurusha kasida katika vyombo vyao. Hawa huzipangilia kasida katika matukio na muktadha unaohusika. Kwa

mfano tunaona kasida zinazosomwa katika mwezi wa Ramadhani ni tafauti na zinazosomwa miezi mengine. Hili lilimsaidia mtafiti kukusanya kasida za matukio tafauti na zenye maudhui tafauti zilizosomwa katika nyakati mbalimbali.

(v) Wapenzi wa kasida nao huzisikiliza kasida na hushiriki katika matukio yanayoambatana na usomwaji wa kasida. Wataweza kueleza mambo yanayowavutia katika kasida kama kuna mabadiliko. Haya yalimsaidia mtafiti katika uchambuzi wake wa vipengele mbalimbali vya fani na dhamira kutokana na data walizozitoa.

## 3.3 Mbinu za Usampulishaji wa Data

Usampulishaji anaueleza Sanga (1999:67), kuwa ni njia ya kuchagua idadi ya watu inayohitajika katika utafiti kutokana na pupulesheni kubwa. Lewis (2012), anafafanua kuwa, usampulishaji unahitajika kwa sababu mtafiti hawezi kuchunguza na kurikodi kila kitu kinachotokea katika utafiti. Jamii inyofanyiwa utafiti huwa ni kubwa ambapo kwa mtafiti si rahisi kuishughulikia yote. Kwa hivyo mtafiti hutakiwa kutumia mbinu zitakazomuwezesha kupata sampuli itakayowakilisha jamii inayofanyiwa utafiti.

### 3.3.1 Uteuzi Nasibu Kutegemea Fursa

Vaus (2001:90), anaeleza kwamba, uteuzi nasibu kutegemea fursa kuwa ni aina ya usampulishaji ambayo kila mtu ana fursa sawa au angalau inayojulikana ya kuteuliwa. Kaendelea kueleza kuwa njia sahihi kabisa ya kupata aina hii ya sampuli ni kutumia uteuzi bila ya kuchagua muhsika katika populesheni inayojulikana.

Uteuzi huu ulipunguza upendeleo wa kuwapata watafitiwa. Morrison (2011), anaeleza faida na ubora wa njia hii kuwa, uteuzi nasibu kutegemea fursa huwa hauna upendeleo katika kuwapata watafitiwa. Pia Babie (1999), anafafanua, kwa kutumia njia hii mtafiti ataweza kulinganisha majibu ama data alizopewa na watafitiwa hao ili kuona uhusiano wake. Mbinu hii ilimsaidia mtafiti kupata data kutoka kwa watafitiwa tafauti bila ya upendeleo. Hivyo watafitiwa wa rika tafauti na jinsia tafauti na hivyo kupata data za kutosha kuhusu mada yake.

### 3.3.2 Uteuzi wa Sampuli wa Kimakusudi

Wamitila (2004), anaeleza kuwa kinachomoungoza mtafiti katika mbinu hii ya utafiti ni kuwa, katika uteuzi huu wa sampuli, mtafiti huwa na sababu fulani maalum alizonazo. Kwa mfano anaweza kuteua kundi au sehemu fulani ya watafitiwa kwa sababu ni rahisi kwenda huko, akapajua vizuri, mdhamini wake anapopapendelea n.k. Mtafiti alitumia mbinu hii ili aweze kuteua kundi linalofaa kulingana na urahisi utakaopatikana katika kuteua watafitiwa wa utafiti wake. Pia ilimsaidia kuteua sampuli inayofaa ili aweze kupata data anazozitaka. Kwa mfano mtafiti alichagua wazee katika sampuli yake ili afahamu vipengele vya fani na maudhui yaliyoainishwa katika kasida kipindi kilichopita na kupata historia ya kasida katika jamii inayohusika, wapenzi wa kasida walisaidia kutoa data zilizohitajika katika kipindi hiki cha mabadiliko ya kijamii kisiasa, kiuchumi na hata kiutamaduni.

### 3.4.1 Sampuli za Data

Babie (1999), anafafanua kuwa sampuli ni kikundi kidogo cha watafitiwa kilichochaguliwa katika populesheni kubwa ambayo ndiyo hutoa data za kuwakilisha kundi zima linalotafitiwa. Sampuli ni kikundi cha vitu au watu kilichochaguliwa kwa

utaratibu maalum ili kitumike katika utafiti. Hii ni kwa sababu sio rahisi kwa mtafiti kutafiti kundi zima kwa wakati mmoja. Babie (1999) anaweka wazi kuwa ni vigumu kwa utafiti kushughulikia idadi kubwa ya wanajamii wanaohusika katika utafiti hata kama anavutiwa na wanajamii hao. Mtafiti hutakiwa kuchagua idadi maalum ya wanajamii wa kuwashughulikia katika utafiti wake. Idadi hiyo ya wanajamii huitwa wanajamii lengwa. Mtafiti katika kukamilisha kazi yake aliteua kundi la wahojiwa ili awahoji maswali mbalimbali yanayohusu utafiti wake. Wahojiwa katika utafiti huu ni wanafunzi wa mad-rasa, walimu, wazee, wapenzi wa kasida na waandishi wa habari wa vyombo vya habari vinavyojihusisha na urushaji wa vipindi vinavyohusisha usomwaji wa kasida.

## 3.5 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

### 3.5.1 Mbinu ya Mahojiano ya Ana kwa Ana

Ndumbaro (2014), anaeleza kuwa, mahojiano ni majibizano ya ana kwa ana (au ya simu, kidijitali au barua pepe) kati ya watu wawili au zaidi kwa lengo la kukusanya taarifa au maoni kuhusu suala fulani la kiutafiti lililoainishwa. Mbinu hii ilitumika kufanya mahojiano ya moja kwa moja (ana kwa ana) kati ya mtafiti na mtafitiwa. Nachmias (1981:188), anaeleza kuwa, usaili unaweza kuzingatiwa kuwa ni hali ambayo kunakuwa na maswali ya ana kwa ana kati ya mtafiti na mtafitiwa ambapo maswali hupangwa ili kupata majawabu ya utafiti. Maswali hayo huwa yamepangiliwa au hayakupangiliwa kwa mpango maalum. Katika zana hii, maswali kwa ajili ya usaili yaliandaliwa kwa ajili ya wahojiwa. Maswali hayo yalimsaidia mtafiti katika kukusanya data kulingana na malengo ya utafiti wake. Mtafiti aliwahoji wanafunzi na walimu wa mad-rasa, wapenzi wa kasida, wazee na

waandaaji wa vipindi vinavyohusu tungo za kasida katika vyombo vya habari kama vile redio na televisheni ili kupata taarifa zinazohusu kasida. Mbinu hii iliambatana na kurikodi sauti na vivuli vya wahojiwa ili kuifanya kazi hii iwe ya uhakika na kuaminika zaidi. Mbinu hii ilimwezesha mtafiti kupata data za msingi moja kwa moja kutoka kwa mtafitiwa. Mara nyingi data hizi huwa ni data zenye uhakika zaidi, kwani mtafitiwa huweza kujieleza mwenyewe. Udhaifu wa mbinu hii ni kuwa si rahisi kuwapata wahojiwa wote na kuweza kuwahoji ana kwa ana kutokana na shughuli zao.

### 3.5.2 Mbinu ya Upitiaji wa Machapisho

Hii ni mbinu inayomuwezesha mtafiti kusoma maandishi katika maktaba. Maandishi hayo ni kama vile vitabu, tasnifu, majarida na wavu pepe. Mbinu hii ilimwezesha mtafiti kusoma kasida alizozikuta katika maandishi hayo. Alijisomea maandishi yanayohusu miundo ya utafiti, maelezo ya nadharia, mifano ya kasida na tasnifu zilizowahi kufanywa na watafiti waliotangulia.

Usomaji huu ulimsaidia mtafiti kupata kazi tangulizi zilizomsaidia kukamilisha kazi yake. Hii ni kwa sababu, bila ya kusoma vya kutosha katika maktaba ni vigumu kwa kazi ya utafiti kuweza kukamilika. Hata hivyo, mbinu hii peke yake haitoshi kwa kukamilisha utafiti huu. Hii ni kwa sababu si data zote zitapatikana katika maktaba. Mtafiti alitumia mbinu ya kushiriki kwenye usomwaji wa kasida ili kujionea mwenyewe yanayotokea wakati wa usomaji wa kasida.

### 3.5.3 Mbinu ya Kushiriki katika Matukio

Hii ni mbinu nyengine aliyoitumia mtafiti baada ya mbinu ya maktabani. Katika mbinu hii, mtafiti atashiriki mwenyewe kwenye matukio mbalimbali ili kuona hali

halisi ya usomwaji na uwasilishwaji wa kasida na yanayotokea katika usomaiji huo hapa Mjini Magharibi katika kisiwa cha Unguja. Mtafiti alishiriki katika sherehe za maulid ya kuzaliwa kwa Mtume Muhammad (S.A.W), katika sherehe za harusi, katika sherehe za uondoshaji wa nadhiri, katika sherehe za kijamii na sherehe nyengine zinazohusisha usomwaji wa kasida. Hapa mtafiti alijionea mwenyewe yanayotendeka katika usomwaji wa kasida na aliweza kukusanya data za msingi kwa kutumia mbinu hii.

## 3.6 Vifaa/ Zana za Utafiti

Kothari (2004), anaeleza kuwa vifaa vya utafiti ni vyombo ambavyo mtafiti huvitumia katika kukusanya data. Zana za utafiti ni vifaa vyote vinavyotumika katika kazi ya utafiti. Miongoni mwa vifaa vya utafiti ni kalamu, shajara, kompyuta, kihifadhi data, tepurekoda n.k. Katika utafiti huu, mtafiti alikusanya data zake kwa kutumia zana zifuatazo:

### 3.6.1 Kinasa Sauti (Tepurekoda)

Wamitila (2004), anafafanua kuwa, kifaa hiki kina faida kubwa kwa mtafiti wa fasihi simulizi. Mtafiti kwa kutumia kinasa sauti alikuwa na uwezo wa kuhifadhi sauti ya mtambaji au muhojiwa na kwa njia hii huweza kupata sifa ambazo hazipatikani kwa njia ya maandishi. Kifaa hiki kilitumika wakati wa usaili kurikodi sauti za mazungumzo yanayohusu utafiti wakati wa ukusanyaji wa data. Umuhimu wa kutumia kifaa hichi ni kurahisisha kurikodi data ambazo mara nyengine huwa ni vigumu kurikodiwa kweye shajara. Vile vile sauti zilizorikodiwa kwa kinasa sauti zilitoa data ambazo ni za kuaminika. Hii ni kwa sababu mtu anaweza kusikia sauti

halisi za watu waliohojiwa. Hivyo data zilihifadhiwa kwenye kinasa sauti kwa matumizi ya baadae au wakati wowote ule zitakapohitajika, pia data hizo zitakuwa ni kumbukumbu ya muda mrefu.

### 3.6.2 Kompyuta

Kifaa hiki ni kifaa cha kisasa kabisa na kilitumika katika utayarishaji wa miongozo ya usaili pamoja na utayarishaji wa hojaji zilizotumika katika kuandaa maswali yaliyotumika kuwahoji watafitiwa juu ya data zilizohitajika katika utafiti. Zaidi, kompyuta ilimsaidia mtafiti katika kuhifadhi data zilizopatikana kutoka kwa watafitiwa mbalimbali. Pia kompyuta ilitumika katika kuhifadhi data na kuandikia ripoti ya utafiti ulipokamilika.

### 3.6.3 Hojaji

Wamitila (2003), anafafanua kuwa hojaji ni hati yenye orodha ya maswali ambayo humuongoza mtafiti katika utafiti wake. Maswali hayo huyalenga kwenye mada, tatizo na malengo ya utafiti wake. Katika utafiti huu hojaji zilitumika kama zana za kukusanyia data ambapo ziliandaliwa kwa ajili ya wahojiwa. Hojaji hizo ziligaiwa kwa wanafunzi wa mad-rasa, walimu, wazee, waandishi wa habari na wapenzi wa kasida. Hojaji hizi zilimpa mtafitiwa muda zaidi wa kufikiri juu ya maswali yaliyoulizwa. Pia njia hii ni nzuri kwa wale wanaojua kusoma na kuandika ambao mara nyingi huwa hawana muda wa kukaa na mtafiti. Hivyo watafitiwa wengi waliweza kutoa data kwa wakati muafaka kwa msaada wa wasaidizi wa utafiti ambao walikua na muda wa kutoa data zinazohitajika na kuyarejesha kwa mtafiti kwa ajili ya uchambuzi.

### 3.6.4 Matini

Matini zinazozungumziwa hapa ni matini za kasida. Mtafiti alikusanya matini za watunzi wa kasida na alizitumia kama zana za ukusanyaji wa data. Mtafiti alisoma, kuchambua na kuchunguza matini hizo ili kubainisha aina za kasida zilizomo katika matini hizo na mabadiliko na maendeleo yaliyofikiwa na utanzu huu wa kasida katika awamu zilizotajwa. Matini hizo zilimsaidia mtafiti kupata hata maandishi ya zamani ambayo si rahisi kupatikana kwa njia nyengine za mahojiano. Pia matini zilimpa mtafiti nafasi ya kusoma tafiti nyengine zilizofanywa kwa maandishi ambazo ni miongoni mwa njia bora za kuhifadhia kazi za fasihi.

## 3.7 Vyanzo vya Data

Utafiti huu ulikusanya data zake uwandani. Vyanzo vya data vilikua ni majibu yaliyotolewa na wahojiwa mbalimbali waliohojiwa maswali na mtafiti. Pia data zilipatikana kutokana na taarifa alizozikusanya mtafiti kutoka katika matukio aliyoshiriki. Data za msingi na data za upili zilikusanywa ambapo data za awali zilitokana na majibu waliyoyatoa wanafunzi na walimu wa madrassa. Pia data hizi zilipatikana kwa mtafiti kushiriki katika matukio mbalimbali yaliyohusu usomwaji wa kasida. Matukio haya ni kama vile sherehe za harusi, sherehe za maulidi ya kuzaliwa Mtume Muhammad (S.A.W) na shughuli nyengine zilizosomwa kasida. Data za upili zilipatikana kutokana na upitiaji wa nyaraka maktabani. Mtafiti alisoma maandishi mbalimbali ili kupata taarifa zinazohusu mada yake.

## 3.8 Mpango Wa Utafiti

Utafiti huu umekusanya data kwa kutumia mbinu ya uwandani kwa kukusanya kasida kutoka kwa watafitiwa. Na shughuli hii ya kukusanya data imetumia muda wa

miezi mitano hadi kukamilika kwake, na kazi ya kuchamabua data imetumia miezi miwili. Na uchambuzi wa data umeoneshwa kwa njia ya majadweli, kwa kuonesha vipengele mbalimbali vya fani na dhamira. Pia kwa njia ya maelezo kwa kuonesha matumizi ya vipengele vya fani na dhamira na kubainisha dhamira zilizojitokeza.

### 3.9 Hitimisho

Sura hii ya tatu imeeleza mbinu zilizotumika katika kukusanyia data tokea mwanzo kabisa wa utafutaji wa data hadi mwisho wake wa kuziandika hadi kuzichambua. Katika sura hii mtafiti ameeleza mbinu  alizozitumia, mpango wa utafiti, walengwa wa utafiti, usampulishaji, mawanda ya utafiti, zana / vifaa vya utafiti, ukusanyaji wa data kama vile data za msingi na data za upili, pamoja na sababu za kutumia mbinu hizo badala ya mbinu ya maktaba, na uchambuzi wa data. Sura ifuatayo itaelezea kuhusu uwasilishaji na uchambuzi wa data.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Katika sura hii mambo mawili makuu yamejadiliwa, ambayo ni uwasilishaji wa data na uchambuzi wa data zilizokusanywa maskanini / uwandani. Data zilizokusanywa zinahusiana na mabadiliko ya kasida visiwani Zanzibar pamoja na kuvichambua vipengele vya fani na dhamira. Kwanza zimewasilishwa kasida zinazosomwa katika shughuli mbalimbali za kijamii na kisha kuvichambua vipengele vya fani kama vile muundo, mtindo na baadhi ya vipengele vya lugha.

Vile vile vipengele vya dhamira za kasida katika matukio tafauti vilichunguzwa. Utafiti pia umetumia majadweli kutoa ufafanuzi wa data zilizokusanywa na kuchambuliwa. Majadweli haya yamefafanuliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti ili kurahisisha uelewa kwa wasomaji na watakaoutumia utafiti huu.

## 4.2 Uwasilishaji na Uchambuzi wa Kasida

Kasida zilizochambuliwa zilikusanywa kutoka kwa wanafunzi wa madrasa, walimu, waandishi wa habari, wazee na wapenzi wa kasida. Kasida hizi pia zimekusanywa kutoka katika matukio yaliyoambatana na usomaji wa kasida hapa Zanzibar. Zipo kasida zinazosomwa katika sherehe za maulid ya Mtume (S.A.W). Hizi humsifu Mtume katika kipindi chake cha maisha hapa ulimwenguni. Kasida za harusi husomwa ili kuburudisha waliohudhuria katika harusi pia hutoa elimu kwa maharusi na hadhira kwa ujumla juu ya mambo yanayohusu maisha ya ndoa. Kasida za nadhiri husomwa wakati wa kuondoa nadhiri zilizowekwa na kasida za kuzaliwa kwa mtoto

kwa kiasi kikubwa huwa ni dua juu ya mtoto na kwa familia yake. Mtafiti amekusanya kasida zipatazo thelathini na sita (36) katika matukio tafauti kwa mujibu wa dhima zake.

## 4.3 Kasida za Wakati wa Baada ya Mapinduzi

### 4.3.1 Kasida za Maulid

Maulid ni kisomo kinachosomwa ili kumsifu Mtume Muhammad (S.A.W) na maisha yake aliyoishi hapa ulimwenguni pamoja na kueleza mazazi yake. Kasida hizi humsifu na kueleza sifa zake kama alivyoishi. Kasida hizi zilikuwapo tokea zamani na pia zilikuwapo baada ya Mapinduzi. Nyengine zinaendelea hata wakati wa soko huria. Baadhi ya kasida hueleza sifa za nje za Mtume kama vile sifa za kimwili mbali na tabia zake. Kasida hizi hujenga mapenzi kwa Waislamu kumpenda Mtume wao. Mfano wa kasida hizi zifuatazo:

1. Tumsifuni nabia nabii wetu Muhammad marhabaya
   Mbora wa sifa mbora wa sifa Nyingi za ajabu nyingi za ajabu
   Ndie wetu muokozi Kesho mbele ya wahabu
   Kapelekwa duniani mtangazaji wa dini Mtume wetu nabia
   Allah tumsalie Muhammad Muokoziwa kiama

2. Ilizagaa mianga Bwana alipozaliwa
   Nuru ikatoa anga Huwa Allah
   Pembe zote za dunia Huwa Allah
   Ukaondoka ujinga Na nyoyo kukunjuliwa
   Tuliambiwa zamani Ataletwa duniani Mtume wetu nabia
   Allah, Tumsalie Muhammad Muokozi wa kiama

3. Pepo iliumbwa kwake — Bwana aipozaliwa
Ikajazwa mapamboye — Huwa Allah
Mazuri ya kuvutia — Huwa Allah
Hakuna aingiae — Bila yeye kuingia
Atapandishwa daraja — Ataekuwa na haya ya kumsifu nabia
Allah, Tumsalie Muhammad — Muokozi wa kiama

4. Swalawatu wasalamu — Ziwe zikimshukia
Na sahaba ikram — Huwa Allah
Pamoja na ally pia — Huwa Allah
Na jamii Islamu — Walomtii jalia
Atavikwa taji jema — Kila ataesimama na kumsifu Nabia
Allah, Tumsalie Muhammad — Muokozi wa kiama

Kasida 2.

Muhammad — Muhammad rasuli
Sote tunamjua — Sote tunamjua
Kiongozi wa dini — Mashuhuri
Mola kamteua — Mola kamteua
Awe mbele yetu — Muhammad rasuli
Siku ya kiama — Huwa safiaallah
Muhammad Swalawatullah

1. Alikuwa mwingi wa ukarimu — Kwa jamii ya walioamini
Na maneno yake ni ya elimu — Yanatoka ndani ya Qur’an
Katuletea karimu — Muangaza wenye shani

Awe mbele yetu Muhammad rasuli
Kiongozi wa dini Huwa safiaallah
Muhammad Swalawatullah

2. Mwendo wake walioubaini Walisema huwa wa kunyatia
Visigino havikugusa chini Na mchanga ili kuuridhia
Na sisi tulioamini Hakika twazingatia
Utukufu wa Muhammad rasuli Alijaliwa huwa safiaallah
Muhammad Swalawatullah

3. Khatimae wakawa miguuni Wakifuata mwendo aendao
Ndipo walipobaini Kufudhu mema yajayo
Aloahidiwa Muhammad rasuli Kwa amali zao, huwa safiaallah
Muhammad Swalawatullah

Kasida hizi zilisomwa wakati wa sherehe za maulid ya Mtume. Zilitumika kumsifu Mtume Muhammad (S.A.W) ili kubainisha sifa zake kwa wafuasi wake. Ziliwashajihisha waumini kumpenda na kumfuata Mtume wao. Zimetaja cheo cha Mtume mbele ya waumini. Pia zinawafunza waumini kufuata zile tabia nzuri alizokuwanazo na kujipamba na tabia hizo. Hii ni kwa sababu unapozijua tabia za mtu huwa ni rahisi kumpenda na kumfuata.

Kakiri bwana Bahiri Alipomwona rasuli
Huyu ndiye mughutari Vitabu vimebashiri

1. Alikuwa Mukhtari Kwenye ya Sham safari
Bado angali swaghiri Tisa yake umuri

2. Katika yao safari — Busra waliwasili
   Akawa bwana Bahiri — Amchunguza rasuli

3. Akayaona Bahiri — Mawingu pia shajari
   Yakimficha rasuli — Na mwanga wa jua kali

4. Tena kaona dhahiri — Begani ana muhuri
   Khatima ya urasuli — Mtume tunasubiri

5. Akampasha habari — Ami yake Abu twalib
   Arudi nae safari — Wasijemuua khufari

6. Ya rabi mola satari — Twaomba utusitiri
   Tungie nzuri dari — Pepo na chumwa bashiri

Kasida hii inaeleza sifa zaidi za Mtume (S.A.W). Inaeleza miujiza aliyokuwa nayo pamoja na alama alizokuwanazo katika mwili wake kama alama ya utume wake. Pia inaeleza kazi alizokua akizifanya pamoja na Ami yake ambayo ilikuwa ni biashara kati ya Makka na Sham. Katika uhai wake Mtume alifanya biashara na kuchunga wanyama kama mbuzi na kondoo. Pia kasida hii inatoa ishara ya Utume wa Mtume Muhammad (S.A.W) iliyotajwa katika vitabu mbalimbali vilivyotangulia.

Alizaliwa rasuli — Kipenzi chake jalia

Katika makazi mema — Ya akhera na dunia

Kheri tunawatakia — Ali na swahaba pia

Pua yake ya upanga — Nyusi zake zimetanda
Mabegani muna mwanga — Mithili ya kamaria

Kheri tunawatakia — Alia na swahaba pia

| | |
|---|---|
| Wastani kimo chake | Mtukufu Umbo Lake |
| Ana mwanya meno yake | Kipenzi chake jalia |
| Kheri tunawatakia | Alia na swhaba pia |
| Tena mwingi wa akili | Tumwa akisema kweli |
| Wala hakua mkali | Kwa watu ni maridhia |
| Kheri tunawatakia | Alia na swahaba pia |

Kasida hii inazidi kufafanua sifa za nje za Mtume Muhammad. Inajaribu kueleza umbo lake na hata kimo chake. Mtunzi anafafanua kuwa Mtume alikuwa ni mtu mwenye kutumia akili katika utendaji wake na daima alizugumza maneno ya kweli. Hakupenda kusema uongo hata wala kupotosha mambo. Pia Mtume alikua mpole mbele ya waislamu na wala hakua mkali kwao. Kasida nyingi hasa za zamani ziltumika kumsifu Mtume.

### 4.3.2 Kasida za Wasia na Mawaidha

Kasida hizi zilisomwa ili kutoa wasia Fulani kwa jamii na kuionya jamii juu ya mambo mbalimbali. Pia ziliwakumbusha wanajamii juu ya maisha ya baada ya kufa kwao na maisha watakayoishi baada huko akhera. Mfano wa kasida hizo ni kasida ya "Tukumbuke Wanadama"

Tukumbuke wanadama, Siku ya malipo

Itafika na kuhukumiwa

Maovu yamekithiri

Nafasi ya haki kuwekwa batili

Hiyo ni hasara tumeshaumia

Kasida hii inawakumbusha wanajamii juu ya maisha ya akhera na inatahadharisha kuwa siku ya malipo itafika na watu watahukumiwa. Inawahusia kuacha maovu miongoni mwao kwani hiyo itakuwa ni hasara kwao.

### 4.3.3 Kasida za Wakati wa Msiba

Msiba ni sehemu ya maisha. Msiba huweza kumtokea mtu wakati wowote na pahala popote alipo. Watu hutafuta njia mbalimbali za kujifariji kutokana na msiba uliomfika. Inafaa mtu ajue kua maisha siku zote hayawi kama anavyotarajia bali huambatana na misukosuko mbalimali. Kasida husomwa kwenye misiba ili kuwapa mawaidha waliofiliwa na kuwakumbusha desturi za maisha.

Allah Allahu maulana		Rabi war-zuqna shahada

Alalh Allahu maulana		Rabi war-zuqna Imana

1. Hii dunia si jambo		Hasa la kutegemea

   Tegemea sala tano		Mtazokuwa pamoja

2. Ukimwambia kuswali		Kitanda hukirukia

   Hukwambia swali wewe		Mola alokjalia

3. Nge atapokubana		Utamkumbuka rabana

   Umwite ya Subhana		Ya Ilahi naangamia

4. Kaburi litakubana		Na mbavu zitaachana

   Na moto mkali sana		Tahadhari nakwambia

5. Kaburini kuna nyoka		Ana vichwa sabiini

   Domo la juu na chini		Sawa sawa na dunia

6. Ya Rabi mola ghafuri Naomba utusitiri
Hiyo siku ya hatari Itakapotufikia

Kasida hii husomwa ikibeba ujumbe wa mawaidha kuhusu maisha ya kaburini. Binadamu wameletwa hapa duniani kwa lengo la kufanya ibada. Kasida inamkumbusha binadamu kutodharau lengo hili ambalo ndilo kuu katika makusudio ya kuumbwa kwake.kwa mtazamo wa Uislamu. Kuna ibada zinazofanywa nyakati za asubuhi, mchana na jioni. Ibada za asubuhi huwa na ugumu lakini mtu hutakiwa ajilazimishe kuhudhuria katika ibada hizo. Pia kasida hii inawaasa Waislamu juu ya adhabu zilizomo kaburini na inawafuza wasiache kuomba dua ili waweze kupata maisha mema huko akhera.

Wafiwa tunawapa pole
Wafiwa shikeni mikono
Tunawapa pole

Hii ni kasida iliyosomwa ili kuwpa pole na kuwafariji wafiwa. Ni kawaida kwa watu wa Zanzibar kuwafariji waliopata msiba kwa kuwapa mikono ikiwa ni alama ya huruma na upendo miongoni mwao. Hii husaidia kuwaunganisha na kuonesha umoja baina ya wanajamii. Kuwafariji wafiwa huwapa nafasi ya kuusahau msiba uliowafika japo kwa muda mfupi.

### 4.3.4 Kasida za Nadhiri

Nadhiri ni ahadi anayoiweka mtu kwa Allah baada ya kupata tatizo au akiwa na hamu ya kupata kitu. Huahidi ikiwa jambo lake litakua kama anavyotarajia atatoa sadaka ya kitu fulani au atasoma dua fulani au atafanya jambo fulani. Nadhiri

huhitajika kuondolewa kwa mtu kulifanya lile aliloahidi baada ya kufanikiwa kwa maombi yake. Mara nyingi uondoaji wa nadhiri huambatana na kisomo cha dua pamoja na usomaji wa kasida.

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mikono yako miwili | Kwa wema ilinyanyuka |
| | Maombi yaso dosari | Kwa mola ukapeleka |
| | Kizazi kilo kizuri | Mzazi uwezepata |
| | Leo kwako ni fakhari | Hilo limeshatimika |
| | | |
| 2. | Uliiweka nadhiri | Ilo njema bila shaka |
| | Hilo litakapojiri | Maulid utaweka |
| | Kwa mola wetu kahari | Kilio kikasikika |
| | Zawadi ilo jamili | Kwako wewe ikaletwa |
| | | |
| 3. | Sala zako ulosali | Vizuri zimejibika |
| | Ukahisi ni vizuri | wanafunzi kutuita |
| | Ikiwa yako dhamiri | Maulid kujaweka |
| | Nasi bila ya kujali | Leo hapa tumefika |
| | | |
| 4. | Nasi leo tutayari | Dua njema kuzileta |
| | Aepukane na shari | Mtoto alozalika |
| | Afate njia halali | Na haramu kuiacha |
| | Lengo zote idhilali | Kweke ziweze ondoka |

Kasida hii husomewa mzazi alieweka nadhiri ya kupata mtoto. Kwa hivyo mzazi huamua kuondoa nadhiri hiyo kwa kusoma maulid. Kasida hii ilisomwa ili kumuombea dua huyo mtoto ili aishi katika maisha ya amani na salama. Pia kasida hii humkumbusha mzazi juu ya dua alizoziomba wakati alipokua akiomba kupata mtoto kukubaliwa kwa dua zake. Hivyo ni wajibu kwa mzazi kutekeleza yale yote aliyoahidi kuyafanya ili mtoto wake asipate matatizo kwani ahadi ni deni. Hii

inatufunza kuwa ni muhimu kutekeleza ahadi tulizoziweka ili tuwe watu wakweli na waaminifu katika maisha yetu ya kila siku. Pia ni muhimu kwa mzazi kumuombea dua mtoto wake ili aweze kuishi maisha mema yasiyo na taabu nyingi.

## 4.4 Kasida za Wakati wa Soko Huria

Wakati wa soko huria ni wakati wa mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Kazi nyingi za fasihi za wakati huu zilibadilika na kuwa biashara katika soko. Kasida nazo zimekumbwa na sifa hii kwani zimekua zikiuzwa katika masoko mbalimbali na hata katika maduka ya kuuza kanda zilizorikodiwa. Kasida za aina mbalimbali zimekuwepo katika wakati huu kama ifuatavyo:

### 4.4.1 Kasida za Harusi

Harusi ni miongoni mwa sunna kubwa katika jamii ya Kiislamu. Kila mwanamme anasuniwa kuoa anapofikia umri wa kuoa na ikiwa anao uwezo wa kufanya hivyo. Wanawake pia hutakiwa kuolewa ili kulinda heshima zao na za jamii kwa ujumla. Kwa kupitia kasida maharusi hufunzwa tabia njema ili kuwaandaa wanandoa hao katika maisha yao ya baadae. Hizi huwasaidia kuishi vyema katika maisha yao ya ndoa. Pia kasida hutumika kuiburudisha hadhira iliyohudhuria katika sherehe inayohusika.

Sunna ya Mtume mwema Twashuhudia

Ndoa nia jnambo adhima Twashangiria

1. Shime Islama Mlohudhuria
   Mekuja waona Walo owana
   Mola wajazie wema Waishi salama

2. Kaanza Adama — Hawa kamuowa
Nasi Isilama — Tukafuatia
Mola wajazie wema — Waishi salama

3. Mtume hashima — Ametuambia
Ndoa nidhama — Kwa sote jamia
Mola wajazie wema — Waishi salama

4. Dua ilo njema — Tukubali Allah
Wape wana wema — Waso na mvia
Mola wajazie wema — Waishi salama

Kasida hii husomwa wakati wa sherehe za harusi. Hueleza umuhimu wa ndoa kwa jamii ya Waislamu. Sunna hii ni ya zamani mno. Kwa mujibu wa kasida hii, ndoa ni sunna muhimu kwa kila Muislamu na imeanza tokea kuanza kwa binadamu hapa duniani. Waislamu wanaamini kuwa watu wa mwanzo kuishi hapa duniani ni Adam na bibi Hawa. Pia inatufunza kuwa ipo haja ya kuwaombea dua maharusi ili waweze kuishi vyema katika maisha yao ya ndoa ambayo yanatarajiwa yawe maisha ya milele hadi mmoja wao atakapoaga dunia. Pamoja na umuhimu huu wa ndoa lakini zipo ndoa ambazo hazikubaliki ktika jamii. Baadhi ya ndoa hizo zinaelezwa katika kasida ifuatayo.

NDOA ZISIZOFAA

Twaja kwenu kuelezea — Sisi kadiria
Zile ndoa zisizofaa — Hasa kisheria
Twaja kwenu kuelezea — Sisi kadiria
Zile ndoa zisizofaa — Hasa kisheria
Ni muhimu kuzikemea — Zisijetokea
Za halali kujifanyia — Aloamuru jalia

Ile ndoa ya awali | Mola anoikemea
Ni ile ya muhalili | Atumwae kwenda owa
Japokua siku mbili | Aishi nae kindoa
Likishatimia hili | Talaka akaitoa
Humwita yule rijali | Alomtuma kuowa
Na kumwambia tayari | Mlango nishafungua

KIITIKIO

Twaja kwenu kuelezea | Sisi kadiria
Zile ndoa zisofaa | Hasa kishe
Twaja kwenu kuelezea | Sisi kadiria
Zile ndoa zisofaa | Hasa kisheria
Ni muhimu kuzikemea | Zisijetokea
Za halali kujifanyia | Aloamuru jalia.

Na ile ndoa ya pili | Sisi tulokataziwa ×2
Ni mtu kutosubiri | Eda ikatimilia ×2
Mke bila ya kujali | Kwengine akaolewa
Na kusahau amri | Mola alotuekea
Ikawa yake dhamiri | Watu wapate kujua
Mwili wake ni shuwari | Uzito hajachukua

KIITIKIO

Ndoa ya tatu batili | Mola asoitambua ×2
Ni yule wake walii | Asokuwa wa sheria ×2
Kwani kapanga jalali | Ndani ya Qur'ania
Wale wote marijali | Wa kusimamia ndoa

Mwanzo baba wa halali | Binti alomzaa
Au babu wa ukweli | Na kaka wa kuzaliwa
Twaja kwenu kuelezea | Sisi kadiria
Zile ndoa zisofaa | Hasa kisheria

| | |
|---|---|
| Ni muhimu kuzitambua | Zisijetokea |
| Za halali kujifanyia | Aloamuru jalia |

Mtunzi na wasomaji wa kasida wanajaribu kuitanabahisha jamii juu ya ndoa zisizokubalika katika jamii. Ndoa zina masharti yake na haziwezi kufungwa kiholela. Ziko ndoa ambazo watu hufunga bila ya kuzingatia masharti ya kukubalika kwa ndoa hizo. Kasida imetaja mfano wa ndoa ambayo haijafungishwa kupitia walii halali wa mwanamke anaeolewa. Pia amezitaja ndoa za muhalili. Hizi ni ndoa zinazofanywa baada ya kumuacha ili aolewe tena na mume wake wa mwanzo. Amezitaja pia, ndoa ambazo hazikuzingatia kumalizika kwa eda kuwa ni ndoa zisizokubalika. Imejaribu kutaja baadhi ya mawalii wanokubalika kuwa ni baba mzazi wa binti anaeolewa. Lengo ni kuhakisha kuwa ndoa zinazofungwa zinakidhi viwango vya ndoa bora katika jamii ya Wazanzibari.

INGIA BIBI HARUSI

| | | |
|---|---|---|
| | Bibi harusi | Ni yako nafasi karibu ingia |
| | Bila wasiwasi | Tena kwa udhati tunakupokea |
| | Bibi harusi | Ni yako nafasi, karibu ingia |
| | Bila wasiwasi | Tena kwa udhati tunakupokea |
| 1. | Vigelegele leo tuvitoe | Wetu kimwana tumshangirie ×2 |
| | Kwa shangwe natumpokee | Atapokuja njia akewe |
| | Kwa shangwe kubwa natumpokee | Atapokuja njia akewe |

KIITIKIO

| | |
|---|---|
| Bibi arusi | Ni yako nafasi karibu ingia |
| Bila wasiwasi | Tena kwa udhati tunakupokea |
| Bibi harusi | Ni yako nafasi karibu ingia |

| | |
|---|---|
| Bila wasiwasi | Tena udhati tuna kupokea |
| 2. Na ndani wote wakusubiri wewe | Umependeza sifa hiyo upewe |
| Na ndani wote wakusubiri wewe | umependeza sifa hiyo upewe |
| Twakupongeza bibiye ujuwe | Na huna mwenza akufikiyae |
| Twakupongeza bibiye ujuwe | Na huna mwenza akufikiyae |

KIITIKIO

| | |
|---|---|
| Bibi harusi | Ni yako nafasi karibu ingia |
| Bila wasiwasi | Tena kwa udhati tunakupokea |
| Bibi harusi | Ni yako nafasi karibu ingia |
| Bila wasiwasi | Tena kwa udhati tunakupokea |
| Bwana harusi kakupenda wewe | Hii nafasi uishikilie ×2 |
| Kwa makini nenda katulie | Kwako ndoa kwa wema ukae ×2 |

Kasida hii husomwa wakati wa kumkaribisha bibi harusi kuingia katika ukumbi. Hujaribu kumsifu na kufunza juu ya maisha ya ndoa na kumuheshimu na kumtii mume ili wakae kwa wema. Huonyesha umoja na upendo walionao wanajamii na ushirikiano miongoni mwao juu ya mambo yao kama vile harusi. Kasida hii pia hutumika kuwastarehesha waliohudhuria kwani harusi ni jambo la furaha kwa maharusi na hata jamii kwa ujumla.

### 4.4.2 Kasida Zinazosomwa Katika Sherehe Mbalimbali

Mbali na harusi, zipo kasida zinazosomwa katika sherehe mbalimbali kama vile sherehe za vyuo na ufunguzi wa miradi mbalimbali. Kasida husomwa ili kuwapongeza wale walioanzisha jambo hilo na wale wanaoviendeleza vyuo hivyo na taasisi hizo ili kufikia malengo yanayotarajiwa katika taasisi hiyo

| | | |
|---|---|---|
| | Sherehe leo jama | Tunashangiria |
| | Sherehe leo | Tunafurahia x2 |
| 1. | Karibuni nyi wageni | Nyote mlohudhuria |
| | Mlo hapa uwanjani | Shukurani twawambia |
| | Mujihisi mu nyumbani | Kama mlikotokea |
| | Hiyo hofu ondoweni | Mkae mkitulia x2 |

KIITIKIO

| | | |
|---|---|---|
| 2. | Twaanza nao wazazi | Ndio waliowalea |
| | Hawa wetu wanafunzi | Hadi hapa kufikia |
| | Pia nao viongozi | Juhudi walichukua |
| | Kuongoza wanafunzi | Ndio leo wanag'ara x2 |

KIITIKIO

| | | |
|---|---|---|
| 3. | Twakuomba ya Rabana | Ilahi mola Jalia |
| | Ukinyanyuwe kwa wima | Chuo chetu Faraghiya |
| | Umpe nyingi neema | Mwalimun wetu Bihila |
| | Kwa kusimamia vyema | Chuo chetu Faraghiya x2 |

KIITIKIO

| | |
|---|---|
| Kwa shangwe jama | Tunashangilia |
| Sherehe leo | Imetufikia |

Kasida hii ni mfano wa kasida zinazosomwa katika sherehe za chuo (madrasa). Imekusudia kuwapongeza walimu wazazi na viongozi waliosaidia kwa njia tafauti ili kufanikisha malengo ya madrasa ile. Sherehe kama hizi hufanyika katika vipindi maalum vilivyopangwa ili kutathmini utendaji na ufanisi wa chuo au taasis fulani.

### 4.4.3 Kasida za Dua

Zipo kasida ambazo husomwa kama dua miongoni mwa jamii. Dua ni muhimu ili kujikinga kutokana na madhara yanayotarajiwa kumfika binadamu. Pia dua husomwa ili kuomba jambo ambalo mtu analihitaji au kujikinga na tatizo.

Twakuomba mola wetu		Utupe nyingi hekima
Kwa uswafi nyoyo zetu		Tukutukuze daima
Pia na Mtume wetu		Muhammadi muadhama
Alokuja mbele yetu		Kuongoza dini njema

Aaa Yarabi

Zipokee dua zetu		Ilahi mola karima
Ufute madhambi yetu		Yote tuliyoyachuma
Utupe nuru Ilahi		Leo na kesho kiama
Tuwe nae chumwa wetu		Katika makazi mema

Aaa Yarabi

Twatubia sisi waja		Wako kwako twarejea
Twataraji msamaha		Kwa yote tulokosea
Utujalie ya Allah		Tuwe wenyekusimama
Katika kundi la wema		Na peponi kuingia

Aaa Yarabi

Kazi nyengine za kasida zinaoneshwa na kasida hii. Kazi hii ni dua juu ya mambo mbalimbali. Waislamu waamini kuhusu kuhusu suala hili la dua kuwa ni muhimu kwa maisha yao ya kila siku. Katika kasida hii dua mbali mbali zimesomwa zikiwa na malengo tafauti. Miongoni mwa dua hizo ni kuomba tupatiwe hekima katika maisha ili tufanye maamuzi yetu kwa busara Dua nyengie ni kufutiwa madhambi

ambayo huwa wanafanya kila siku na kila wakati. Madhambi yanaweza kumsababisha mtu kupata maangamizi na mateso hasa huko akhera. Kasida hii inatufunza kuwa ni muhimu kwa binadamu kufikiri madhambi aliyoyafanya na kuomba asamehewe madhambi hayo ili akaishi vyema katika maisha ya baadae.

### 4.5 Uchambuzi wa Data

Kothari (2004.122), anafafanua kuwa uchambuzi wa data ni mchakato wa kuzishughulikia data kwa kuchunguza muundo wa uhusiano uliopo miongoni mwa data zilizopo. Uchambuzi wa data hufanyika baada ya kumalizika ukusanyaji wa data. Uchambuzi wa data ndio unaomuwezesha mtafiti katika kuandika ripoti ya utafiti wake. Hii ni kwa sababu mtafiti huchambua majibu aliyoyapata kutoka kwa watafitiwa waliotafitiwa katika utafiti uliohusika. Uchambuzi wa data katika utafiti huu ulifanywa kwa kutumia mbinu ya maelezo na takwimu. Mbinu hii ilimsaidia mtafiti kwani ilimruhusu mtafiti kuyasoma maandiko na kuyafahamu na kuyachambua majibu yaliyotolewa na watafitiwa ili aweze kuyafahamu vizuri majibu yaliyotolewa na wahojiwa na kubaini idadi ya watafitiwa waliotafitiwa na walioshiriki katika ukusanyaji wa data na baadae kuzichambua.

#### 4.5.1 Uchambuzi wa Data katika Vipengele vya Fani Baada ya Mapinduzi

Kasida zimechambuliwa kwa kutumia lugha fasaha. Madumulla (2009) anafafanua kuwa fani hujumuisha umbo, ufundi na muundo wa kazi za sanaa, mambo kama lugha itumikayo, mtindo, muundo na mandhari. Nadharia ya umuundo ilitumika katika uchambuzi wa vipengele hivi vya fani kama ilivyoelezwa. Nadharia hii hujihusisha zaidi na uchambuzi wa fani hasa miundo ya lugha katika kazi za fasihi.

Kasida hizi zimechambuliwa kwa kupitia vipengele mbalimbali vya fani vinavyojotokeza ambavyo ni muundo wa kasida kwa kuangalia urari wa vina, miundo ya beti na mizani au muwala. Vipengele vyengine ni mtindo na matumizi ya lugha kama yalivyojitokeza katika kasida mbalimbali zilizochambuliwa.

### 4.5.2 Miundo ya Kasida

Kama anavyofafanua Mulokozi (1996), muundo ni msuko, muingiliano na uwiano wa vipengele vyote vinavyojenga shairi au kazi ya sanaa. Katika uchambuzi wa kasida imeonekana kuwa kasida huundwa kwa miundo tafauti. Imeonekana zikiwa na miundo tafauti ya vina, mizani na beti. kuna muundo wa kibwagizo cha nusu mstari. Muundo huu unaonekana katika kasida ifuatayo:

Waumini tunajumuika          Kwa hakika tumefurahika
Tumsifu chumwa msifika          Aloletwa na mola Rabuka
Ni amri yake Rahmani          Kuileta kwetu waumini
Tuifate vyema kwa yakini          Kwa kudumu sote ikhiwani
Jamii waumini

Tukifata misingi ya dini          Na nyoyoni kuwa na imani
Kwa hilo waumini
Shufaa kwetu waumini          Kwa kipenzi chake Rahmani
Isilamu naye l'Amini          Kwa pamoya tungie peponi
Kwa hilo waumini

Kasida hii imeundwa kwa mizani 10 katika uketo na 10 katika ukwapi katika ubeti wa kwanza. Pia imeundwa kwa vina vya kati “ka” na kina cha mwisho “ka” katika mistari miwili ya mwanzo na kina cha kati “ni” na cha mwisho “ni” katika mistari

miwili ya mwisho. Katika kasida hii, kila mwisho wa ubeti kimetumika kibwagizo cha nusu mstari. Mara nyingi kibwagizo kina maneno machache zaidi na huwa nusu mstari.

Muundo mwengine unaonekana katika kasida ifuatayo.

| | | |
|---|---|---|
| Nuru ilimemetuka | Kutoka nchi ya Makaa | Kuelekea Madina |
| Nuru ya mtume mwema | Kiongozi msifika | Tangu vitabu vya tana |
| Ya habibi | Salamu alaykaa | |
| Ya shafii | Salamu alaykaa | |
| Ibada tukufu | Kumsalia chumwa | Mukhtari |
| Chumwa maarufu | Aloteuliwa na mola wake | Kahari |
| Leo imefika | siku njema ya furaha | Siku alozaliwa chumwa Mustafa |
| Sote waumini | Tulohudhuria | Kwa imani zetu tunamsa |
| Ya habibi | Salamu alaykaa | |
| Ya shafii | Salamu alaykaa | |

Kasida hii imeundwa kwa vipande vitatu kwa kila mstari, tafauti na vipande viwili vya kawaida. Pia kasida hii haifuati urari wa vina na mizani kwani kila kipande kima mizani tafauti na kipande chengine isipokua kipande cha kwanza ambapo kina mizani sita (6) katika kila ubeti katika beti mbili za mwisho. Kila ubeti umeundwa kwa mistari miwili, ambapo vina vinafanana katika kipande cha kwanza na kipande cha mwisho. Hata hivyo utaratibu huu haukufuatwa katika shairi zima. Hii inathibitika kwa kuangalia beti mbili za mwisho katika kasida hii. Katika ubeti wa kwanza kina cha mwanzo ni “fu” na cha mwisho ni “ri” lakini ubeti wa pili hauna utaratibu huu wa vina. Pia kasida hii ina kiitikio kila mwisho wa ubeti.

Muundo wa vipande vine pia umetumika katika utungaji wa kasida. Kasida ifuatayo inathibitisha muundo huo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Imeshawadia | Tarehe adhima | Waumini wema | Twafurahia |
| Aliyoshukia | Kiongozi mwema | waumini wema | Twafurahia |
| | | | |
| Katuhudhuria | Mtume mwema | Kwa yakini | Twashingiria |
| Vyema twatubia | Mtume mwema | Sifa zake | Tukitongoa |
| | | | |
| Tunaposikia | Mtume mwema | Asemayo | Twamswalia |
| Nyoyo za tumwa | Mtume mwema | Muhammad | Tukisikia |
| | | | |
| Kutuelezea | Mtume mwema | Nuru yake | hutung’aria |
| Hutusimamia | Mtume mwema | Dua njema | kutuombea |

Kasida hii imeundwa na vipande vinne. Kila kipande hutafautiana katika vina na mizani isipokua katika kipande cha pili ambapo maneno “Mtume mwema” yamerudiwa katika kila mstari. Muundo huu si maarufu sana kwani mara nyingi mashairi huwa vipande viwili.

Zipo kasida zenye beti moja tu. Hizi huwa ni kasida fupi sana ambapo usomaji wake huwa wa kurudia rudia beti hiyo. Mara nyingi kasida hizi ni zile za zamani. Mfano ni kasida ifuatayo

Usiringe kwa ujana

Wala mali na wana

Wangapi vijana waliokufa

Wazee wakabakia

Kasida hii imeundwa kwa ubeti mmoja wenye mistari minne. Haizingatii urari wa vina na mizani katika muundo wake kwani mstari wa kwanza umeundwa kwa mizani nane lakini mstari wa tatu una mizani kumi na moja. Kwa mujibu wa mzee Ilyas Mwevura mwenye miaka 49, anasema kasida hii ilisomwa mwanzoni mwa miaka ya 1990. Uchunguzi umeonesha kuwa kasida nyingi za zamani zilikuwa fupi fupi tafauti na kasida za zama hizi ambazo nyingi zao huwa refu.

Kwa ujumla kasida hutafautiana katika miundo yake. Tafauti hizo huonekana katika miundo ya beti zake, vina na wingi wa mistari katika kila ubeti. Uchambuzi na ufafanuzi umefanywa ili kubaini tafauti hizo kwa kuzichunguza kasida mbalimbali zinazosomwa katika matukio mbalimbali ya nyakati za baada ya Mapinduzi na Wakati wa Soko Huria.

### 4.5.3 Mitindo ya Kasida

Madumulla (2009). Anafafanua kuwa mtindo wa ushairi hujidhihirisha katika matumizi yake ya lugha yaani uteuzi mzuri wa maneno anayoyatumia, upangaji wa maneno hayo, mpangilio wa sauti kuleta athari fulani na matumizi ya tamathali za semi. Katika kasida mitindo mbalimbali imetumika ili kuzifanya ziendane na fani na maudhui yaliyokusudiwa. Miongoni mwa mitindo hiyo ni kama ifuatayo.

#### 4.5.3.1 Mtindo wa Mshangao

Watunzi wa kasida wameutumia mtindo huu ili kuonyesha ufundi Fulani katika utungaji wao. Mtindo huu unadhihirika katika kasida ifuatayo:

Vipi tusimswalie		Mtume muadhama

Kwamba ni yupi mwengine		Atae muegama

| | |
|---|---|
| Ikiwa sio yeye | Na mwengine hapana |
| Ataetuombea | Mbele yake karima! |
| Humswalia Amini | Mola wetu manani |
| Na yale ya mbinguni | Pia ya ardhini |
| Jee ! sisi waumini | Aya zipi bayani |
| Katika Qur'an | Kitabu cha manani |
| | |
| Enyi waumini | Vipi tusimswalie Mtume Muhammad |
| Hali yeye Allah | Anamswalia Mtume Muhammad |
| Jee ! sisi waumini | Tusimswalie Nabia |
| | |
| Hima waumini | Tumswalie Mtume Muhammad |
| Swalallahu allaa | Shafiina wa Maulana Muhammad |
| Ya Habiballah | Ya rasulllah |
| Ya Shafiaaallah | Ya Nnabiaalah |

Mtunzi wa kasida hii anaonesha mshangao kwa waumini ambao wana wajibu wa kumswalia Mtume Muhammad lakini wakawa hawamswalii. Ni haki ya kila muislamu kumuombea dua Mtume ili na yeye akamuombee msamaha siku ya Kiama. Kumswalia Mtume katika Uislamu ni miongoni mwa ibada muhimu nay a lazima kwa kila mtu.

#### 4.5.3.2 Mtindo wa Takriri

Takriri ni mbinu ya kisanaa au kitendo cha kurudia rudia neno au maneno ili kuonyesha msisitizo au kutilia mkazo juu ya jambo au hali Fulani. Takriri inaweza

kuwa ya silabi moja, neno au maneno na hata sentensi. Mtindo huu umetumika katika kasida kama ifuatavyo.

Ya Zamzama Ya Zamzama

Alikunywa chumwa Maji mema

Ya Zamzama

Tufunge safari waumini Kweda Madina

Kwenda kulidhuru Kaburi la chumwa amini

Lenye utukufu wa sharafu Kila aina

Lilopitishwa maji mema Ya Zamzama

Tupate msifu Mustwafa Mtume mwema

Huzidi sharafu kwetu sote Waislama

Huzunguka swafu Malaika Wakitazama

Wakiturushia maji mema Ya Zamzama.

Wale watukufu maswahaba Wa zake zama.

Waliojikifu kwa udhati Wakamwegama

Kaaba tukufu mbele yake Walisimama

Wakafurahia maji mema Ya Zamzama

Katika kasida hii neno 'Ya Zamzama' limerudiwa rudiwa mara nyingi. Hii ni kasida ambayo ilitumika tokea katika wakati wa baada ya Mapinduzi na bado inaendelea

kutumika lengo la kurudiwa rudiwa neno hilo ni kuonyesha msisitizo kuhusu maji haya ya zamzam. Maji haya yanapatikana mjini Saudi Arabia (Makkah). Mbinu hii huonesha upekee wa mwandishi katika kubuni kazi ya fasihi.

| | | |
|---|---|---|
| Katuhudhuria | Mtume mwema | Kwa yakini twafurahia |
| Vyema twatubia | Mtume mwema | Sifa zako twazitongoa |
| Tunaposikia | Mtume mwema | Isimuye twamswalia |
| Nyoyo zachanua | Mtume mwema | Muhammad tukisikia |
| Katuelezea | Mtume mwema | Nuru yake hutung'aria |
| Hutusimamia | Mtume mwema | Dua njema kutuombea |
| Sala na salamu | Mtume mwema | Na baraka twakutakia |
| Kwake muadhamu | Mtume mwema | Shufaae twatarajia. |

Katika kasida hii maneno "Mtume mwema" yamerudiwa rudiwa katika kila ubeti. Hapa kasida inaonesha msisitizo juu ya sifa za mtume kuwa yeye ni mwema. Takiriri hutumiwa katika kazi za fasihi kama mbinu mojawapo ya uwasilishaji wa kazi za kifasihi ili kuifanya kazi hiyo iwe ya kuvutia na isiwachoshe wasiklizaji wake. Kwa hivyo matumizi haya ya takriri katika kasida inaipa kazi hii upekee na inaonesha ubunifu wa mtunzi wa kazi hii.

### 4.5.4 Mtindo wa Kutumia Nafsi

Matumizi ya nafsi ni mbinu nyengine inayotumiwa na watunzi wa kasida. Nafsi mbalimbali zimetumika katika kasida. Nafsi hizi hutumika ili kupata urari wa vina na

mizani au kuifanya kasida iweze kuwa katika hali inayokubalika na kuwavutia wasomaji na wasikilizaji. Mfano wa nafsi ni kama zifuatazo:

#### 4.5.4.1 Nafsi ya Kwanza Wingi

| | |
|---|---|
| Tufunge safari waumini | Kwenda Madina |
| Kwenda kulidhuru | La chumwa Amini |
| Lenye utukufu wa sharafu | Kila aina |
| Lilopitishwa maji mema | Ya Zamzama |
| Tupate msifu mustwafa | Mtume mwema |
| Huzidi sharafu kwetu sote | Waislama |
| Huzunguka swafu malaika | Wakitazama |
| Wakiturushia maji mema | Ya Zamzama |

Katika kasida hii matumizi ya nafsi ya kwanza wingi imetumika. Matumizi haya ya nafsi yanaonekana mwanzoni mwa ubeti wa kwanza na mwanzoni mwa ubeti wa pili. Maneno "tufunge" na "tupate" ni ushahidi wa matumizi haya ya nafsi ya kwanza wingi.

#### 4.5.4.2 Nafsi ya Pili Umoja

Mtindo huu umetumika katika kasida mbalimbali. Imetumika ili kuonesha msisitizo na kuvuta usikivu wa msikilizaji aweze kuisikiliza kasida kwa makini. Mfano wa kasida zilizotumia nafsi ya pili umoja ni kama ifuatayo:

| | |
|---|---|
| Wewe ni mlezi | Unaewalea |
| Umati wako | Wafate njia njema |
| Pia ni mpenzi | Unaewapenda |
| Kwa hadhi yako | Wanaowafanya wema |

| | |
|---|---|
| Kwa kauli yako | Uliyoisema |
| Kuhusu dini | Uliyokabidhiwa |
| Ni fakhari kwako | Itaposimama |
| Na waumini | Wakaitunmikia |

Kasida hii inatuonesha ufundi na ustadi wa mtunzi katika matumizi ya nafsi. Katika kasida hii mwandishi wa kasida amejaribu kumsifu Mtume pamoja na dini aliyopewa. Maneno kama "wewe" yametumika yakiashiria Mtume Muhammad nbila ya kumtaja kwa jina. Kwa hivyo nafsi hutumika ili kutoa ishasra fulani.

#### 4.5.4.3 Nafsi ya Pili Wingi

| | |
|---|---|
| Enyi waumini | Vipi tusimswalie mtume Muhammad |
| Hali yeye Allah | Anamswalia Mtume Muhammad |
| Jee ! sisi waumini | Tusimswalie Nabia |

Hapa neno "enyi" lenye maana ya nyinyi limetumika likiwakilisha nafsi ya pili wingi. Imetumika nafsi hii ili kuwazindua waumini wajibu wao wa kumswalia na kumsifu Mtume Muhammad. Kwa hivyo matumizi haya ya nafsi yanaleta msisitizo juu ya kumswalia Mtume.

#### 4.5.4.4 Nafsi ya Tatu Umoja

| | |
|---|---|
| Kaanza Raufu | Mola Rahmani |
| Yeye kumsifu | Kwenye Qur'an |
| Hana upungufu | Wetul-Amini |
| Katika uongofu | Watu na majini |

Yeye ndie nuri		Mfano qamari
Ameleta kheri		Kafuta batwili
Wengi makufari		Wakamkubali
Kwa njema hubiri	Toka kwa Jalali

Katika kasida hii nafsi ya tatu umoja imetumika. Maneno “yeye” yametumika katika ubeti wa kwanza na wa pili. Katika ubeti wa kwanza limetumika katika kipande cha tatu mwanzoni na katika ubeti wa pili limetumika mwanzoni mwa ubeti. Neno hilo limetumika likimushiria Mtume Muhammad.

### 4.6 Matumizi ya Lugha

Lugha ni kipengele muhimu katika uchambuzi wa kazi za fasihi. Kasida zimechambuliwa kwa lugha fasaha. Zimechambuliwa kwa kupitia vipengele mbalimbali vya lugha vinavyojitokeza katika kasida hizo kama vile matumizi ya lugha ya Kiarabu, matumizi ya lahaja.

#### 4.6.1 Matumizi ya Lahaja za Kimombasa (Kimvita)

Lahaja ya Kimvita imeonekana kutumika sana katika kasida za Kiswahili. Lugha hii imetumika ili kuibua uzuri wa kasida. Miongoni mwa kasida zinazotumia lahaja hii ni kama zifuatazo:

Swala tunamswalia		Rahma kumzidishia
Chumwa rasulillah		Huwa Habibullah

Dua njema za waumini		Zimwendee kipenzi cha manani
Alomleta mola Rahmani		Kuthibitisha nguzo ya dini

Inampasa kila muhisani		Kumfuata chumwal- amini
Ambae pia ndie jemedari		Wa waumini kote duniani

Katika kasida hii neno “chumwa” lenye maana ya “Mtume” limetumika. Neno hili asili yake ni lahaja ya kimvita inayozungumzwa katika maeneo ya Mombasa nchini Kenya. Matumizi ya maneno ya lahaja hii yametumika kutokana na maingiliano makubwa kati ya watu wa Zanzibar na watu wa Mombasa. Inatumika lahaja hii ili kuweza kupata urari wa vina na mizani. Neno jengine la lahaja hii ni “pamoya” lenye maana ya “pamoja”. Limetumika katika kasida ifuatayo

| | |
|---|---|
| Swala tunamswalia | Kipenzi chake jalia |
| Muhammad nabiyullah | Joho kubwa alipewa |
| Hapo akawa Mur-saa | Akrama khalkia |
| Nasi sote kwa pamoya | Twamuombea afua |
| Yarabana rahmatuka | Ala rasulullah |
| Swalatullah alannabbiyy | Huwa habiballah |

Matumizi ya lahaja huwavutia wasikilizaji wengi na kuzifannya kasida ziweze kufahamika na kupendwa na wasikilizaji.

### 4.6.2 Matumizi ya Tash-hisi

Tash-hisi imetumika ili kuifanya kazi ya fasihi kuwa na mvuto kwa wasomajin na wasikilizaji. Hapa vitu huwepewa sifa ya kiumbe hai ambayo haina. Kasida ifuatayo inaonesha matumizi ya tash-hisi:

| | |
|---|---|
| Vitisho vilisimama | Rehema ikawasili |
| Zote Makka na Madina | Zilinawirika |
| Ilipoingian nuru | Yake Muhammad |

Katika kasida hii kuna maneno “ vitisho vilisimama“. Hapa neno vitisho vimepewa sifa ya kusimama ambapo hii ni sifa ya kiumbe hai. Vitisho havina uwezo wa kusimama kwani huu ni uwezo wa viumbe hai. Lugha hii inatoa msisimko kwa wasomaji na wsikilizaji wa kasida na inaongeza hamu ya ya kusikiliza kasida hiyo.

### 4.6.3 Matumizi ya Mubalagha

Mubalagha nin hali ya kutia chumvi juu ya jambo Fulani.kitu au mtu hupewa sifa ya juu kulingana na uwezo wake. Ubeti ufuatao unaonesha matumizi ya mubalagha.

| | |
|---|---|
| Ardhi ilikunjuka | Mimea ikanawiri |
| Na neema zikashuka | Za siri na za dhahiri |
| Watu waloelimika | Ndipo walipobashiri |
| Imekwisha dhihirika | Nuru ya chumwa hashima. |

## 4.7 Hitimisho

Sehemu hii inaeleza kuhusu uchambuzi wa data katika wakati wa baada ya Mapinduzi. Vipengele mbalimbali vya fani vimechambuliwa kama vile miundo ya kasida, mitindo, matumizi ya lugha na matumizi ya nafsi. Utafiti umegundua kuwa katika kasida zilizosomwa wakati wa baada ya mapinduzi zimetumia vipengele hivi vya fani.

## 4.8 Uchambuzi wa Data katika Vipengele vya Fani wakati wa Soko Huria

### 4.8.1 Miundo ya Kasida

#### 4.8.1.1 Vina na Mizani

Kasida za Wakati wa Soko Huria, pia zimeundwa kwa kutumia vina na mizani. Kasida ifuatayo inaonesha miundo ya vina na mizani kama zilivyotumika.

1. Tunatoa heko Pia na wasia

   Tena wende kwako Unaeolewa

   Uyo mume wako Anaekuoa

   Mpe moyo wako Kwa yanovutia

2. Leo zamu yako Imekufikia

   Unakwenda kwako Tena kwa sheria

   Ishi na wenzako Kwa njema tabia

   Majirani zako Watakuridhia

Kasida hii imeundwa kwa mizani 6 katika uketo na 6 katika ukwapi katika beti zote mbili. Imeundwa kwa vina vya kati "ko" na vina vya mwisho "a". Kila ubeti umeundwa mishororo mine. Kasida hii haikufuata muundo wa kawaida wa mizani 8 katika ukwapi na 8 katika uketo.

Pia katika muundo tunaangalia muundo wa beti. Kwa mfano kasida ya hapo juu imeundwa kwa beti mbili:

Mfano mwengine unaonekana, kwa kuangalia kasida ya "Leo Imefika". Katika kasida hii katika beti zake zote imetumia muundo wa mizania 6 kwa 6 lakini katika kiitikio muundo umeachwa na mistari yake imeundwa na mizani zaidi ya 6. Ushahidi wa maelezo haya tuangalie kasida yenyewe kama ilivyonukuliwa

Tunatoa heko Pia na wasia

Tena wende kwako Unayeolewa

Uyo mume wako Anayekuoa

Mpe moyo wako Kwa yanayovutia

Leo zamu yako Imekufikia

Unakwenda kwako		Tena kwa sheria
Ishi na wenzako		Kwa njema tabia
Majirani zako		Watakuridhia

Chunga kinywa chako		Ukijisemea
Ili hadhi yako		Izidi kung'aa
Wacha micharuko		Ya kuruka njia
Dada kazi kwako		Kufata wasia

KIITIKIO

Wamependana wakaoana		Wenyewe wameamua
Cheza kwa kituo mama arusi		Leo ni mwanao hebu jinafasi
Waaqadiria tunaomba dua		Yahya nabia kutushuhudia
Wamependana wakaoana		Wenyewe wameamua.

Kasida hii imeundwa kwa beti nne (4) na kiitikio. Kila ubeti una mistari minne. Kasida hii imeudwa kwa kutumia vina vya kati, ambavyo ni "ko" na kina cha mwisho ambacho ni "a" kama inavyoonekana. Kila mstari umeundwa kwa mizani kumi na mbili (12), sita katika kipande cha mwanzo (uketo) na sita katika kipande cha pili (ukwapi). Kwa mfano tuangalie ubeti ufuatao

Chunga kinywa chako		Ukijisemea
Ili hadhi yako		Izidi kung'aa
Wacha micharuko		Ya kuruka njia
Dada kazi kwako		Kufata wasia

Kila mstari katika ubeti huu na beti nyengine umeundwa kwa mizani kumi na mbili kama inavyoonekana hapo juu. Mtindo huu si wa kawaida kwani kwa kawaida shairi huwa na mizani kumi na sita; nane katika ukwapi na nane katika uketo.

Hata hivyo utaratibu huu haukutumika katika kiitikio ambapo kila mstari una mizani tafauti na mstari mwengine. Kwa mfano katika mstari wa kwanza, kipande cha kwanza kina mizani kumi na kipande cha pili mizani nane. Katika mstari wa pili wa kiitikio kipande cha kwanza kimeundwa na mizani kumi na moja na katika kipande cha pili kuna mizani kumi na mbili. Pia kuna muundo wa kibwagizo cha nusu mstari

Muundo mwengine uliotumika katika kasida ni muundo wa kutumia neno moja katika kipande cha pili kwa kila mstari. Muudo huu unaoekaa katika kasida zifuatazo

Oa ndugu yangu oa        Kama ilivyo sheria
Mtume kafunga ndoa        Pia mahari akatoa
Kahalalisha manani        Oaaa
Kwenye yake Qur’an        Oaaa
Harusi hii yakini        Oaaa
Furaha kwa waumini        Oaaa

Hakika ya Rahmani        Oaaa
Ndoa huleta amani        Oaaa

Harusi iwe ya kheri        Oaaa
Mufurahi maishani        Oaaa

Kasida nyengine yenye muundo kama huu ni kasida ifuatayo:

Sote tunashangiria        aaa        Harusi ya kaka yetu
Leo umefunga ndoa
Ndugu yetu mtukufu        Aaaa
Leo twamvika taji        Aaaa

Tunakuomba raufu Aaaa

Uzidi kumfariji Aaaa

Akujalie Latifu aaa Mema yawe mahitaji

Rabi umpe Baraka Aaaa

Ndani ya machumi yake Aaaa

Umuepushie shaka Aaaa

Jamii kazini wake Aaaa

Katika kasida hii muundo huu umetumika katika beti zote. Katika kipande cha kwanza mtunzi ametumia mizani nane nane lakini katika kipande cha pili limetumika neno moja ambalo ni herufi tu “aaa”. Neno hili linatumika kama kiitikio.

Hata hivyo utaratibu huu haukutumika katika kiitikio ambapo kila mstari una mizani zake tafauti na mstari mwengine. Kwa mfano katika mstari wa kwanza, kipande cha kwanza kina mizani kumi na kipande cha pili mizani nane. Katika mstari wa pili wa kiitikio kipande cha kwanza kimeundwa na mizani kumi na moja na katika kipande cha pili kuna mizani kumi na mbili.

#### 4.8.2 Mitindo ya Kasida

Madumulla (2009). Anafafanua kuwa mtindo wa ushairi hujidhihirisha katika matumizi yake ya lugha yaani uteuzi mzuri wa maneno anayoyatumia, upangaji wa maneno hayo, mpangilio wa sauti kuleta athari fulani na matumizi ya tamathali za semi. Katika kasida mitindo mbalimbali imetumika ili kuzifanya ziendane na fani na maudhui yaliyokusudiwa. Miongoni mwa mitindo hiyo ni kama ifuatayo.

### 4.8.3 Mtindo wa Kutumia Nafsi

Matumizi ya nafsi ni mbinu nyengine inayotumiwa na watunzi wa kasida. Nafsi mbalimbali zimetumika katika kasida. Nafsi hizi hutumika ili kupata urari wa vina na mizani au kuifanya kasida iweze kuwa katika hali inayokubalika na kuwavutia wasomaji na wasikilizaji. Mfano wa nafsi ni kama zifuatazo.

#### 4.8.3.1 Nafsi ya Kwanza Wingi

Mtindo huu umetumika katika kasida mbalimbali. Mfano nzuri wa mtindo huu umo katika kasida inayoitwa "Dua njema", mfano katika ubeti wa pili anaeleza

| | |
|---|---|
| Tufanyeni hiba | Swala za Nabia |
| Iwe ndio twiba | Katika dunia |
| Na zote ukuba | Kutuepushia |
| Yetu matilaba | Tutakubaliwa |

Katika kasida hii matumizi ya nafsi ya kwanza wingi imetumika. Matumizi haya ya nafsi yanaonekana mwanzoni mwa ubeti wa kwanza na mwanzoni mwa ubeti wa pili. Maneno "tufanyeni hiba" ni ushahidi wa matumizi haya ya nafsi ya kwanza wingi.

### 4.9 Matumizi ya Lugha

Lugha ni kipengele muhimu katika uchambuzi wa kazi za fasihi. Kasida zimechambuliwa kwa lugha fasaha. Zimechambuliwa kwa kupitia vipengele mbalimbali vya lugha vinavyojitokeza katika kasida hizo kama vile matumizi ya lugha ya Kiarabu, matumizi ya lahaja.

### 4.9.1 Matumizi ya Tamathali ya Semi ya Sitiari

Tamathali ya semi ya sitiari ni aina ya tamathali inayotumika katika kuhusisha matendo, kitu au tabia ya vitu vyenye maumbile tofauti (huleta uhamisho wa kimaana). Vilevile Mulokozi na Kahigi (1979) wamefasiri maana ya sitiari kuwa ni uhamishaji wa maana na hisi kutoka katika kitu au dhana nyengine, vitu hivyo vinavyohusishwa kwa kawaida huwa havina uhusiano wa moja kwa moja.

Wakati mwengine sitiari haitumii kiunganishi katika kuhusisha matendo tofauti. Hivyo tunaweza kusema sitiari ni tamathali ya semi inayotumika kulinganisha vitu viwili vyenye sifa tofauti bila ya kutumia kiunganishi. Kasida ifuatayo inaonesha matumizi ya sitiari

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Maisha mazur ikuwajaalia | Na yote ya shari kuwaepushia |
| | Kila la fakhari kuwamiminia | Na mwanga wa nuri kuwaangazia |
| | Maneno ya shariyatawakimbia | Waishi vizuri pasi a ubaya |
| 2. | Kuondoka kwako ukatukimbia | Mazoea yako yakatupotea |
| | Na haiba yako tuloizoea | Ya swauti yako yenye kuvutia |
| | Kwetu sikitiko lisiloishia | Tukukumbukapo hwenda tukalia |
| 3. | Ila kwa sababu hii ni sharia | Twamuomba Rabu kukujaalia |
| | Moyo wa dhahabu kukukunjulia | Madhila na tabu kupotea njia |
| | Kwako umuhimu kwenda muombea | Iwe ni sababu neema kungia |

Katika kasida hii maneno “Moyo wa dhahabu” yametumika kisitiari. Maneno haya yanaonesha uzuri wa moyo wa muhusika. Matumizi ya tamathali hii inaonesha ufundi wa mtunzi na pia huwavutia hadhira na wasikilzaji wa kasida.

### 4.9.2 Matumizi ya Ishara

Ishara ni mbinu ya kisanaa au kitendo cha kuashiria neno au maneno ili kuonyesha msisitizo, kuficha jambo au kutilia mkazo juu ya jambo au hali fulani. Ishara inaweza kuwa ya neno moja au maneno na hata sentensi. Mtindo huu umetumika katika kasida ya "Furaha ya Wazazi". Katika kasida hii, ubeti wa pili mwandishi anaeleza:

| | |
|---|---|
| Hufanya kila aina | Mwana asije kupinda |
| Hulinda yake heshima | Kwa kila anaporanda |
| Huipalilia vyema | Ipendeze yao shamba |
| Ili atokuja vuna | Isije ikamshinda |
| Humsimamia, humfatilia | Asijepotea njia mbaya |

Katika kasida hii maneno yaliyokozeshwa kama vile neno " shamba" linaashiria mtoto wa kike. Lengo la kutumia ishara ni neno hilo ni kuonyesha ufundi Fulani wa utunzi na kupunguza baadhi ya maneno ambayo mara nyengine huwa hayapendezi sana katika mkusanyiko wa watu. Pia mbinu hii huwavutia wasikilizaji wa kasida. Mbinu hii huonesha upekee wa mwandishi katika kubuni kazi ya fasihi.

### 4.9.3 Matumizi ya maneno ya Lugha ya Kiarabu

Kasida za Kiswahili mara nyingi hutumia maneno ya lugha ya Kiarabu pamoja na Kiswahili. Hii imetokana na maingiliano kati ya lugha ya Kiswahili na Kiarabu. Mfano wa kasida zilizotumia lugha ya Kiarabu ni kama zifuatazo:

| | | |
|---|---|---|
| Mazazi ya kheri | | Tunasimulia |
| Shafii nnuri | | Alipofikia |
| Rabiil-awal | Jumatatu | Thani Ashiria |

Ni alfajiri Saa njema Alipozaliwa

Kote ardhini na mbinguni Amepokelewa

Kasida hii imetuonyesha matumizi ya maneno ya lugha ya Kiarabu. Imetumia maneno mengi ya Kiarabu katika kibwagizo na hata katika mistari ya beti mbalimbali. Mfano wa maneno ya Kiarabu yaliyotumika ni "shafii nuri, rabiil-awal na thani ashiria". Maneno haya yana maana tafauti kama ifuatavyo

Shafii -Mwenye kuombea

Rabiil-awal -Mwezi wa mfunguo sita (mwezi wa tatu kwa kalenda ya Kiislam)

Thani ashiria -Mwezi kumi na mbili

Watunzi wa kasida hutumia lugha ya Kiarabu ili waweze kuibua dhamira kwa urahisi na kuzifanya kasida ziweze kusomeka na kughanika kwa urahisi. Matumizi ya lugha hii huwavutia wasiklizaji na kuwashajihisha kuzisikiliza kasida zinaposomwa na kuvuna ujumbe uliokusudiwa.

### 4.9.4 Matumizi ya Tash-hisi

Tash-hisi imetumika ili kuifanya kazi ya fasihi kuwa na mvuto kwa wasomajin na wasikilizaji. Hapa vitu huwepewa sifa ya kiumbe hai ambayo haina. Kasida ifuatayo inaonesha matumizi ya tash-hisi:

Vitisho vilisimama Rehema ikawasili

Zote Makka na Madina Zilinawirika

Ilipoingian nuru Yake Muhammad

Katika kasida hii kuna maneno “ vitisho vilisimama“. Hapa neno vitisho vimepewa sifa ya kusimama ambapo hii ni sifa ya kiumbe hai. Vitisho havina uwezo wa kusimama kwani huu ni uwezo wa viumbe hai. Lugha hii inatoa msisimko kwa wasomaji na wsikilizaji wa kasida na inaongeza hamu ya ya kusikiliza kasida hiyo.

### 4.9.5 Matumizi ya Mubalagha

Mubalagha ni hali ya kutia chumvi juu ya jambo fulani. Kitu au mtu hupewa sifa ya juu kulingana na uwezo wake. Senkoro (2011: 12) tamathali hii hutia chumvi kuhusu uwezo wa viumbe, tabia zao na sifa zao kwa madhumuni ya kuchekesha na kusisitiza jambo. Ubeti ufuatao unaonesha matumizi ya mubalagha.

| | |
|---|---|
| Ardhi ilikunjuka | Mimea ikanawiri |
| Na neema zikashuka | Za siri na za dhahiri |
| Watu waloelimika | Ndipo walipobashiri |
| Imekwisha dhihirika | Nuru ya chumwa hashima. |

Katika kasida hii ardhi inaoneshwa kuwa imekunjuka kama kwamba mwanzoni ilijikunja. Hapa pametiwa chumvi ili kuonesha na kusisitiza kuhusu miujiza ya Mtume tokea alipozaliwa. Haiwezekani kwa ardhi kujikunja na kujikunjua wenyewe katika hali ya kawaida.

## 4.10 Hitimisho

Sehemu hii imefafanua kuhusu vipengele vya fani katika wakati wa Soko Huria. Utafiti umegundua kuwa vipengele mbalimbali vya fani vimeendelea kutumika katika utungaji wa kasida za Kiswahili katika wakati huu. Miundo na mitindo tafauti imetumika pamoja na matumizi ya lugha na matumizi ya nafsi. Mabadiliko

yaliyoonekana ni kwamba, kasida za wakati wa soko huria baadhi yake hazizingatii urari wa vina na mizani. Kasida nyengine za wakati wa baada ya Mapinduzi ni fupi sana, pia kuna baadhi ya kasida zina beti moja tu. Baadhi ya kasida pia huwa na kipande kimoja. Katika wakati wa soko huria kumekua na uhuru mkubwa katika utungaji wa kazi za fasihi na kwa hivyo kasida nazo zimeathiriwa na uhuru huu.

## 4.11 Uchambuzi wa Data katika Vipengele vya Maudhui katika Wakati wa Baada ya Mapinduzi

Maudhui ni sehemu muhimu katika uchambuzi wa kazi za fasihi. Madumulla (2009) anaeleza kuwa maudhui ni mawazo, fikra na ujumbe katika kazi za fasihi. Nadharia ya sosholojia ya fasihi ilitumika katika uchambuzi wa dhamira. Nadharia hii huchambua vipengele vya ndani vya kazi za fasihi. Inaamini kuwa mabadiliko ya kiuchumi na kisiasa huchangia katika mabadiliko ya kijamii ambapo kasida ni miongoni mwa mambo ya kijamii. Katika kasida vipengele vya dhamira vimechambuliwa kwa kutumia lugha fasaha.

### 4.11.1 Uchambuzi wa Dhamira katika Kasida

Dhamira ni wazo kuu ambalo linajadiliwa katika kazi za fasihi. Kasida nazo hazijaacha kubeba dhamira ambazo zinakusudiwa kuwafika wasikilizaji na wapenzi wa kasida. Dhamira mbalimbali zimejadiliwa katika kasida katika kipindi cha bbada ya Mapinduzi kama ifuatavyo:

### 4.11.2 Kuwa na Tabia Njema

Miongoni mwa Dhamira zilizoshughulikiwa na kasida ni umsifu Mtume (s.a.w). Dhamira hii ya kueleza tabia njema za mtume ni muhimu kwani ndio asili ya kasida

tangu zilipoanzishwa. Kasida zifuatazo zinabeba dhamira ya kueleza tabia njema za Mtume Muhammad (s.a.w)

| | |
|---|---|
| Muhammad | Muhammad rasuli |
| Sote tunamjua | Sote tunamjua |
| Kiongozi wa dini | Mashuhuri |
| Mola kamteua | Mola kamteua |
| Awe mbele yetu | Muhammad rasuli |
| Siku ya kiama | Huwa safiaallah |

Muhammad Swalawatullah

| | |
|---|---|
| Alikuwa mwingi wa ukarimu | Kwa jamii ya walioamini |
| Na maneno yake ni ya elimu | Yanatoka ndani ya Qur’an |
| Katuletea karimu | Muangaza wenye shani |
| Awe mbele yetu | Muhammad rasuli |
| Kiongozi wa dini | Huwa safiaallah |

Muhammad Swalawatullah

| | |
|---|---|
| Mwendo wake walioubaini | Walisema huwa wa kunyatia |
| Visigino havikugusa chini | Na mchanga ili kuuridhia |
| Na sisi tulioamini | Hakika twazingatia |
| Utukufu wa Muhammad rasuli | Alijaliwa huwa safiaallah |

Muhammad Swalawatullah

| | |
|---|---|
| Khatimae wakawa miguuni | Wakifuata mwendo aendao |
| Ndipo walipobaini | Kufudhu mema yajayo |
| Aloahidiwa Muhammad rasuli | Kwa amali zao, huwa safiaallah |

Muhammad Swalawatullah

Kasida hii inabeba moja kwa moja dhamira ya tabia njema kama alizokuanazo Mtume Muhammad (s.a.w). Inaeleza sifa na tabia za Mtume huyu. Inaeleza kuwa alikua mtukufu, mpole na mkarimu kwa waumini wote. Alikuwa akizungumza maneno ya hekima na maneno ya kielimu ambayo yatasaidia jamii kwenda mbele na kupata maendeleo katika nyanja zote za maisha. Mtume hakua mtu wa kujivuna na kuwa na kiburi juu ya wafuasi wake. Kutokana na sifa na ubora wa mtume Muhammad alifanikiwa kuwavuta na kuwapata wafuasi wengi na kuwafundisha tabia njema na dini ya Kiislamu. Kasida nyengine inayoelezea sifa za Mtume ni kasida ifuatayo:-

Nasi waumini Tumejumuika Hadhara adhima
Tuko furahani Tunasheherekea Kuzawa hashima
Tunamtakia Rehema Msifika
Mtume nabia Chumwa Alotukuka

Walimsifia Makafiri pia Mtume nabia
Mali za thamani Alipelekewa Kuwahifadhia
Akiwakabidhi Yote Iliyotimia
Jina la amini Wakamtunukia

Utukufu wake Ulidhirika Tangia Adama
Walotangulia Wakanusurika Kwa jinale jema
Kawafata wote Mussa na Burahima
Hata nabii Issa Na walotakadama

Kasida hii inazidi kudhirisha dhamira ya kumsifu Mtume Muhammad (S.A.W). Inaeleza kuwa, alikuwa muaminifu na hata watu mbalimbali waliweza kumpa amana

zao ili awahifadhie. Alifanya hivyo kwa uaminifu na walipata walichokiweka kwa ukamilifu wake bila kupunguza chochote katika vile vilivyohifadhiwa kwake. Ukweli na uaminifu ni tabia njema mabyo kila mtu anatakiwa kujipamba na sifa hiyo. Pia kasida inamsifu Mtume kwa kuwafuata mitume iliyotangulia kama vile Nabii Mussa, Ibrahim na Nabii Issa.

### 4.11.3 Umoja na Mshikamano

Kasida za wakati wa baada ya Mapinduzi zilijikita pia, katika kujenga umoja na mshikamano miongoni mwa wanajamii. Ziliijenga jamii kuishi pamoja na kusaidiana wakati wa dhiki na faraja.

Wafiwa tunawapa pole
Wafiwa shikeni mikono
Tunawapa pole

Ilikuwa ni kawaida kwa watu wa Zanzibar tokea hapo zamani kushirikiana katika mambo yao. Mambo hayo yanaweza kuwa ya furaha na hata misiba. Katika mambo ya misiba waliweza kupeana pole na kusaidiana ili kupunguza ugumu wa msiba kwa waliofikwa na msiba huo.

### 4.11.4 Utekelezaji wa Ahadi

Utekelezaji wa ahadi katika jamii ni jambo muhimu ili kuleta utengamano miongoni mwao. Jamii inatakiwa kutekeleza ahadi zao walzoziweka ili kudhihirisha ukweli wao. Katika kasida nyigi za nadhiri dhamira za utekelezaji wa ahadi hujitokeza kwa tendo lenyewe la kuweka nadhiri ambalo huambatana na ahadi.

1. Mikono yako miwili — Kwa wema ilinyanyuka
   Maombi yaso dosari — Kwa mola ukapelekwa

| | | |
|---|---|---|
| | Kizazi kilo kizuri | Mzazi uweze pata |
| | Leo kwako ni fakhari | Hili limeshatimika |
| 2. | Uliiweka nadhiri | Ilo njema bila shaka |
| | Hilo litakapojiri | Maulidi utaweka |
| | Kwa mola wetu kahari | Kilio kikasikika |
| | Zawadi ilo jamili | Kwako wewe ikaletwa |
| 3. | Sala zako ulosali | Vizuri zimejibika |
| | Ukahisi ni vizuri | Wanafunzi kutuita |
| | Ikiwa yako dhamiri | Maulidi kujaweka |
| | Nasi bila ya kujali | Leo hapa tumefika |
| 4. | Nasi leo tutayari | Dua njema kuzileta |
| | Aepukane na shari | Mtoto alozalika |
| | Afate njia halali | Na haramu kuiacha |
| | Lengo zote idhilali | Kwake ziweze ondoka |

Katika kasida hii tumeona kuwa yule anaesomewa kasida alieka ahadi (nadhiri) ya kusoma maulidi ikiwa atapata mtoto. Aliomba dua kwa Allah (S.W) ili apate motto huyo. Alipompata mtoto alihitajika atekeleze ile ahadi aliyoiweka hapomwanzo. Hivyo akaamua kuwaita wanafunzi wa madrasa ili wamsomee maulid aliyoahidi na kumuombea dua mtoto wake.

### 4.11.5 Wasia

Baadhi ya kasida za wakati huu zilikuwa ni kasida za wasia kwa jamii juu ya mambo mbalimbali. Ziliwaelekeza katika kufanya mambo mema na kuwatahadharisha juu ya athari za kutenda maovu. Mfano ni kasida ya "Wacha Maringo Mwanadama". Mwandishi anaeleza:

Usiringe kwa ujana

Wala mali na wana

Wangapi vijana waliokufa

Wazee wakabakia?

Hapa kasida inawausia wanajamii kuacha maringo kwa kutegemea ujana. Ujana utamalizika na mtu ataingia katika utu uzima. Katika wakati huu mtu huwa na upungufu fulani katika kiwiliwili chake, hivyo hushindwa kuyafanya baadhi ya majukumu yake. Inawaasa waache kuringa kwa ujana na mali kwani haya yote akiyatumia vizuri yatamuwezesha kuishi.

## 4.12 Hitimisho

Katika sehemu hii dhamira mbalimbali zimechambuliwa. Dhamira zilizochambuliwa ni zile za wakati wa baada ya mapinduzi. Dhamira za kua na tabia njema, umoja na mshikamano na utekelezaji wa ahadi na kasida za wasia zimechambuliwa. Dhamira hizi zimeonesha asili ya kasida. Katika wakati huu, kasida zaidi zilimsifu Mtume Muhammad (S.A.W). Utafiti umegundua kuwa zilikuwa za kidini zaidi kuliko kuwa za kibiashara. Dhamira zililenga pia katika kuwausia wanajamii katika kutenda mema na kuacha mabaya na zilikua na atahari kubwa kwa waliozisikiliza.

## 4.13 Uchambuzi wa Data za Dhamira Wakati wa Soko Huria

### 4.13.1 Umuhimu wa Kutenda Haki katika Jamii

Kasida hutumika kuelimisha jamii katika mambo mbalimbali yanayohusu maisha ya jamii hasa maisha ya ndoa. Hujaribu kuionya na kukosoa jamii juu ya mambo yasiyofaa yanayotendwa na wanadoa. Huelimisha umuhimu wa kutenda haki katika

jamii. Kasida zifuatazo zinaelimsha umuhimun wa kutenda haki katika jamii kama ifuatavyo:

Vyema muelewe hili	Kwa wake muloolewa
Munaomiliki mali	Nafasi na nyadhifa pia
Mukajitia kiburi	Kuwakosea
Na kuzipinga amri	Zake Jalia
Zile haki za rijali	Kuziondoa
Eti yeye hana mali	Kajichokea
Ni vizuri kuwajali	Wanowambia
Japo kama zao hali	Sio sawia.

Mwazitengua amri	Wanawake twawambia
Muda kwenu ni thakili	Wao kuwahudumia
Kwa kweli muna khiari	Kushughulikiwa
Na wanawake wambali	Wasowaowa
Wawe wanawakabili	Kuwapikia
Pia mambo mbali mbali	Kuwafanyia
Na ujira mutayari	Kuwapatia
Jambo hili si sahihi	Munakosea

Na kwa upande wa pili	Pia wanazo tabia
Waume twawahubiri	Walobeba ya dunia
Huwadharau kikweli	Walowaowa
Pia na kuwakejeli	Kwa mbaya njia

Kwani huwa hawajali Waloamriwa
Kazi zimewakabili Bize wajitia
Muda kwao ni muhali Kuwa pamoya
Na mke hana kauli Hujinamia
Japo kama si halali Anofanyiwa
Lakini huyakubali Ndo kaolewa

Haki zenu muheshimu Mke na mume kwa pamoya
Hata kama mnajikimu Musizibadili sharia
Muhimu kuhudumiana Pia ndani kutulizana
Muupate na muda vyema Kukaa pamoya na wana
Hapo ndipo mtapendana Na ndoa yenu itafana
Kwa kule kushirikiana Na haki kutimiziana
Na izidi yenu heshima Hili mulielewe vyema
Na sio kwenu kuvutana Usiku unaposimama
Yapasa muelewe vyema Enyi ndugu waislama

Haki zenu muheshimu Mke na mume kwa pamoya
Hata kama mnajikimu Musizibadili sharia

Kasida hii inawafunza mabibi harusi na mabwana harusi kuheshimiana na kutekeleza haki zao kwa wengine bila kuziendea kinyume. Miongoni mwa haki za mke kwa mumewe ni kumheshimu hata ikiwa hana uwezo wa mali kama alionao yeye mke. Mwanamme nae awajibike kutenda haki kwa mkewe hata kama ni dhaifu kwa

kukosa uwezo wa kifedha. Pia kasida hii inatuelimisha umuhumu wa malezi kwa watoto. Inashajihisha wazazi kukaa pamoja na watoto wao, kuwafunza yanayowahusu. Kama kasida ya hapo juu inavyoeleza.

"Muupate na muda vyema     Kukaa pamoya na wana"

Hapa wazazi wanafunzwa kukaa pamoja na watoto wao ili kuwafunza mambo yanayohusu maisha yao. Malezi ya watoto huhitajika kutoka kwa wazazi wote wawili (baba na mama). Kasida hii pia haikuacha kuwakosoa wanawake walioolewa kwa tabia yao ya kutowahudumia waume zao. Inakosoa tabia yao ya kuajiri wafanyakazi wa ndani na kuwaruhusu kuwahudumikia waume zao kwa kila hali. Hili athari zake huwa ni kuharibika kwa ndoa kwa waliooana ikwa hawakua makini juu ya mfanyakazi wao. Katika hili kasida ifuatayo inaeleza

| | |
|---|---|
| Mwazitengua amri | Wanawake twawambia |
| Muda kwenu ni thakili | Wao kuwahudumia |
| Kwa kweli muna khiari | Kushughulikiwa |
| Na wanawake wambali | Wasowaowa |
| Wawe wanawakabili | Kuwapikia |
| Pia mambo mbali mbali | Kuwafanyia |
| Na ujira mutayari | Kuwapatia |
| Jambo hili si sahihi | Munakosea. |

Hivyo kasida inawakosoa wanandoa kuacha kuwaamini sana wafanyakazi wa ndani. Bali ni vyema kazi muhimu za ndani zifanywe na mke mwenyewe ili kudumisha mapenzi na uaminifu miongoni mwao. Si vyema kwa mke kujishughulisha sana na

kukosa muda wa kumuhudumika mumewe. Kwa ujumla kasida hii inawafuza wanandoa kujenga doa yenye mapenzi na kujenga ushirikiano baina yao.

### 4.13.2 Sifa za Mtume

Kasida za wakati wa soko Huria nazo hazikuacha dhamira hii ya kueleza sifa na tabia njema za Mtume Muhammad (S.A.W). Hii ndio dhamira ya msingi ya kasida tokea katika historia yake. Dhamira hii imekua ikiendelea hata baada ya mabadiliko ya jamii kisiasa na kiuchumi. Kasida mbalimbali zinasomwa zikiwa na lengo hili. Kasida ifuatayo inathibitisha maelezo haya

| | |
|---|---|
| Jamii ya mwendo wake | Mkamilifu Nabia |
| Pamoja na sifa zake | Kwa khuluka na tabia |
| Ajabu ya moyo wake | Hamaki hakutumia |
| Taratibu mwendo wake | Mpole akikujia |

| | |
|---|---|
| Wallahi twanena kweli | Sifa zake zote njema |
| Mkamilifu Rasuli | Mbele ya Mola Qarima |
| Mkweli chumwa Amini | Hakuwa mtu khiyana |
| Pamoja na nyingi shari | Za makuhani wa Makka |

Kasida hii inaeleza sifa za Mtume Muhammad (S.A.W) kuwa alikua na tabia njema. Hata mwendo wake haukua wa madaha na kujiona. Pia kasida inamsifu Mtume kuwa hakua na hamaki alipozungumza na mtu yoyote. Mtume huyu alikua mkweli na muaminifu hata wakati wa shida na dhiki zilizotokana na wanadamu. Kwa mujibu wa Mwalimu (Ustadh) Ali anaeleza kuwa kasida hii ilitungwa mwaka 2005. Hii inadhihirisha kuwa bado kasida zinabeba dhamira za kumsifu Mtume Muhammad (S.A.W)

### 4.13.3 Kuwa na Tabia Njema

Kasida nyingi pia huifunza jamii kuwa na tabia njema ili kuishi vyema katika jamii yao. Tabia njema hujenga udugu na ushirikiano miongoni mwao na tabia mbaya huleta mfarakano miongoni mwa wanajamii kama inavyoelezwa katika kasida ya "Leo Imefika".

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Tunatoa heko | Pia na wasia |
| | Tena wende kwako | Unayeolewa |
| | Uyo mume wako | Anaekuoa |
| | Mpe moyo wako | Kwa yanayovutia |
| 2. | Leo zamu yako | Imekufikia |
| | Unakwenda kwako | Tena kwa sharia |
| | Ishi na wenzako | Kwa njema tabia |
| | Majirani zako | Watakuridhia |
| 3. | Chunga kinywa chako | Ukijisemea |
| | Ili hadhi yako | Izidi kung'aa |
| | Wacha micharuko | Ya kuruka njia |
| | Dada kazi kwako | Kufata wasia |

Katika kasida hii, jamii inafunzwa kuwa na tabia njema katika kuishi na wanajamii wengine. Inawafunza wanajamii kuishi vyema na majirani na watu wengine katika sehemu mbalimbali za jamii hiyo. Inatufuza kuwa tukiwa na tabia njema watu katika jamii wataturidhia na kutupenda na hata kutuheshimu. Inawakataza wanajamii kuwa na tabia mbaya ya kutojiheshimu katika maisha yao ya ndoa kwani jambo hilo linaweza kuvuruga ndoa hizo.

Kasida inatuelekeza katika matumizi mazuri ya midomo yetu. Haifai kwa mtu kupayuka maneno yasiyokuwa na faida na maneno yenye kuleta madhara kwa jamii. Matusi na maneno yasiyofaa huleta mfarakano miongoni mwa wanajamii. Kasida inaeleza.

Chunga kinywa chako Ukijisemea
Ili hadhi yako Izidi kung'aa
Wacha micharuko Ya kuruka njia
Dada kazi kwako Kufata wasia

Kama inavyoeleza, kasida hii inawafunza wanajamii na hasa wale walioolewa kujituliza na kuzungumza maneno mazuri yanayojenga jamii safi. Maneno machafu kama vile matusi hupunguza hadhi na heshima ya mzungumzaji. Inawakataza kufanya mambo machafu na yasiyoleta faida kwa jamii kama vile vitendo vya uasharati.

### 4.13.4 Utekelezaji wa Ahadi

Utekelezaji wa ahadi katika jamii ni jambo muhimu ili kuleta utengamano miongoni mwao. Jamii inatakiwa kutekeleza ahadi zao walzoziweka ili kudhihirisha ukweli wao. Katika kasida nyigi za nadhiri dhamira za utekelezaji wa ahadi hujitokeza kwa tendo lenyewe la kuweka nadhiri ambalo huambatana na ahadi.

Mikono yako miwili Kwa wema ilinyanyuka
Maombi yaso dosari Kwa mola ukapelekwa
Kizazi kilo kizuri Mzazi uweze pata
Leo kwako ni fakhari Hili limeshatimika

| | |
|---|---|
| Uliiweka nadhiri | Ilo njema bila shaka |
| Hilo litakapojiri | Maulidi utaweka |
| Kwa mola wetu kahari | Kilio kikasikika |
| Zawadi ilo jamili | Kwako wewe ikaletwa |
| | |
| Sala zako ulosali | Vizuri zimejibika |
| Ukahisi ni vizuri | Wanafunzi kutuita |
| Ikiwa yako dhamiri | Maulidi kujaweka |
| Nasi bila ya kujali | Leo hapa tumefika |
| | |
| Nasi leo tutayari | Dua njema kuzileta |
| Aepukane na shari | Mtoto alozalika |
| Afate njia halali | Na haramu kuiacha |
| Lengo zote idhilali | Kwake ziweze ondoka |

Katika kasida hii tumeona kuwa yule anaesomewa kasida alieka ahadi (nadhiri) ya kusoma maulidi ikiwa atapata mtoto. Aliomba dua kwa Allah (S.W) ili apate mtoto huyo. Alipompata mtoto alihitajika atekeleze ile ahadi aliyoiweka hapo mwanzo. Hivyo akaamua kuwaita wanafunzi wa madrasa ili wamsomee maulid aliyoahidi na kumuombea dua mtoto wake.

### 4.13.5 Kuwaheshimu Wazazi

Wazazi ndio chanzo cha kupatikana kwa kizazi. Ni wajibu wa watoto kuwaheshimu na kuwatumikia wazazi wao ili nao wajisikie wanaishi kwa amani na upendo hasa wanapokua watu wazima. Wakati huu ni wakati ambao wazazi huuhitaji zaidi msaada wa watoto wao. Dhamira hii imezungumziwa katika kasida kama ifuatavyo

Huzuni moyoni mwangu — Kwa kufikiri dunia
Nashindwa na malimwengu — Kwa nnayoshuhudia
Musinitupe wanangu — Shikeni wangu wasia
Hino ndio hali yangu — Kuliko kunikimbia

Hapa mzazi analalamika kutokana na kukimbiwa na kutupwa na watoto wake. Kumkimbia mzazi kunaashiria kutokuwajali na kuwaheshimu wazazi hao. Ni wajibu wa kila mtoto kuwaheshimu wazazi wake ili waweze kuishi maisha mema na ya furaha hapa duniani. Sio busara kuwaasi na kutowaheshimu wazazi kwani kutowaheshimu wakati wa uzee wao. Kuwakimbia kunawafanya waishi maisha ya tabu na huzuni baada ya kumlea mtoto wao tokea utotoni kwake.

### 4.13.6 Umuhimu wa Malezi Bora

Malezi ya wazazi katika kuwaandaa watoto wao kuishi vyema katika jamii ni muhimu. Wazazi hutakiwa kuwapatia watoto wao malezi bora ili wajewaishi vyema katika jamii zao. Miongoni mwa tabia njema wanazofunzwa watoto ni kuwa na adabu njema ili waweze kuishi katika jamii bila ya kupata tabu. Pia hufunzwa kujiheshimu popote wawapo. Hili huwaawezesha kuishi kwa kujiamini na kuaminiwa. Kasida ifuatayo inaonesha dhamira hii kama ifuatavyo:

1. Ngome iliyo adhimu — Wazazi wao hulinda
   Huinza na mapema — Dhumuni lao kulenga
   Awe wao msichana — Adabu mweye kutenda
   Humpa mafunzo mema — Hasa kwa somo huenda

2. Na humuambia umekua — Unayotakiwa kufanya haya
   Hufanya kila aina — Mwana asije kupinda

| | |
|---|---|
| Hulinda yake heshima | Kwa kila anaporanda |
| Huipalilia vyema | Ipendeze yao shamba |
| 3. Ili atokujavuna | Isije ikamshinda |
| Humsimamia, humfatilia | Asijepotea njia mbaya |
| Leo sasa twawaona | Wazazi wanavyotamba |
| Wamefurahika sana | Wamejifunga na kanga |
| 4. Kazi waliyoifanya | Mwana kumuenga enga |
| Leo wanampa bwana | Mwenyewe alompenda |
| Wanafurahia wanafamilia | Kwa kuwafikia harusi murua |

Kasida hii inatuekea wazi umuhimu wa kuwafunza watoto tabia njema. Tabia njema hujengwa kutokana na malezi bora ya wazazi kwa watoto wao. Malezi bora humfanya mtoto aweze kujifahamu na kujiheshimu. Hali hii hupelekea wazazi kufurahia tabia za mtoto wao popote aendapo kwani humuamini. Kwa mfano siku ya harusi, wazazi huwa hawana wasiwasi juu ya maisha ya ndoa ya mtoto wao kutokana na malezi waliyomlea mtoto huyo. Wanaamini kuwa ataishi vyema katika maisha hayo kutokana na tabia njema walizomfundisha. Hivyo huwafanya kuwa na furaha na kushereheka kwa amani na kujiamini bila ya wasiwasi juu ya mtoto wao kutokana na tabia njema alizozionesha wakati wa utoto wake. Kinyume chake kwa mtoto mwenye tabia mbaya huwakosesha raha wazazi wake kwani hawajui ataishi vipi na mwenza wake katika maisha ya ndoa.

## 14 Hitimisho

Katika sehemu hii dhamira mbalimbali za kasida za wakati wa soko huria zimejadiliwa. Dhamira kama vile kuelimisha jamii, kumsifu Mtume Muhammad

(S.A.W), kuwa na tabia njema, utekelezaji wa ahadi, kuwaheshimu wazazi na umuhimu wa malezi bora zimejadiliwa. Mabadiliko yaliyoonekana ni kwamba kasida nyingi za wakati wa baada ya mapinduzi zilikuwa na dhamira zilizohusu kumsifu Mtume, na wasia kwa jamii. Kasida za wakati wa soko huria zinaelezea dhamira zinazohusu zaidi mambo ya kijamii kama vile dhamira zinazopatikana katika kasida za harusi na kasida zinazokemea tabia mbaya za vijana zinazotokana mabadiliko ya tabia ya vijana hao.

## 4.15 Uchambuzi wa Data Zilizokusanywa Maskanini

Idadi wa watafitiwa waliohojiwa katika utafiti huu ni 100. Mtafiti amefanikiwa kuwahoji watafitiwa 50 wanawake na 50 wanaume sawa na asilimia 100% ya watafitiwa wote waliotarajiwa kutafitiwa katika madrasa mbalimbali za wilaya ya Magharib. Wazee wote, wanawake na wanaume ni asilimia 20%, walimu wa mad-ras, wanawake na wanaume ni 20%, wanafunzi wa mad-ras, wanawake na waaume ni asilinmia 20%, waandishi wa habari wanawake na wanaume ni asilimia 20%. Na wapenzi wa kasida, wanawake na wanaume ni asilimia 20%. Wote kwa ujumla ni asilimia 100% ya watafitiwa. Maswali ya hojaji yalitumika katika kukusanya data hizi. Majibu ya maswali hayo na maoni ya watafitiwa yameoneshwa hapa chini kama ifuatavyo:

Jedweli Na 4. 1: Orodha ya Wahojiwa

| Kundi | Wanawake | Wanaume | Jumla | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Wazee | 10 | 10 | 20 | 20% |
| Walimu Wa Mad-Ras | 10 | 10 | 20 | 20% |
| Wanafunzi Wa Mad-Ras | 10 | 10 | 20 | 20% |
| Waandishi Wa Habari | 10 | 10 | 20 | 20% |
| Wapenzi Wa Kasida | 10 | 10 | 20 | 20% |
| Jumla Kuu | 50 | 50 | 100 | 100% |

Chanzo: Utafiti (2016)

### 4.15.1 Njia za Ukusanyaji wa Data Zilivyofanikisha Lengo

Njia na mbinu za utafiti zilzotumika katika kukusanya data kutoka kwa watafitiwa hao, zilifanikisha lengo na madhumuni ya utafiti huu. Majibu ya maswali ya utafiti waliyoulizwa watafitiwa yametolewa ufafanuzi kama ifuatavyo:

### 4.15.2 Aina za Kasida

Madhumuni ya kwanza ya utafiti huu ni kuainisha aina za kasida zinazosomwa katika jamii. Madhumuni haya yaliongozwa na swali, Je, ni kasida za aina gani zilisomwa baada ya mapinduzi na wakati wa soko huria katika jamii ya Wazanzibari?

Kwa mujibu wa majibu ya watafitiwa, wazee 18 kati ya 20 ambao kati yao, wanawakwe ni 10 Na wanaume 08 sawa na asilimia 90% ya wazee wote, wameeleza kuwa zipo aina mbalimbali za kasida katika jamii ya Wazanzibari. Kwa maelezo yao kasida nazo hutegemea matukio maalum katika uwasilishwaji wake kama vile sherehe za kuzaliwa kwa Mtume Muhammad, harusi, kuzaliwa kwa mtoto, kuondoa nadhiri na katika khitima. Watafitiwa waliobakia, ambao ni wanaume wawili (2) sawa na asilimia 10% hawakuweza kufafanua kuhusu matukio muhimu ambayo kasida husomwa.

**Jedweli Na 4.2: Watafitiwa Wazee Wanaoeleza Aina za Kasida**

| Wazee | Aina Mbalimbali za Kasida | Asilimia | Hawapambanui Aina za Kasida | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Wanawake | 10 | 50% | - | 00% |
| Wanaume | 08 | 40% | 02 | 10% |
| **Jumla** | **18** | **90%** | **02** | **10%** |

Chanzo: Utafiti (2016)

Walimu wa madrasa waliohojiwa walikua 20, ambao wanaume ni 10 na wanawake ni 10. Wanaume wote 10 ambao ni sawa na aslimia 50% n wanawake wote 10, ambao ni sawa na asilimia 50%, wameeleza kuwa zipo aina mbalimbali za kasida. Wameeleza kwamba kasida huambatana na matukio.

Wanafafanua kuwa zipo kasida zinazosomwa wakati wa sherehe za mauled ya kuzaliwa kwa Mtume Muhammad, katika sherehe za harusi, katka kuwasomea dua watoto na katika sherehe za serikali. Watafitiwa wote wanaume na wanawake wameweza kueleza aina mbalimbali za kasida kupitia matukio yanayoambatana na usomwaji wa kasida.

**Jedweli Na 4.3: Walimu wa Mad-Rasa Wanaozieleza Aina za Kasida**

| Walimu wa Mad-Rasa | Aina Mbalimbali za Kasida | Asilimia | Hawapambanui Aina za Kasida | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Wanaume | 10 | 50% | 00 | 00% |
| Wanawake | 10 | 50% | 00 | 00% |
| Jumla | 20 | 100% | 00 | 00% |

Chanzo: Utafiti (2016)

Wanafunzi wa mad-rasa wote ni 20 ambao ni sawa wanaume 10 na wanawake 10 sawa na asilimia 100%, wameeleza kuwa zipo aina mbalimbali za kasida kutokana na matukio maalum yanayoambatana na usomaji wa kasida. Wameeleza kuwa zipo kasida zinazosomwa wakati wa sherehe za mauilid ya kuzaliwa Mtume Muhammad, katika sherehe za harusi, kuwaombea dua watoto na zinazosomwa wakati wa sherehe mbalimbali.

**Jedweli Na 4. 4: Wanafunzi wa Mad-Rasa Wanaoeleza Aina za Kasida**

| Wanafunzi Wa Mad-Rasa | Aina Mbalimbali za Kasida | Asilimia | Hawapambanui Aina za Kasida | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Wanaume | 10 | 50% | 00 | 00% |
| Wanawake | 10 | 50% | 00 | 00% |
| **Jumla** | **20** | **100%** | **00** | **00%** |

Chanzo: Utafiti (2016)

Jumla ya waandishi wa habari 20 walikuwa ni miongoni mwa watafitiwa waliohojiwa. Kati yao wanaume 10 na wanawake walikua10 sawa na asilimia 100%. Wameeleza aina mbalimbali za kasida zinazosomwa katika matukio mbalimbali kama vile sherehe za harusi, sherehe za kuzaliwa kwa Mtume Muhammad, sherehe za serikali, dua za watoto na kuondoa nadhiri.

**Jedweli Na 4.5: Waandishi wa Habari Wanaoeleza Aina za Kasida**

| Waandishi Wa Habari | Aina Mbalimbali za Kasida | Asilimia | Hawapambanui Aina za Kasida | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Wanaume | 10 | 50% | 00 | 00% |
| Wanawake | 10 | 50% | 00 | 00% |
| **Jumla** | **20** | **100%** | **00** | **00%** |

Chanzo: Utafiti (2016)

### 4.16 Vipengele Vya Fani Vinavyotumika Katika Kasida

Madhumuni ya pili ya utafiti huu yalikua ni kuainisha vipengele vya fani vinavyotumika katika. Kasida za Kiswahili. Madhumuni haya yaliongozwa na swali la pili, lililoulizwa kuwa, Je, ni vipengele gani vya fani vinavyojitokeza katika fasihi

ya kasida katika awamu hizi mbili?Walimu wa mad-ras 20 kati ya 20 walihojiwa, ambao wanaume ni 10 na wanawake ni 10 sawa na asilimia 100% wametaja vipengele vya fani vinavyojitokeza katika kasida kuwa ni muundo, mtindo na matumizi ya lugha. Wameeleza kuwa kuna miundo mbalimbali ya kasida kama vile miundo ya vina, mizani na beti. Pia wameeleza mitindo inayotumiwa katika kasida kama vile mtindo wa mshangao, mtindo wa takriri na mtindo wa kutumia nafsi. Katika matumizi ya lugha, kuna matumizi ya lugha za lahaja, lugha ya Kiarabu. Matumizi ya vipengele vya fani husaidia katika kuibua maudhui na pia husaidia kuipamba kazi ya fasihi na kuifanya iwe na mvuto kwa wasomaji na wasikilizaji wa kasida.

**Jedweli Na 4.6: Walimu wa Mad-Rasa Wanaoeleza Vipengele vya Fani Katika Kasida**

| **Walimu wa Mad-Rasa** | **Vipengele Vya Fani Katika Kasida** | **Asilimia** | **Wasioeleza Vipengele Vya Fani** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|---|
| Wanaume | 09 | 45% | 01 | 05% |
| Wanawake | 08 | 40% | 02 | 10% |
| **Jumla** | **17** | **85%** | **03** | **15%** |

Chanzo: Utafiti (2016)

Wanafunzi wa mad-rasa waliohojiwa walikuwa 20, ambapo wanaume walikua 10 na wanawake ni 10. Watafitiwa 16 kati 20 wameeleza vipengele mbalimbali vya fani vinavyotumika katika kasida.kama vile muundo, mtindo na matumizi ya lugha na matumizi ya nafsi. Wamedhihirisha kuwa kuna miundo tafauti ya kasida kama vile matumizi ya vina na mizani. Pia wameeleza mitindo inayotumika katika kasida kama

vile mtindo wa mshangao, matumizi ya takriri na matumizi ya lugha mchanganyiko katika utungaji na uwasilshaji wa kasda.

**Jedweli Na 4.7: Wanafunzi Wanaoeleza Vipengele vya Fani katika Kasida**

| **Wanafunzi wa Mad-Rasa** | **Vipengele vya Fani Katika Kasida** | **Asilimia** | **Wasioeleza Vipengele vya Fani** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|---|
| Wanaume | 09 | 45% | 01 | 05% |
| Wanawake | 07 | 35% | 03 | 15% |
| **Jumla** | **16** | **80%** | **04** | **20%** |

Chanzo: Utafiti (2016)

Wazee waliohojiwa walikua 20, kati yao 10 ni wanaume na 10 ni wanawake. Watafitiwa 15 kati ya 20 wameeleza vipengele mbalimbali vya fani vinavyotumika katika kasida. Watafitiwa 5 ambao wanaume ni 3 na wanawake ni 2 wameshindwa kueleza vipengele vya fani katika kasida.

**Jedweli Na 4.8: Wazee Wanaelezea Vipengele vya Fani Katika Kasida**

| **Wazee** | **Vipengele vya Fani** | **Asilimia** | **Wasioeleza Vipengele vya Fani** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|---|
| Wanaume | 07 | 35% | 03 | 15% |
| Wanawake | O8 | 40% | 02 | 10% |
| **Jumla** | **15** | **75%** | **05** | **25%** |

Chanzo: Utafiti (2016)

### 4.17 Dhamira za Kasida

Madhumuni ya tatu ya utafiti huu yalikuwa ni kubainisha dhamira mbalimbali za kasida. Madhumuni haya yaliongozwa na swali lililoulizwa kuwa, Je, ni dhamira zipi zinazojitokeza katika kasida katika awamu mbili zilizotajwa? Walimu wa mad-rasa

20 waliohojiwa, ambapo wanaume ni 10 na wanawake ni 10. Watafitiwa wote wameeleza dhamira tafauti zinazopatikana katika kasida kama vile kuhabarisha, kuelimisha, kufunza mambo mema na kukataza mabaya, umuhimu wa tabia njema, kuwafunza maharusi na kuikosoa jamii juu ya mambo yasiyofaa. Wameendelea kueleza kuwa maudhui hayo hutofautiana kutokana na matukio yanayoambatana na usomwaji wa kasida hizo.

Kila tukio huweza kubeba maudhui tafauti ukilinganisha na tukio jengine. Kwa mfano kasida zinazosomwa katika sherehe za maulid ya kuzaliwa Mtume, hueleza sifa na maisha ya Mtume aliyoishi hapa duniani na zile za harusini huzungumzia maudhui yanayoendana na harusi kama kuwafunza maharusi kuhusu maisha ya ndoa.

**Jedweli Na 4. 9: Walimu Wanaoeleza Dhamira za Kasida**

| Walimu wa Mad-Rasa | Wanaoeleza Dhamira za Kasida | Asilimia | Wasioeleza Dhamira za Kasida | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Wanaume | 10 | 50% | 00 | 00% |
| Wanawake | 10 | 50% | 00 | 00% |
| **Jumla** | **20** | **100%** | **00** | **00%** |

Chanzo: Utafiti (2016)

Wanafunzi wa mad-rasa waliohojiwa walikuwa 20, miongoni mwao 10 ni wanaume na10 ni wanawake. Wahojiwa 10 wanaume wameeleza dhamira za kasida na wanawake 09 wameeleza dhamira hizo. Mwanamke mmoja (01) sawa na asilimia 05% ameshindwa kueleza dhamira za kasida.

**Jedweli Na 4.10: Wanafunzi Wanaoeleza Dhamira Za Kasida**

| Wanafunzi wa Mad-Rasa | Wanaoeleza Dhamira za Kasida | Asilimia | Wasioeleza Dhamira za Kasida | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Wanaume | 10 | 50% | 00 | 00% |
| Wanawake | 09 | 45% | 01 | 05% |
| **Jumla** | **19** | **95%** | **01** | **05%** |

Chanzo: Utafiti (2016)

Wasikilizaji wa kasida waliohojiwa walikua 20. Miongoni mwao wanaume ni 10 na wanawake ni 10. Watafitiwa 09 wanaume na 10 wanawake wameeleza kuwa kasida zina dhamirambalimbali katika jamii ya Wazanzibari. Wameeleza dhamira hizo kuwa ni kufunza mambo mema, kuburudisha jamii, kufunza maadili, umuhimu wa malezi bora, kusisimua, na kuishi vyema katika maisha ya ndoa.

**Jedweli Na 4.11: Wasikiliza Wanaoeleza Dhamira za Kasida**

| Wasikilizaji wa Kasida | Wanaoeleza Dhamira za Kasida | Asilimia | Wasioeleza Dhamira za Kasida | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Wanaume | 09 | 40% | 01 | 10% |
| Wanawake | 10 | 50% | 00 | 00% |
| **Jumla** | **19** | **90%** | **01** | **10%** |

Chanzo: Utafiti (2016)

Data zilizokusanywa katika utafiti huu zinathibitisha kuwa kasida zina maudhui mbalimbali yanayokusudiwa yawafikie wanajamii. Maudhui hayo hutafautiana kulingana na mazingira na matukio yanayoambatana na usomaji wa kasida hizo. Jamii hufaidika na kasida kwa kujifunza mambo mbalimbali yanayohusiana na

maisha yao pamoja na dini yao. Pia zinatumika katika kuiburudishsa jamii katika sherehe mbalimbali zinazojitokea katika jamii. Kutokana na utafiti huu kasida huwafunza maharusi na kuwatayarisha kuishi vyema katika maisha yao ya ndoa. Vijana na wasikilizaji wa kasida huburudika kwa kuangalia na kusikiliza kasida.

Watafitiwa, wanaona kuwa ipo haja kwa usomaji wa kasida kusimamiwa vyema ili zisitoke katika maadili na maudhui yanayokusudiwa kwani fani hii imevamiwa na watu wengi na kuwa inapoteza uhalisia wake. Wazee wanakosoa utaratibu unaotumika katika uwasilishaji na utugaji wa kasida kwani kasida za kisasa zinaambatana na mchanganyiko mkubwa wa wanawake na wanaume namatumizi makubwa ya vifaa (zana) za kisasa kama vile vinanda na ala za muziki ambapo haziwezi kutafautika na miziki mengine.

### 4.18 Mabadiliko Katika Kasida

Madhumuni ya nne ya utafiti huu yalikua ni kubainisha mabadiliko ya kifani na kimaudhui yaliyoingia katika kasida katika kipindi cha awamu mbili za maendeleo ya watu wa Zanzibar. Lengo hili liliongozwa na swali, Je, ni mabadiliko gani ya kifani na kidhamira yaliyojitokeza katika kasida katika awamu mbili zilizoainishwa.

Kwa mujibu wa majibu ya watafitiwa, walimu wa mad-rasa 20 walihojiwa, miongoni mwao 10 ni wanaume na 10 ni wanawake sawa na asilimia 100%. Watafitiwa hao wameeleza mabadiliko mbalimbali yaliyotokea katika kasida. Wameeleza kuwa mabadiliko hayo yamo katika vipengele vya fani kama uwasilishaji wa kasida na dhamira zinazopatikana katika kasida.

**Jedweli Na 4. 12: Walimu wa Mad-Rasa Wanaoeleza Mabadiliko Ya Kasida**

| Walimu Wa Mad-Rasa | Wanaoeleza Mabadiliko Katika Kasida | Asilimia | Wasioeleza Mabadiliko Katika Kasida | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Wanaume | 10 | 50% | 00 | 50% |
| Wanawake | 10 | 50% | 00 | 50% |
| **Jumla** | **20** | **100%** | **00** | **100%** |

Chanzo: Utafiti (2016)

Wanafunzi wa mad-rasa 20 wamehojiwa, miongoni mwao 10 ni wanaume na 10 ni wanawake, sawa na asilimia 100%. Wanaume 08 kati ya 10 sawa na asilimia 40% na wanawake 09 kati 10 sawa na asilimia 45% wameeleza mabadiliko katika kasida. Katika uwasilishaji wake wameeleza kuwa, kasida hivi sasa huwasilishwa kwa mchangayiko mkubwa kati ya wanawake na wanaume. Pia watu huwa wanacheza kama wanavyocheza ngoma, jambo ambalo kwa maoni yao hayaendani na uwasilishaji wake hapo zamani ambapo wasomaji na wasikilizaji walikaa kitako bila ya kucheza, wao walikua waangaliaji tu. Wameeleza kuwa hata maudhui yake kwa sasa huwa yako wazi zaidi kuliko za zamani ambapo maudhui yake yalikua yamejificha.

**Jedweli Na 4.13: Wanafunzi wa Mad-Rasa Wanaoeleza Mabadiliko ya Kasida**

| Wanafunzi wa Mad-Rasa | Wanaoeleza Mabadiliko Katika Kasida | Asilimia | Wasioeleza Mabadiliko Katika Kasida | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Wanaume | 08 | 40% | 02 | 10% |
| Wanawake | 09 | 45% | 01 | 05% |
| **Jumla** | **17** | **85%** | **03** | **15%** |

Chanzo: Utafiti (2016)

Waandishi wa habari 20 walihojiwa, miongoni mwao 10 ni wanaume na 10 ni wanawake. Watafitiwa 09 wanaume wameweza kueleza mabadiliko katika kasida na wanawake 07 wameeleza mabadiliko yanayojitokeza katika kasida. Wameeleza kuwa kasida za zamani hazikuwasilishwa kwa vinanda, za sasa ni za kibiashara, zinaonesha uhlisia wa yanayotokea katika jamii, zinaeleza kuhusu mporomoko wa maadili na za sasa ni za kuburudisha zaidi.

**Jedweli Na 4.14: Waandishi wa Habari Wanaoeleza Mabadiliko Katika Kasida**

| Waandishi wa Habari | Wanaoeleza Mabadiliko Katika Kasida | Asilimia | Wasioeleza Mabadiliko Katika Kasida | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Wanaume | 09 | 45% | 01 | 05% |
| Wanawake | 07 | 35% | 03 | 15% |
| **Jumla** | **16** | **80%** | **04** | **20%** |

Chanzo: Utafiti (2016)

Wazee 20 wamehojiwa kuhusu mabadiliko katika kasida. Miongini mwao wanaume ni 10 na wanawake ni 10. Watafitiwa wote 20 wameweza kueleza mabadiliko yaliyotokea katika kasida. Wameeleza kuwa uwasilishaji wa sasa unaondoa uhalisia wa kasida kutoka za kidini na kuwa za kitamaduni, za sasa hutumia vinanda na ala za muziki, za zamani zilikua na utaratibu na utulivu, za sasa zinazungumzia hata masuali ya siasa badala ya dini, za sasa zinachanganya dhamira.

**Jedweli Na 4.15: Wazee Wanaoeleza Mabadiliko katika Kasida**

| Wazee | Wanaoeleza Mabadiliko Katika Kasida | Asilimia | Wasioeleza Mabadiliko Katika Kasida | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Wanaume | 10 | 50% | 00 | 00% |
| Wanawake | 10 | 50% | 00 | 00% |
| **Jumla** | **20** | **100%** | **00** | **00%** |

Chanzo: Utafiti (2016)

Wasikilizaji wa kasida 20 wamehojiwa, kati yao wanaume ni 10 na wanawake ni 10. Watafitiwa 09 wanaume na 08 wanawake wameweza kueleza mabadiliko katika kasida. Wameeleza kuwa maendeleo ya sayansi na teknolojia na kutanuka kwa soko la biashara ya kasida yamesababisha mabadiliko makubwa katika kasida.

**Jedweli Na 4. 16: Wasikilizaji Wanaoeleza Mabadiliko katika kasida**

| Wasikilizaji wa Kasida | Wanaoeleza Mabadiliko Katika Kasida | Asilimia | Wasioweza Kueleza Mabadiliko Katika Kasida | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Wanaume | 09 | 45% | 01 | 05% |
| Wanawake | 08 | 40% | 02 | 10% |
| **Jumla** | **17** | **85%** | **03** | **15%** |

Chanzo: Utafiti (2016)

Data zilizokusanywa zinathibitisha kuwa kuna mabadiliko yaliyotokea katika kasida kutokana na Maendeleo ya sayansi na teknolojia. Utafiti umegundua mabadiliko katika uwasilishaji wa kasida zenyewe, kwani kasida hivi sasa huwasilishwa kwa kutumia vifaa vya kisasa kama vile kwa kutumia vipaza sauti, vinanda, na maiki. Utafiti umegundua kuwa kasida za zamani zilisomwa bila kutumia vifaa hivi. Zilisomwa kwa mdomo mtupu au kwa kutumia madufu. Pia za zamani ziliwasilshwa na watu wa jinsia moja bila ya mchanganyiko wajinsia kama zinavyowasilishwa hivi sasa. Kwa upande wa maudhui, kasida hivi sasa hubeba maudhui ya kijamii zaidi.

Huzungumzia mambo yanayotokea katika jamii kama vile mporomoko wa maadili. Kwa mfano Zipo zinazoiasa jamii kuacha kuwauwa walemavu wa ngozi (albino) na zile zinazowakataza wanajamii kuacha matumizi ya madawa ya kulevya. Kasida za

zamani zilielezea sifa za Mtume Muhammad na maisha yake aliyoishi hapa duniani na sifa za maswaha (wafuasi) wake ambazo baadhi yaken zinaendelea kusomwa. Pia zilikumbusha kuhusu maisha baada ya kufa na kuihimiza jamii kujitayarisha na maisha hayo kwa kufanya mambo mema. Kwa ujumla utafiti umeonesha ushiriki wa watafitiwa katika kutoa majibu sahihi ya maswali ya utafiti.

## 4.19 Upungufu wa Ukamilifu wa Utafiti

Utafiti si jambo rahisi, na pia hauachi kuwa na matatizo yake wakati wa kufanya utafiti huo. Utafiti huu ulikabiliwa na upungufu ufuatao:

### 4.19.1 Kasida nyingi hutumia lugha ya Kiarabu

Kasida nyingi zilizosomwa na watafitiwa zilitumia lugha mchanganyiko, kati ya lugha ya Kiarabu na Kiswahili ambapo mara nyengine ilikuwa ni vigumu kuzifahamu. Kasida nyengine zilitumia lahaja za kigeni kiasi ambacho baadhi ya maneno hayafahamiki vyema maana yake na Waswahili wa kawaida.

### 4.19.2 Baadhi ya Kasida Zilizosomwa na Watafitiwa Zilikuwa Fupi Mno

Kasida nyigi za zamani zilizosomwa na watafitiwa zilionekana kuwa fupi mno. Kwa mfano baadhi ya kasida zilkuwa na ubeti mmoja wenye mistari miwili au mitatu. Kwa hivyo kasida hizi hazikuwa na muendelezo.

## 4.20 Hitimisho

Sura hii imewasilisha na kuchambua data zilizokusanywa maskanini. Uchambuzi wa data hizo umechambua vipengele vya fani, dhamira na mabadiliko yaliyotokana na

maendeleo ya sayansi na teknolojia. Uchambuzi huo umeonesha maendeleo na mabadiliko yaliyotokea katika fasihi hii ya kasida katika vipengele vya fani na dhamira. Pia maendeleo na mabadiliko yameonekana katika uwasilishaji wa kasida katika sherehe mbalimbali. Matumizi ya vifaa vya kisasa vya muziki kwenye kasida ni mabadiliko ya wazi katika fani hii.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza mambo matatu makubwa na ya msingi. Jambo la kwanza ni kuelezea muhtasari wa tasnifu hii, jambo la pili ni kutoa matokeo ya utafiti huu kwa kuzingatia nadharia zilizotumika kutokana na madhumuni ya utafiti huu. Jambo la tatu ni kutoa mapendekezo yanayotarajiwa kuwa changamoto na chachu kwa watafiti wengine kufanya utafiti wa kasida katika vipengele vyengine na jamii nyengine.

## 5.2 Muhtasari wa Tasnifu

Tasnifu hii ilikusudia kukusanya na kuchambua data zinazoelezea mabadiliko ya Kasida Visiwani Zanzibar. Utafiti ulichunguza aina za kasida zinazosomwa katika matukio na sherehe zinazoambatana na usomwaji wa kasida. Utafiti ulizingatia vipengele vya fani, dhamira na mabadiliko yanayotokea katika kasida katika awamu mbili ambazo ni wakati wa baada ya mapinduzi na wakati wa soko huria. Katika vipengele vya fani, utafiti ulichunguza miundo ya kasida, mitindo na matumizi ya lugha.

Kwa upande wa maudhui, utafiti ulichunguza dhamira zinazopatikana katika kasida katika nyakati zilizochunguzwa. Pia, utafiti ulichunguza mabadiliko ya fani na dhamira yaliyotokea katika kasida kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Nadharia mbili zilitumika katika uchambuzi wa data za utafiti huu. Nadharia hizo ni Nadharia ya umuundo na nadharia ya sosholojia. Utoshelevu wa nadharia hizi umefanikisha katika kufikia lengo la utafiti.

Utafiti huu umegawanywa katika sura tano (5). Sura ya kwanza ni utangulizi, ambao umejumuisha usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, madhumuni maalum ya utafiti, Maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, vikwazo vya utafiti na utatuzi wake na mwisho ni hitimisho.

Sura ya pili ni utalii wa kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Sura hii ilishughulikia mapitio mbalimbali ya maandishi aliyoyasoma mtafiti kama vile vitabu, majarida na tasnifu. Imebainisha maandishi yaliyohusiana na kasida na vipengele vya fani na maudhui. Vilevile ilielezea mapitio yaliyoandikwa kuhusu maana ya kasida na dhana nyengine zinazohusiana na kasida. Sura hii, Pia iljadili nadharia mbili zilizotumika katika utafiti huu, ambazo ni nadharia ya umuundo Iliyochambua vipengele vya fani na nadharia ya sosholojia iliyochambua dhamira.

Sura ya tatu imeelezea mbinu na njia za utafiti. Sura hii imefafanua mbinu zilizotumika katika ukusanyaji na uchambuzi wa data. Mbinu hizo ni hojaji, usaili na kushiriki katika matukio zilizomsaidia mtafiti kupata data alizozichambua. Sura hii pia, imebainisha aina ya utafiti, Eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, usampulishaji. Pia ilibainisha vifaa vya utafiti ambavyo vilitumika kusaidia kufanikisha utafiti huu. Mwisho ilieleza vyanzo vya data ambavyo vilitumika kupata data za utafiti huu.

Sura ya nne ni uwasilishaji na uchambuzi wa data. Sura hii imewasilishwa na kuchambua data zilizokusanywa kutoka kwa watafitiwa. Imeainisha kasida zilizokusanywa maskanini/ au Uwandani na kuchambua vipengele vya fani. Dhamira na mabadiliko yaliyotokea katika kasida pia yamechunguzwa katika utafiti huu. Miongoni mwa dhamira zilizobainishwa katika utafiti huu ni kuelimisha, kuwa na

tabia njema, umoja na mshikamano, utekelezaji wa ahadi, umuhimu wa kutenda haki katika jamii, sifa za Mtume, kuwaheshimu wazazi na kuwakumbusha kuhusu maisha baada kifo zimechambuliwa.

Sura ya tano ni muhtasari wa utafiti, matokeo ya utafiti na mapendekezo. Sura hii inatoa muhtasari wa utafiti nzima kutoka sura ya mwanzo hadi ya mwisho. Vilevile sura hii inatoa mapendekezo yanayotokana na matokeo ya utafiti wenyewe, miongoni mwa mapendekezo hayo ni kuwataka wanajamii kusimamia utungaji na uwasilishaji wa kasida kwani fani hii ni muhimu kwao na kwa kizazi kijacho kutokana na mafunzo yanayopatikana. Pia kasida ni miongoni mwa utanzu wa zamani ulio na historia refu, kwa hivyo si vyema kuuacha kuvamiwa na watu wasiozigatia malengo ya utanzu huu. Kasida pia ni chuo bora kwa vijana na wanandoa katika maisha yao ya ndoa, huwafunza jinsi ya kuwa na ndoa bora na zenye upendo miongoni mwao.

## 5.3 Matokeo ya Utafiti

Katika utafiti huu, nadharia mbili zimetumika kuchambua data zinazohusiana na kasida za Kiswahili, kwa kuzingatia madhumuni maalum ya utafiti.

## 5.4 Nadharia za Utafiti

Nadharia hizo zilisaidia kukamilisha madhumuni ya utafiti na kujibu maswali ya utafiti, hivyo kukamilisha utafiti huu. Nadharia ya kwanza ya utafiti huu ni nadharia ya Umuundo. Nadharia hii ilisaidia kukamilisha madhumuni ya kwanza ya utafiti, ambayo ni kuainisha kasida zinazosomwa katika matukio mbalimbali. Nadharia hii

pia, ilisaidia kuchambua aina za kasida zinazosomwa hapa Visiwani Zanzibar. Pia nadharia hii imesaidia kukamilsha na kuchambua madhumuni ya pili, ambayo yalikuwa ni kuainisha vipengele vya fani. Vipengele mbalimbali vimeainishwa na kuchambuliwa. Hivyo nadharia hii ilisaidia katika kuvichambua vipengele hivyo.

Nadharia ya pili ni nadharia ya sosholojia ambayo ilisaidia kukamilisha madhumuni ya tatu ya utafiti, kwa kuchunguza vipengele vya dhamira vilivyotumika katika kasida. Vipengele hivyo vimechambuliwa kama vilivyoainishwa na watafitiwa. Miongoni mwa dhamira zilizoainshwa katika kasida ni kumsifu Mtume Muhammad, kuelimisha jamii juu ya yanayowapasa kuyafanya katika kipindi chote cha maisha yao hapa duniani na kuionya jamii juu ya maovu wanayoyafanya. Pia nadharia hii imesaidia katika ubainishaji na uchambuzi wa data zilizohusiana na mabadiliko katika kasida kutokana na maendeleo ya sayansi na teknnolojia. Hivyo ilisaidia katika kuchambua mabadiliko hayo ambayo yalikua ni miongoni mwa madhumuni ya utafiti huu.

## 5.5 Mapya ya Utafiti

Mapya yaliyojitokeza katika utafiti huu ni kwamba, jamii ya Wazanzibari nayo imeathiriwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Baadhi ya waandaaji wa kasida wameacha kuandaa kasida zinazomsifu Mtume Muhammad na kutunga kasida zinazoelezea mambo ya kijamii. Kasida zinazotungwa hivi sasa sio za kidini badala yake zimekua ni za kijamii na kibiashara, hivyo kupoteza uhalisia wake. Uwasilishaji wa kasida pia, umekua tafauti na ule uwasilishaji wa miaka ya kipindi cha kabla ya soko huria na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Hivi sasa kasida huwasilishwa kwa mchanganyiko wa kijinsia. Pia, wasomaji wa kasida katika sherehe mbalimbali

wakati huu ni vijana wa mitaani badala ya wanafunzi wa mad-rasa (chuoni) ambapo, zamani kasida zilisomwa na watoto (wanafunzi) wadogo wadogo au watu wazima katika matukio maalum. Matumizi ya vyombo na ala za kisasa za muziki ni baadhi ya mambo yaliyobainika katika uwasilishaji wa kasida. Maudhui ya kasida kwa mujibu wa watafitiwa umekua wa kupigana vijembe baina chuo na chuo. Vifaa hivi kama vile vinanda vimeelezwa kuwa vinabadilisha mtazamo na muonekano wa kasida na kufananishwa na muziki au taarab.

Aidha, mtafiti alipohudhuria katika baadhi ya sherehe kama vile harusi, aliwaona watu mchanganyiko wakicheza wakati wa usomaji wa kasida kwa kuzunguka bila kujali utaratibu wa kidini wa kutochanganyika kijinsia na wanawake kutokuonyesha mapambo yao na kunyanyua sauti zao mbele ya wanaume. Jambo hili linakemewa sana na wazee huku wakieleza kuwa kasida ziliwasilishwa kwa heshima na kulinda mipaka ya dini wakati wa zama zao tafauti na hivi sasa.

## 5.6 Hitimisho

Utafiti huu unahitimisha kwamba, maendeleo ya sayansi na teknolojia, maingiliano ya watu, na mabadiliko ya jamii kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni yana athari kubwa katika kubadilisha mila na desturi za jamii. Mtafiti wa utafiti huu, anathibitisha na kukiri kuwa endapo jamii hazitachukua tahadhari mila na desturi za jamii zikiwamo kasida zitapotea. Kasida katika jamii ya Wazanzibari zina mchango mkubwa kwa jamii kwani zinafunza mambo mema na kukataza maovu. Pia ziawakumbusha wanajamii umuhimu wa kuishi vyema katika jamii kwa kuheshimu kanuni na taratibu za maisha ya kila siku. Ni vyema kwa jamii kuzingatia yale mafunzo mema

yanayopatikana katika kasida ili kudumisha mila, silka na utamaduni wa Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla.

### 5.7 Mapendekezo

Kwa kiasi kikubwa utafiti huu umesaidia kuwakumbusha wanajamii juu ya maendeleo na mabadiliko ya kasida pamoja na dhamira zinazopatikana katika kasida. Unakumbusha kuwa dhamira za kasida hutafautina kutokana na matukio, wahusika na mahala zinapowasilishwa. Kasida ni sehemu ya utamaduni wa Wazanzibari, Watanzania na jamii ya Kiislamu kwa ujumla. Kwa hivyo wanajamii hasa jamii ya Wazanzibari wanawajibu wa kuzienzi, kuzidumisha na kuziendeleza kasida ili kuzirithisha kwa vizazi vijavyo.

Kasida ni sehemu ya utamaduni wa jamii ya Wazanzibari na pia ni utanzu mmojawapo wa fasihi simulizi. Hivyo ni vyema kwa waandishi na wahakiki wa kazi za fasihi kujadili na kutilia mkazo katika uandishi wa kipengele hiki cha kasida kama vinavyofafanuliwa vipengele vyengine vya fasihi katika vitabu vyao. Zifannyiwe kazi kwa kina na kuenziwa kwa mapana ili ziweze kurithishwa kwa vizazi vijavyo.

Jamii iziangalie kasida kwa mtazamo chanya, kwani zina dhima kubwa na manufaa mengi kwa wanajamii. Halikadhalika, jamii zijali, kuheshimu na kuzingatia mipaka ya kasida ili kuepuka vikwazo viavyojitokeza na kuenzi uhalisia wake katika muda ujao. Walimu wa mad-rasa na watunzi wa kasida wazingatie malengo ya kasida ili ziweze kubakia katika uhalisia wake. Waache tamaa za nafsi zao kwa kuzifanya kasida ni biashara na chanzo cha mapato katika maisha yao. Watunge kasida zitakazoleta faida na manufaa katika jamii badala ya zile zenye kuigawa jamii.

Wataalamu wengine zaidi wakifanyie kazi kipengele hiki cha kasida za Kiswahili ili jamii izidi kushawishika, kuzipenda, kuzithamini kuziendeleza na kuzihifadhi. Pia wataalamu wengine zaidi wazifanyie kazi, kwa kufanya tafiti zaidi ili kuona mitazamo ya jamii nyengine juu ya kipengele hiki cha kasida za Kiswahili hasa ukizingatia jamii nyingi zimeathiriwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia na utandawazi, na hivyo baadhi ya tamaduni zimeathiriwa ikiwamo hii ya kasida za Kiswahili.

Vyombo vya habari, mabaraza ya Kiswahili na taasisi mbalimbali za elimu ziwe mstari wa mbele kuelimisha, kukuza, kudumisha na kuendeleza mila na desturi za jamii, kwa kuzipa kipaumbele kazi za fasihi. Wizara ya elimu na mafunzo ya Amali ya Zanzibar, itumie njia mbalimbali kuielimisha jamii juu ya malengo ya utafiti, watafiti na faida za kazi zao. Pia, wizara hii iwashajihishe na kuwasaidia watafiti kwa mbalimbali kwa kuwadhamini ili kukamilisha tafiti zao kwani zina faida kubwa kwa jamii.

Katika wilaya na shehia kuwe na maktaba, ofisi au chumba maalum cha kuhifadhi tafiti zinazofanyika ambazo zitawawezesha watafiti wapya kupata marejeleo kutoka katika tafiti zilizopita.

**MAREJELEO**

Abeid, K. (1973). *Sheria za Kutunga Mashairi ya Diwani,* Dar es Salaam: East Africa literature Bureau.

Abobakar, E. (2013). *Maendeleo ya Lugha ya Kiswahili na athari zake kwa jamiiya Kiarabu*. Dar-es-Salaam: The Open University of Tanzania.

Babie, E, (1999), *The Basics of Social Research*. Belmont: Wadsorth Publishing Company.

BAKITA, (2004). *Makala za siku ya Kiswahili .Kiswahili na Utandawazi*. Dar es Salaam. Baraza la Kiswahli la Taifa.

BAKIZA, (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Zanzibar. Literature Bureau.

Creswell, J. (2009), *Qualitative, Quantitative, and Mixed Method Approach*. London: SAGE publication.

Chacha, Ch, (1992), *Sauti ya Utetezi*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Faqih, M. (1980). *Utenzi wa Rasi L-Ghuli*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Kezilahabi, E, (1982), *Ushairi wa Shaaban Robert*. Nairobi: Literature Bureau.

Kihore, Y na Chuwa A, (2004), *Kiswahili katika karne ya ishirini na moja*. Dar-es-Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Haji, A. (1981). *Misingi ya Nadharia ya Fasihi*. Zanizibar: Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni.

Haji, M. O. (2013). *Nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema, shule za sekondari visiwani, Zanzibar*. Chuo kikuu huria cha Tanzania.

Hashil, S. H, (1986), *Sauti ya Muhajirina*. Sweedeni, Repro-Centralen.

Hichens, W. (1972). *Al-Inkishafi. The Soul's Awakening*. London: Oxford University Press. Nairobi.

Hornsby, A. (2000). *Advanced Learner's Dictionary.6th ed*. London: Oxford University Press.

Kineene wa mutiso, (2005). *Utenzi wa Hamziyyah*. Dar-es-Salaam.Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Chuo kikuu cha Dar-es- Salaam

Kombo, na Tromp, (2006), *Proposal and Thesis Writing. An Introduction*. Nairobi: Paulines Publication. Africa.

Kothari, (2001), *Research Methodology.Methods and Techniques*. Ed. New Delhi: Wiley Eastern. India

Kothari, C. R, (2004), *Research Methodology, Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International (P) Ltd.

Kothari, R, (2009). *Research Methodology, Methods and Techniques*. New Delhi: Age International Publisher.

Kumar, R. (1999), *Research Methodology. A step by Guide For Beginners*. New Delhi: Sage Publication.

Lewis, J na Ritchie, J. (2012). *Qualitative research practice. A guide for Social Science Students and Researchers*. Carlifonia: SAGE PublicationS.

Madumulla, J (2009), *Riwaya ya Kiswahili. Nadharia, Historian a misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Education Publishers Ltd.

Masabo, T.na Kiango J (1996), *Mulika na. 23*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. TUKI.

Masawe, M, (2010), *Athari za dini kwenye tambiko katika jamii ya Warombo, Tarafa ya Mengwe*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mbunda, F, (2006), *Application of teaching and learning theories*. Dar-es-Salaam. The open University of Tanzania

Mdee, J. na Mbogo, E. (1985), *Mulika Vol. 17*. Dar es Salaam: Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Momanyi, C. (2012), *Kiswahili na Utaifa nchini Kenya*. Nairobi: Twaweza Communication. Kenya

Morrison, K, (2011). *Research Methods in Education. 7th edition*. New York. Routledge.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Publishers Ltd.

Mulokozi, M. M. (1989). *Mgawanyo wa Tanzu na Vipera vya Fasihi Simulizi*. Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi, M. M, (1996), *Fasihi ya Kiswahili.Dares Salaam*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Mulokozi, M. M, (1999), *Tenzi Tatu za Kale. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Mulokozi, M.M na Kahigi, K.K (1979). Kunga za Ushairi na Diwani yetu. Dar es salaam. Tanzania Publishing House.

Nachmias, D, (1981). *Research Methods in Social Sciences*. St Martin's Press Inc. London.

Nassir, A, (1974), *Malenga wa Mvita. Diwani ya Ustadh Bhalo*. London: Oxford University Press.

Ndumbaro, F, (2014), *Ripoti ya utafiti*. Dar-es-salam.Chuo Kikuu Cha Dar-es-Salaam: Taasisi ya taaluma za Kiswahili.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999), *Ufundishaji wa fasihi, Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Ntarangwi, Ch, (2004). *Uhakiki wa kazi za fasihi*. Nairobi: Oxford University Press.

Salum, S. R, (2007). *Tasnifu Ndogo, Nafasi ya Kasida za Kiswahili kwa Jamii ya Wazanzibari*. Zanzibar: Chuo Kikuu cha Taifa Cha Zanzibar.

Saleh, T, (2011), *Dhima ya nyimbo katika matambikoya Wazaramo*. Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Sanga, A, (1999). *Social Science Research Methods.* Dar-es- Salaam. The Open University of Tanzania.

Senkoro, F. (1988). *Ushairi. Nadharia na Tahakiki*. Dar-es-Salaam: Dar-es- Salaam University Press.

Sengo T. S, (1979). *Mashairi ya Mfungo wa Ramadhani.* Dares Salaam: Eastern Africa Publication

Sengo, T. S. Y. ( 2009). *Sengo na fasihi za Kinchi*. Dar-es Salaam: AERA Kiswahili Researched Product.

Senyamanza, Ch. (2015). Tathmini ya Mabadiliko ya Rara Mintarafu Maendeleo ya Jamii. Uchunguzi katika mikoa ya Mbeya na Dar-es Salaam. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Shariff, I, (1988), *Tungo zetu. Msingi wa mashairi na Tungo nyenginezo*. Trenton: The Red Sea Press.

Urassa, C, (2011), *Athari za Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia katika Nyimbo za Michezo ya Watoto*. Dar-es-Salaam.Chuo Kikuu Cha Dar-es-Salaam.

Vaus, D, (2011), *Research Design in Social Research.* London: SAGE Publication Ltd.

Wamitila, K. W. (2002), *Uhakiki wa Fasihi. Misingi na vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K. W, (2003), *Kamusi ya fasihi. Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publication Limited.

Wamitila, K. (2004), *Kichocheo cha Fasihi. Simulizi na Andishi*. Nairobi. Focus Publication Limited.

TUKI, (2004), *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Nairobi: Oxford University Press.

# VIAMBATANISHI

## Kiambatanishi A: Muongozo wa Maswali ya Usaili kwa Ajili ya Wanafunzi wa Mad-Rasa

Mpendwa Mhojiwa,

Ninafanya utafiti kuhusu Mabadiliko ya kasida, fani na dhamira. Lengo la utafiti huu ni kuchunguza maendeleo ya fasihi ya kasida hapa Wilaya ya Mjini Magharibi. Nitashukuru sana ikiwa utajibu maswali haya kwa makini, uwazi, usahihi na ushirikiano wa hali ya juu. Taarifa zote utakazozitoa zitakuwa ni siri baina yetu na hazitotumika kwa kwa lengo jengine lolote zaidi ya lengo lililoelezwa hapo juu.

Maswali yenyewe ni kama yafuatayo

Jaza taarifa hizi kwa makini

Umri…………………………………………………………………………………

Jinsia ……………………………………………………………………………….

Nambari ya simu ……………………………………………………………………..

i) Ni wakati gani kasida husomwa
…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

ii) Je wewe umeshawahi kushiriki katika usomaji wa kasida?

……………………………………………………………………………………..…

iii) Kama ndio eleza ni akina nani hushiriki katika usomaji wa kasida?

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

iv) Eleza shughuli tatu ambazo huwa mnasoma kasida hapa Zanzibar

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

v) Kwa nini mnasoma kasida katika shughuli mbalimbali?
…………………………………………………………………….…………

…………………………………………………………………………………………

vi) Jee, kasida zina faida yoyote kwa jamii?

…………………………………………………………………………………………
……

vii) Eleza maudhui muhimu yanayopaikana katika kasida za Kiswahili zinazosomwa hapa Zanzibar

……………………………………………………………………………………...…

…………………………………………………………………………..………

viii) Jee kasida wakati wote husomwa sawa au huzingatia matukio maalum?

……………………………………………………………………………………..…

ix) Ni akina nani husoma kasida hapa Unguja?
…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

x) Ni mafunzo gani hupatikana kutokana na usomaji wa kasida?

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

xi) Eleza hasara tatu ambazo hupatikana katika usomaji wa kasida

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

**AHSANTE KWA USHIRIKI WAKO**

**Kiambatanishi B: Muongozo wa Maswali ya Usaili kwa Ajili ya Walimu wa Mad-Rasa**

Mpendwa Mhojiwa,

Ninafanya utafiti kuhusu Mabadiliko ya kasida, fani na dhamira. Lengo la utafiti huu ni kuchunguza maendeleo ya fasihi ya kasida hapa Wilaya ya Mjini Magharibi. Nitashukuru sana ikiwa utajibu maswali haya kwa makini, uwazi, usahihi na ushirikiano wa hali ya juu. Taarifa zote utakazozitoa zitakuwa ni siri baina yetu na hazitotumika kwa lengo jengine lolote zaidi ya lengo lililoelezwa hapo juu.

Maswali yenyewe ni kama yafuatayo

Jaza taarifa hizi kwa makini

Umri………………………………………………………………………………………

Jinsia ……………………………………………………………………….………………

Nambari ya simu ……………………………………………………………………………

i) Jee umeshawahi kutunga kasida za aina yoyote?....................................................

ii) Kwa maoni yako eleza maana ya kasida? …………………………………………

iii) Ni ufundi upi wa kifani unaotumika katika utungaji wa kasida?…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

iv) Kuna tafauti gani kati ya kasida zilizotungwa na kusomwa wakati wa mapinduzi na zile za

baada ya mapinduzi? Elezea tatu
……………………………………………………………………….............................
.........................................................................................................…........................
......................

v) Mtunzi wa kasida husukumwa na mambo gani kabla ya kutunga kasida yake?

………………………………………………………………………………………………
……

viii) Ni mbinu gani zinazotumika katika utungaji wakasida?

………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
…………

vi) Kuna tafauti gani ya kifani na kimaudhui kati ya kasida zilizosomwa wakati wa mapinduzi na zilizosomwa wakati wa utandawazi na soko huria? Eleza tafauti tatu.

………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
…………

vii) Unafikiri tafauti hizo zinasababishwa na kitu gani?
.....................................................................................................................................
.....................................................................................................................................
......................

viii) Ni maudhui gani yanatarajiwa yapatikane katika tungo za kasida? Eleza maudhui matatu tu

.....................................................................................................................................
.....................................................................................................................................
......................

ix) Eleza mafunzo muhimu yanayopatikana katika usomaji wa kasida
…………………………………………………………………………………...………
………………………………………………………………………………………………
…………

AHSANTE KWA USHIRIKI WAKO

**Kiambatanishi C: Muongozo Wa Maswali Ya Usaili Kwa Ajili Ya Wasikilizaji Wa Kasida**

Mpendwa Mhojiwa,

Ninafanya utafiti kuhusu Mabadiliko ya kasida, fani na dhamira. Lengo la utafiti huu ni kuchunguza maendeleo ya fasihi ya kasida hapa Wilaya ya Mjini Magharibi. Nitashukuru sana ikiwa utajibu maswali haya kwa makini, uwazi, usahihi na ushirikiano wa hali ya juu. Taarifa zote utakazozitoa zitakuwa ni siri baina yetu na hazitotumika kwa lengo jengine lolote zaidi ya lengo lililoelezwa hapo juu.

Maswali yenyewe ni kama yafuatayo

Jaza taarifa hizi kwa makini
Umri…………………………………………Jinsia ………..……………………

Nambari ya simu ……………………………………..……………………….……

i) Jee, umeshawahi kusikiliza kasida? ………………………………………………

ii) Kama ndiyo, ni aina gani ya kasida ulizowahi kuzisikiliza? ................................

iii) Ni nini kazi ya kasida kwa jamii ya Wazanzibar?

.........................................................................................................................................
...........iv) Jee kuna dhamira zozote zinazokusudiwa katika usomaji wa kasida? Taja mbili

……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
…………

v) Unafikiri kuna tafauti yoyote kati ya usomwaji wa kasida leo na kipindi cha miaka 20

iliyopita?…………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………...

vi) Kama kuna tafauti, eleza tafauti mbili
...........................................................................................................................
...........................................................................................................................
...................... vii) Unafikiri kuna hasara yoyote katika kusikiliza kasida?
...........................................................................................................................
...........................................................................................................................
......................

viii) Jee lugha inayotumika katika uwasilishaji wa kasida inaendana na hadhira? Elezea

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………

ix) Kasida zinazosomwa harusini huwa na maudhui gani? Taja dhamira mbili.

i)……………………………………………………………………………
ii)……………………………………………………………………………

x) Taja ala tatu zinazotumika katika usomaji wa kasida.

a) ……………………………………………………………………………………
……
b) ……………………………………………………………………………………
……
c) ……………………………………………………………………………………
……

xi) Ni athari gani zinajitokeza katika kasida kutokana na maendeleo ya sayansi teknolojia? Taja athari mbili.

a) …………………………………………………………..……………………
……………….…………………………………………………………………
………………
b) ……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
…………

AHSANTE KWA USHIRIKI WAKO.

**Kiambatanishi D: Muongozo Wa Maswali Ya Usaili Kwa Ajili Ya Waandishi Wa Habari**

Mpendwa Mhojiwa,

Ninafanya utafiti kuhusu Mabadiliko ya kasida, fani na dhamira. Lengo la utafiti huu ni kuchunguza maendeleo ya fasihi ya kasida hapa Wilaya ya Mjini Magharibi. Nitashukuru sana ikiwa utajibu maswali haya kwa makini, uwazi, usahihi na ushirikiano wa hali ya juu. Taarifa zote utakazozitoa zitakuwa ni siri baina yetu na hazitotumika kwa lengo jengine lolote zaidi ya lengo lililoelezwa hapo juu.

Maswali yenyewe ni kama yafuatayo

Jaza taarifa hizi kwa makini,

Umri………………………………………………………………………………

Jinsia ………………………………………………………………………………

Nambari ya simu
……………………………………………………………………………….

i) Jee umeshawahi kushiriki katika kuandaa au kurusha vipindi vinavyohusu kasida?
…………………………………………………………………………………………

ii) Kwa nini mnaandaa vipindi vya kasida?
…………………………………………………
……………………………………………………………..………………………
………

iii) Ni wapi nyinyi huzipata hizo kasida?
……………………………………………………
……………………………………………………………………………...…………
………

…………………………………………………………………………………………
……...

iv) Ni kasida za aina gani redio / televisheni yako hupendelea kurusha?
……………………

…………………………………………………………………………………………………
……...

v) Ni dhamira gani hupatikanan katika kasida?
……………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………
……..

v) Ni faida gani unatarajia jamii hupata kwa kusikiliza au kutazama kasida mnazowaandalia?

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………

vi) Unafikiri kasida huwasaidia wanajamii? Eleza kwa ufupi huwasaidia vipi?
…………..…
……………………………………..…………………..……………………………
…………………………..……………………………………………………………
………………

vii) Jee, umegundua tafauti yoyote ya kimaudhui kati ya kasida za miaka ya hivi karibuni na zileza zamani?
…………………………………………………………………………………………………
……
…………………………………………………………………………………………………
……

viii) Kama zipo ni zipi?…………………………………..……………………………….
…………………………………………………………………………………………………
……

AHSANTE KWA USHIRIKI WAKO

**Kiambatanishi E: Muongozo wa Maswali ya Usaili kwa Ajili ya Wazee**

Mpendwa Mhojiwa,

Ninafanya utafiti kuhusu mabadiliko ya kasida, fani na dhamira. Lengo la utafiti huu ni kuchunguza maendeleo ya fasihi ya kasida hapa Wilaya ya Mjini Magharibi. Nitashukuru sana ikiwa utajibu maswali haya kwa makini, uwazi, usahihi na ushirikiano wa hali ya juu. Taarifa zote utakazozitoa zitakuwa ni siri baina yetu na hazitotumika kwa lengo jengine lolote zaidi ya lengo lililoelezwa hapo juu.

Maswali yenyewe ni kama yafuatayo

Jaza taarifa hizi kwa makini

Umri……………………………………………….. Jinsia ………………………………. Nambari ya simu ……………………………………………………….…………….

i) Unafahamu nini kuhusu kasida? ………………………………………………….
…………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………
………………

ii) Taja matukio matatu yanayoamabatana na usomaji wa kasida
a) ………………………………………………………………………………
b)……………………………………………………………………………
c) ………………………………………………………………………………

iii) Je kasida zinazosomwa katika matukio tafauti huwa na dhamira sawa? Kama ni tafauti eleza tafauti hizo
…………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………
………………………

iv) Ni ala gani zilitumika katika uwasilishaji wa kasida kwa hadhira hapo zamani?

…………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………
………………

v) Kuna tafauti gani kati ya usomaji wa kasida siku hizi na zile za zamani?

…………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………
………………………

vi) Ni lugha ya aina gani ilitumika katika usomaji wa kasida kati ya zifuatazo?

A: Lugha ngumu
B: Lugha ya mafumbo
C: Lugha rahisi

vii) Nisomee kasida unayoijua na unieleze maudhui yake

viii) Ni watu wa rika gani walisoma kasida katika miaka ya 1970?

…………………………………………………..……………………………
……………………………………………………………………………………
……………

ix) Jee usomaji huo ulikuwa wa kuchanganyika kijinsia au bila ya kuchanganyika?

…………………………………………………..……………………………
……………………………………………………………………………………
……………

x) Jee kuna haja yoyote ya kuziendeleza kasida? Toa sababu mbili

a) ……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
…………

b) ……………………………………………………………………………………
…………………………………………………………..……………………
……………

c) Unafikiri maendeleo ya sayansi na teknolojia yameathiri uwasilishaji wa kasida? Kama yameathiri, eleza athari hizo

……………………………………………………………………………………
……………………………………………..…………………………………
……………………………………………………………………………………
………………..…………………………………………………………………
…………………………

d) Kasida za zamani zilikuwa refu au fupi fupi

……………………………………………………………………………………
..……

e) Toa maoni yako juu ya usomaji wa kasida katika zama tulizonazo.
………………………………………………………………………………
…………………………………………..………………………………
………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………
……………………………

AHSANTE KWA USHIRIKI WAKO.

**Kiambatanishi F: Faharasa ya Kasida**

1. **Tarehe ya Uzawa**

Tarehe ya uzao Wa tumwa Muhammad
Ilithibitika Na hao Maulana
Ikathibitika pasi na inadi
Na wanazuoni Wapokezi wema
Kwa utakatifu Wa elimu zao
Na sisi wafuasi Tunawaegema
Alizaliwa rasuli Nabia nabia habiballah
Ya habiballah Ya Rasulillah

Upepo ulitulia Na mawimbi ya bahari
Wakati wa kuzaliwa Saa za alfajiri
Hapo ikanakiliwa Tarehe hiyo ya kheri
Amezawa mlezi Muhammad Kipenzi cha Waislamu pia
Malaika wa kheri walishuhudia
Uzazi wa fakhari wa chumwa nabia
Alihudumiwa Mwana Aminati
Na mama Mariamu Na mama Asia
Pia kwa hekima Za mola karima
Mahiri wa peponi Walihudhuria
Kumpokea kipenzi Nabia nabia habiballah
Kuongoza yake enzi Nabia nabia habiballah
Yahabiballah ya rasullillah

Zilisikika kauli Za wanyama wa baria

| | |
|---|---|
| Zikatamkwa kwa ari | Lugha ya kiarabia |
| Amezaliwa jabbari | Bwana wa mitume pia |

Muhammad rasuli kiongozi wa kweli kwa umatiwe jamia

| | |
|---|---|
| Muangaza wa nuru | Ulizagaa |
| Na kutoa bishara | katika dunia |
| Ulithibitika | Utukufu wake |
| Tokea utotoni | Alipoanzia |
| Mingi miujiza | Mikononi mwake |
| Na nuru ya utume | ikauzingia |
| Alipambika kikweli | Nabia nabia habiballah |
| Kwa sifa zisothakili | Nabia nabia habiballah |

Yahabiballah yarasullah

| | |
|---|---|
| Swalawatu wa salamu | Ziwe zikimshukia |
| Na sahabaze kiramu | Na Alizake jamia |
| Na sote Waislamu | Wake na waume pia |
| Nuru yake hashimia | Chumwa wetuMuhammad |

Ituangazie njia

| | |
|---|---|
| Alizaliwa rasuli | Kipenzi chake jalia |
| Katika makazi mema | Ya akhera na dunia |
| Kheri tunawatakia | Ali na swahaba pia |
| Pua yake ya upanga | Nyusi zake zimetanda |
| Mabegani muna mwanga | Mithili ya kamaria |
| Kheri tunwawatakia | Alia na swahaba pia |
| Wastani kimo chake | Mtukufu Umbo Lake |

| | |
|---|---|
| Ana mwanya meno yake | Kipenzi chake jalia |
| Kheri tunawatakia | Alia na swhaba pia |
| Tena mwingi wa akili | Tumwa akisema kweli |
| Wala hakua mkali | Kwa watu na maridhia |
| Kheri tunawatakia | Alia na swahaba pia |

2. **Mwezi Rabiul-awwal**

| | |
|---|---|
| Mwezi rabiul-awal | Saa za kupambanukia |
| Alizaliwa rasuli | Kipenzi chake jalia |
| Katika nyingi kauli | Za waliotangulia |
| Mtume alizaliwa | Katika kiza kikali |
| Cha watu wasoelewa | Kharamu wala halali |
| Ndipo akafaradhiwa | Kuiondoa batili |
| Baada ya kutimia | Arubaini miaka |
| Miaka ya kuhesabiwa | Tangu alipozaliwa |
| Hapo akakabidhiwa | Kila lilowajibika |
| Alishiriwa mema | Kwa waumini jalia |
| Iwapo atasimama | Kufuata yake njia |
| Kupata malipo mema | na peponi kuingia |
| Nasi tunamtakia | Sala na salamu pia |
| Ziwe zikimshukia | kutoka kwake jalia |
| Azidi kuhifadhiwa | na nuru kumuingia |
| Tumwa tunamuombea | Alii na swahaba pia |
| Na kila Muislamu | Dini alozingatia |
| Kwa Baraka za hashima | Fijanna kwenda ingia |

### 3. Twaomba Shifaa

Ghulama wametongoa / Mahali pa kuzaliwa
Vyema ni kisimamiwa / Ghadabu na taadhima
Kanuni uso mithali / Na swifa zako kamili
Wallahi nanena kweli / Swifa zako zote njema

Sote twataraji kwako / Utupe Baraka zako
Twaomba shifaa zako / Tushufaiwe adhimu
Ya rasula tumekuja / Na madhambi ya daraja
Wala hatuna zoroja / Madhambi yetu adhimu

Zimefunikwa mifupa / Na nyoyo zinaogopa
Twaomba kwako kutupa / Mtume shifaa njema
Kwani viumbe dhaifu / Sifa zao zote njema
Na mambo yetu machafu / Mtume wetu simama

Iwapo hutosimama / Hatuna wa kumuegama
Hasara huko kiama / Tushafaiwe adhima
Na laana tulizoshika / Moyoni mwetu hakika
Jinsi tulivyoweka / Kukutumia hashima

### 4. Tumsifuni Nabia

Tumsifuni nabia / nabii wetu Muhammad / marhabaya
Mbora wa sifa / mbora wa sifa nyingi za ajabu / nyingi za ajabu
Ndie wetu muokozi / Kesho mbele ya wahabu
Kapelekwa duniani / mtangazaji wa dini / mtume wetu nabia

Allah tumsalie Muhammad Muokozi wa kiama

Ilizagaa mianga Bwana alipozaliwa

Nuru ikatoa anga Huwa Allah

Pembe zote za dunia Huwa Allah

Ukaondoka ujinga Na nyoyo kukunjuliwa

Tuliambiwa zamani Ataletwa duniani mtume wetu nabia

Allah tumsalie Muhammad Muokozi wa kiama

Pepo iliumbwa kwake Bwana alipozaliwa

Ikajazwa mapamboe Huwa Allah

Mazuri ya kuvutia Huwa Allah

Hakuna aingiae Bila yeye kuingia

Atapandishwa daraja ataekuwa na haja ya kumsifu nabia

Allah tumsalie Muhammad Muokozi wa kiama

Sala watu wa salamu Ziwe zikimshukia

Na sahaba ikiramu Huwa Allah

Pamoja na Alii pia Huwa Allah

Na jamii isilamu Walomtii jalia

Atavikwa taji jema kila ataesimama na kumsifu nabia

Allah tumsalie Muhammad Muokozi wa kiama

5. **Uzuri wake Nabia**

Haiba na ukunjufu wa tumwa nabia, Muhammad

Na sifa za utukufu kutung’arishia, Muhammad

Hakika zake shauku zimetuingia, Muhammad

Na nyingi zaka sharafu kutumiminia, Muhammad
Hii ni kutushauri sote jamia    kufata njia ya kheri yake nabia

Baada ya kukithiri katika dunia, Muhammad
Zilienea habari kwa viumbe pia, Muhammad
Jamii vitu vya kheri vilimsalia, Muhammad
Na khofu kwa makafiri walimsemea, Muhammad
Kwa kuzaliwa kipenzi cha waumini
Aliyempa Mwenyezi daraja njema

Sote tunashuhudia kwa imani zetu, Muhammad
Hali aliyosifiwa kiongozi wetu, Muhammad
Kisha akafaradhiwa kwa niaba yetu, Muhammad
Ibada ya kutimia, faida ni yetu, Muhammad
Kamuahidi karima chumwa Amini    kulipwa fadhila njema kwa waumini

Katika bishara zake za utakatifu, Muhammad
Na kuuweka umma wake kwenye insafu, Muhammad
Na kuyaondoa yote yaliyo machafu, Muhammad
Tupate menendo wake, kwa njia nadhifu, Muhammad
Ili kukaa pamoja kesho kiama    kulipwa daraja njema hashima

Rehema za mola wake, tunamtakia, Muhammad
Swahaba na ndugu zake, walofuatia, Muhammad
Twaomba kushufaiwa na makosa yetu, Muhammad
Na pia kufadhaiwa kwa hidaya yetu, Muhammad

Kamuahidi Karimmu, mola jalia na pepo ni yake, adhimu kwenda ingia

**6**. **Ndoto ya Mama Amin**a

Ndoto ya mama Amina — Ilithibitika kweli
Ya kuzawa hashima — Mtume wetu rasuli
Alfajiri adhima — tarehe kumi na mbili
Vitisho vilisimama — Rehema ikawasili
Zote Makka na Madina — Zilinawirika
Ilipoingia nuru — Yake Muhammad
Mengi yalidhihirika — Mema yaliyokithiri
Ya dalili za hakika — Za uzao wa Rasuli
Mambo yanahesabika — Ya miujiza kamili
Ndipo zikawashituka — Roho zao Makafiri

Ardhi ilikunjuka — mimea ikanawiri
Na neema zikashuka — Za siri na za dhahiri
Watu waloelimika — Ndipo walipobashiri
Imekwisha dhihirika — Nuru ya chumwa hashima

Kwa kule kuzawa kwake — Zimefurahi suduri
Litajwapo jina lake — Nyoyo zetu hunawiri
Huomba kwa mola wetu — Amrehemu jabbari

Na sisi umati wake — Hatima iwe ya kheri
Sala na salamu zetu — Ya rabbi tufikishie
Kwa tumwa kipenzi chetu — Rehema mzidishie

Zifurahi nyoyo zetu kwa kukutana na yeye
Mbele ya hakimu wetu Bendera ashikilie

Zote Makka na Madina Zilinawirika
Ilpoingia nuru Yake Muhammad

**7. Sherehe Leo**

Leo imefika sherehe Tuloingojea
Kuja shangiria harusi Ya wenzetu pia *x2*

Ile siku yetu Furahaa
Imetufikia Kwa rahaa
Ya vipenzi vyetu Furahaa
Kuvishangiria Furaha *x2*
Tumuombe Mola Illah Karima
Marashi adhimu kuwa nyunyuzia *x2*

**Answer**

Wamependana wakaoana Wenyewe wameamua
Cheza kwa kituo mama arusi Leo ni mwanao hebu jinafasi
Taji lenye cheo tunakutajia Ni wa juu yao walofunga ndoa
Wana Qadiria tunaomba dua Yahaya Nabia kutushuhudia
Wamependana wakaoana Wenyewe wameamua

**8. Swifa za Nabia**

| | |
|---|---|
| Faida njema hutushukia | Tukimsalia Muhammad |
| Kauli Rabbi inaelezea | Kutoka ndani ya Qur'an |
| Hakika yake na malaika | Wanamsalia Muhammad |
| Haya isilamu | Sallu aley |
| Heshima kubwa aliyopewa | Na mola wake Muhammad |
| Na ithibati aliyopewa | Ya kuongoza katika dini |
| Ajira yake na umma wake | Katimiziwa Muhammad |
| Haya isilamu | Sallu aley |
| Nyoyoni mwetu tunafuraha | Ya kuzaliwa Muhammad |
| Na nuru yake ikamea | Kutuletea matumaini |
| Kwa utukufu aliopewa | Tunamsalia Muhammad |
| Haya isilamu | Sallu aley |
| Fadhila nyingi tunamsalia | Kutoka kwake Muhammad |
| Na radhi zake hutushukia | Zituokoe na mitihani |
| Tabia zake na sifa zake | Twazifatia Muhammad |
| Haya isilamu | Sallu aley |
| Wingi wa sala tunamsalia | Mtume wetu Muhammad |
| Na as-habu waliokuwa | Ubavuni mwake chumwa amini |
| Tupate radhi za chumwa wetu | Kwa kumsalia Muhammad |
| Haya isilamu | Sallu aley |

**9. Makureish wa Makka**

| | |
|---|---|
| Maudhi yaliposhitadi | Kwa makafiri yakini |
| Wakachukua juhudi | Ili waipinge dini |
| Wakazidisha inadi | Kubwa isiyo kifani |

Na mwisho ikawabidi Watoke Makka nchini

Hawakutaka kuhama Lakini wafanye nini?
Dhila zimewaegema Na kupinga yao dini
Kila wanalolisema Huwa hawana thamani
Ikawabidi kuhama Kukimbiza yao dini

Walikuwa mjabari Katu hawana imani
Kumpinga mukhtari Na kila aloamini
Wakawa wamevinjari Kuwatia matesoni
Wakaifanya safari Kukimbia mtaani

Hakika walikereka Wakakatika maini
Isilanu kuinuka Kuenea vijijini
Mungu kwa zake baraka Kufatia kifadhini
Ndipo tumwa katamka Bora sasa tuhameni

Njia akawaonyesha akawapa maskani
Madina kuelekea Huko wao wataani
Wakamwabudu jalia Pasi khofu asilani
Na tumwa kufuatia Abubakkr mwandani

Wakapokewa vizuri Kwa shangwe kubwa yakini
Muhajiri, answari Wakawemo furahani
Na dini ikanawiri Kuenea duniani
Walishindwa makafiri Wakawa ni watu duni

10. **Nuru Ilimemetuka**

Nuru ilimemetuka Kutoka nchi ya Makaa Kuelekea madina

Nuru ya mtume mwema Kiongozi msifika Tangu vitabu vya tana

Ya habibi Salamu alaykaa

Ya shafii Salamu alaykaa

Ibada tukufu Kumsalia chumwa mukhtari

Chumwa maarufu Aloteuliwa na mola wake kahari

Leo imefika siku njema ya furaha Siku alozaliwa chumwa Mustafa

Sote waumini Tulohudhuria Kwa imani zetu tunamsa

Ya habibi Salamu alaykaa

Ya shafii Salamu alaykaa

Ibada tukufu Kumsalia chumwa mukhtari

Chumwa maarufu Aloteuliwa na mola kahari

Ghufari wa Makka Hakika walishangaa Walipoiona nuru iliyozagaa

Moto wa mbioni ukawaingia Akili kichwani Zikawakimbia

Ya habibi Salamu alaykaa

Ya shafii Salamu alaykaa

Ibada tukufu Kumsalia chumwa mukhtari

Chumwa maarufu Aloteuliwa na mola wake

Vifuani mwetu Furaha imetujaa Na kumrahimu kwa imani na ridhaa

Hakika ya shetani alotuekea Nguzo ya imani kuitegemea

Ya habii Salamu alaykaa

Ya shafii Salamu alaykaa

Ibada tukufu Kumsalia chumwa mukhtari

Chumwa maarufu Aloteuliwa na mola kahari

Ushauri wake Ulijaa manufaa Kwa imani yake hekima na ushujaa

Elimu ya ndani Aloshushiwa Ndio usukani aloutumia

Ya habibi Salamu alaykaa

Ya shafii Salamu alaykaa

Ibada tukufu Kumsalia chumwa mukhtari

Chumwa maarufu Aloteuliwa na mola kahari

Sala na salamu ziwe zikimshukia Chumwa mkarimu na maswahabaze jamia

Nasi isilamu Tulomsalia Jannatu naimu kwenda kuingia

Ya habibi Salamu alaykaa

Ya shafii Salamu alaykaa

**11. Tumefurahika**

Waumini tumefurahika Siku ya leo kufika

Na nyoyo zetu hakika    Leo tumefurahika

Kwa kuzaliwa    Kipenzi chake rabuka

Sallu aley tunaitikia    Kwa mahaba yake nabia

Makafiri walikasirika    Chumwa wetu kuzalika

Uhasama wakaweka    Wakataka kuvunjika

Dini yetu    Isilamu ilotakasika

Mola wetu aso mshirika    Kawalani wakafedheheka

Alikuwa Mtume hashima    Ni mtu mwenye huruma

**12. Sifa za Kuoa**

KIITIKIO

Mtume maneno yake    Leo tunayapitia

Kila anotaka mke    Yupi atamchagua

Sifa nne zilopeke    Chumwa ametutajia

Kwanza ni kwa mali yake    Mwanamke huolewa

Pili ni uzuri wake    Umbo, sura na tabia

Hata na nasabu yake    Ya tatu kuangalia

Na mwisho ni dini yake    Iwe ya Isilamia

Na ili unufaike    Ni mweye dini chagua.

**Answar**

Wanaotaka kuoa    Nawamfate nabia

| | |
|---|---|
| Na wasia wake chumwa nabia | Waufate wakifunga ndoa |
| Wachague wake waliotimia | Wenye sifa zote nne ziso doa |
| Kama hana zote sifa jamia | Japo dini yake ndo inatakiwa |
| Na waombe kwake mola jalia | Wawapate wake waliotimia |
| Wanaotaka kuoa | Nawamfate nabia |

**13. Leo Imefika**

KIITIKIO

| | |
|---|---|
| Imetufikia Arusi | Tuloingojea |
| Nasi Qadiria kwa kasi | Tuashangiria |

| | |
|---|---|
| Tunatoa heko | Pia na wasia |
| Tena wende kwako | Unayeolewa |
| Uyo mume wako | Anayekuoa |
| Mpe moyo wako | kwa yanayovutia |

| | |
|---|---|
| Leo zamu yako | Imekufikia |
| Unakwenda kwako | Tena kwa sheria |
| Ishi na wenzako | Kwa njema tabia |
| Majirani zako | Watakuridhia |

| | |
|---|---|
| Chunga kinywa chako | Ukijisemea |
| Ili hadhi yako | Izidi kung’aa |

Wacha micharuko Ya kuruka njia

Dada kazi kwako Kufata wasia

Answar

Wamependana wakaoana Wenyewe wameamua

Cheza kwa kituo mama arusi Leo ni mwanao hebu jinafasi

Taji lenye cheo tunakutajia Ni wa juu yao walofunga ndoa

Wana Qadiria tunaomba dua Yahaya Nabia kutushuhudia

**14. Cheo cha Ndoa**

KIITIKIO

Mke cheo cha mumewe Kwenye ndoa
Hakifuti kwa malie Wala kwa twaa
Na pia mume asiwe Ajivunia
Sababu ya elimuye wala uluwa

Vyema muelewe hili Kwa wake muloolewa
Munaomiliki mali Nafasi na nyadhifa pia
Mukajitia kiburi Kuwakosea
Na kuzipinga amri Zake Jalia
Zile haki za rijali Kuziondoa
Eti yeye hana mali Kajichokea
Ni vizuri kuwajali Wanowambia
Japo kama zao hali Sio sawia.

Mwazitengua amri Wanawake twawambia

Muda kwenu ni thakili Wao kuwahudumia

Kwa kweli muna khiari Kushughulikiwa

Na wanawake wambali Wasowaowa
Wawe wanawakabili Kuwapikia
Pia mambo mbali mbali Kuwafanyia
Na ujira mutayari Kuwapatia
Jambo hili si sahihi Munakosea

Na kwa upande wa pili Pia wanazo tabia
Waume twawahubiri Walobeba ya dunia
Huwadharau kikweli Walowaowa
Pia na kuwakejeli Kwa mbaya njia
Kwani huwa hawajali Waloamriwa
Kazi zimewakabili Bize wajitia
Muda kwao ni muhali Kuwa pamoya
Na mke hana kauli Hujinamia
Japo kama si halali Anofanyiwa
Lakini huyakubali Ndo kaolewa

Haki zenu muheshimu Mke na mume pamoya
Hata kama mnajikimu Musizibadili sharia

Muhimu kuhudumiana Pia ndani kutulizana
Muupate na muda vyema Kukaa pamoya na wana
Hapo ndipo mtapendana Na ndoa yenu itafana
Kwa kule kushirikiana Na haki kutimiziana
Na izidi yenu heshima Hili mulielewe vyema

Na sio kwenu kuvutana	Usiku unaposimama
Yapasa muelewe vyema	Enyi ndugu waislama
Haki zenu muheshimu	Mke na mume kwa pamoya
Hata kama mnajikimu	Musizibadili sharia

**15. Wacha Maringo Mwanadama**

Usiringe kwa ujana
Wala mali na wana
Wangapi vijana waliokufa
Wazee wakabakia?

**16. Namshukuru Jalia**

Namshukuru jalia
Kuna wengi walifadhaika
Na wachache wakasikitika
Na kuhuzunika kwa kupata mtihani
Dua njema wakaniombea
Shani yake Rabbana
Si kama kanionea
Apendapo Subhana
Mtihani atauondoa.

**17. Tunaomba Kwako**

Naomba kwako jaala	Rabi utupe maisha mema

Pia utulinde na mabaya Amina Rabbi Amina

**18. Kiza ya Illhi Kiza**

Kiza ya Illahi kiza

Utupe muangaza mwema

Illahi mola jalia

Utukimbizie na moto

Moto wa jahannama

**19. Uzao wa Tumwa**

| | |
|---|---|
| Alipozaliwa Mtume | Nyumba tukufu |
| Ardhi ya Makka | Mahala hapo maarufu |
| Amepatukuza Taala | Mola Raufu |
| Kwani kazaliwa kiwanja hicho | Tumwa khatima. |

**20. Siku ya Malipo**

Tukumbuke wanadama, Siku ya malipo

Itafika na kuhukumiwa

Maovu yamekithiri

Nafasi ya haki kuwekwa batili

Hiyo ni hasara tumeshaumia

**21. Mama Arusi Hongera**

Mama arusi Hongerax3 Mama arusi hongera

Baba arusi Hongerax3 Baba arusi hongera

1. Leo siku imetimu Aloandika Raufu
   Yenye tukio muhimu La furaha timilifu
   Tumejaa tabasamu Na nyoyo zetu kunjufu
   Na haki jambo adhimu Nderemo bila ya khofu.
2. Hongera mama hongera Ndie alo mswarifu
   Hongera baba hongera Umemfunza Uwongofu
   Mmeshampa nusura Mumemuondolea machafu
   Wallahi leo mwangaza Kazi yenu timilifu
3. Ndugu zake wakarimu Nao pia twawaswifia
   Kwa kiwango maalum Mukatoa zurufa
   Mukachukua jukumu Mipango kuisarifu
   Leo arusi metimu Rai zenu twazisifia
4. Sasa ni yenu adhara Majirani twawasifia
   Mmeishi kwa busara Na roho za ukunjufu
   Mkafanya kila bora Ndoa iwe timilifu
   Leo twawapa hongera Majirani twawasifu
5. Mwisho twaomba Qarima Mola wetu mtukufu
   Arusi hii adhimu Idumishe muda mrefu
   Neema kila sehemu Uwajazie kwa safu
   Swiratu mustaqima Waongoze ya raufu.

**22. Furaha Iyoo**

Furaha iyoo Harusi yoyoo
Furaha iyoo Harusi yoyoo

1. Vijana wa Qamariyya Furaha metuingia
   Shime na nyote jamia Harusi kufurahia
2. Leo tunashuhudia Ndoa iso mithilia
   Kwa Baraka za nabia Muishi bila udhia
3. Usia kwa wanandoa Muzidumishe sharia
   Jema kulifuatia Ovu kulipuuzia

4. Tunakuomba jalia    Idumishe yao ndoa
   Uwape njema twabia    Na mema yasoudhia

**23. Mtume Mwema**

Katuhudhuria    Mtume mwema    Kwa yakini twafurahia
Vyema twatubia    Mtume mwema    Sifa zako twazitongoa

Tunaposikia    Mtume mwema    Isimuye twamswalia
Nyoyo zachanua    Mtume mwema    Muhammad tukisikia

Katuelezea    Mtume mwema    Nuru yake hutung'aria
Hutusimamia    Mtume mwema    Dua njema kutuombea
Sala na salamu    Mtume mwema    Na baraka twakutakia

Kwake muadhamu    Mtume mwema    Shufaae twatarajia.

**24. Imeshawadia**

Imeshawadia    Tarehe adhima    Waumini wema    Twafurahia
Aliyoshukia    Kiongozi mwema    waumini wema    Twafurahia

Katuhudhuria    Mtume mwema    Kwa yakini    Twashingiria
Vyema twatubia    Mtume mwema    Sifa zake    Tukitongoa

Tunaposikia    Mtume mwema    Asemayo    Twamswalia
Nyoyo za tumwa    Mtume mwema    Muhammad    Tukisikia

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kutuelezea | Mtume mwema | Nuru yake | hutung'aria |
| Hutusimamia | Mtume mwema | Dua njema | kutuombea |

**25. Ya Zamzam**

Ya Zamzama Ya Zamzama
Alikunywa chumwa Maji mema
Ya Zamzama

Tufunge safari waumini Kweda Madina
Kwenda kulidhuru Kaburi la chumwa amini
Lenye utukufu wa sharafu Kila aina
Lilopitishwa maji mema Ya Zamzama

Tupate msifu Mustwafa Mtume mwema
Huzidi sharafu kwetu sote Waislama
Huzunguka swafu Malaika Wakitazama
Wakiturushia maji mema Ya Zamzama.

Wale watukufu maswahaba Wa zake zama.
Waliojikifu kwa udhati Wakamwegama
Kaaba tukufu mbele yake Walisimama
Wakafurahia maji mema Ya Zamzama

26. **Oa dugu yangu Oa**

Oa ndugu yangu oa Kama ilivyo sheria
Mtume kafunga ndoa Pia mahari akatoa
Kahalalisha manani Oaaa

Kwenye yake Qur'an Oaaa

Harusi hii yakini Oaaa
Furaha kwa waumini Oaaa

Hakika ya Rahmani Oaaa
Ndoa huleta amani Oaaa

Harusi iwe ya kheri Oaaa
Mufurahi maishani Oaaa

**27. Leo umefunga ndoa**

Sote tunashangiria aaa Harusi ya kaka yetu
Leo umefunga ndoa
Ndugu yetu mtukufu Aaaa
Leo twamvika taji Aaaa
Tunakuomba raufu Aaaa
Uzidi kumfariji Aaaa
Akujalie Latifu aaa Mema yawe mahitaji

Rabi umpe Baraka Aaaa
Ndani ya machumi yake Aaaa
Umuepushie shaka Aaaa
Jamii kazini wake Aaaa

**28. Ya Rabbi Salama**

| | |
|---|---|
| Twakuomba mola wetu | Utupe nyingi hekima |
| Kwa uswafi nyoyo zetu | Tukutukuze daima |
| Pia na Mtume wetu | Muhammadi muadhama |
| Alokuja mbele yetu | Kuongoza dini njema |

Aaa Yarabi

| | |
|---|---|
| Zipokee dua zetu | Ilahi mola karima |
| Ufute madhambi yetu | Yote tuliyoyachuma |
| Utupe nuru Ilahi | Leo na kesho kiama |
| Tuwe nae chumwa wetu | Katika makazi mema |

Aaa Yarabi

| | |
|---|---|
| Twatubia sisi waja | Wako kwako twarejea |
| Twataraji msamaha | Kwa yote tulokosea |
| Utujalie ya Allah | Tuwe wenyekusimama |
| Katika kundi la wema | Na peponi kuingia |

Aaa Yarabi

**29. Wafiwa Shikeni Mikono**

Wafiwa tunawapa pole

Wafiwa shikeni mikono

Tunawapa pole

**30. Nadhiri Leo Tuaiondoa**

| | |
|---|---|
| Mikono yako miwili | Kwa wema ilinyanyuka |
| Maombi yaso dosari | Kwa mola ukapelekwa |

Kizazi kilo kizuri — Mzazi uweze pata
Leo kwako ni fakhari — Hili limeshatimika

Uliiweka nadhiri — Ilo njema bila shaka
Hilo litakapojiri — Maulidi utaweka
Kwa mola wetu kahari — Kilio kikasikika
Zawadi ilo jamili — Kwako wewe ikaletwa

Sala zako ulosali — Vizuri zimejibika
Ukahisi ni vizuri — Wanafunzi kutuita
Ikiwa yako dhamiri — Maulidi kujaweka
Nasi bila ya kujali — Leo hapa tumefika

Nasi leo tutayari — Dua njema kuzileta
Aepukane na shari — Mtoto alozalika
Afate njia halali — Na haramu kuiacha
Lengo zote idhilali — Kwake ziweze ondoka

**30. Muhammad Rasuli**

Muhammad — Muhammad rasuli
Sote tunamjua — Sote tunamjua
Kiongozi wa dini — Mashuhuri
Mola kamteua — Mola kamteua
Awe mbele yetu — Muhammad rasuli
Siku ya kiama — Huwa safiaallah

Muhammad Swalawatullah

Alikuwa mwingi wa ukarimu		Kwa jamii ya walioamini
Na maneno yake ni ya elimu		Yanatoka ndani ya Qur'an
Katuletea karimu		Muangaza wenye shani
Awe mbele yetu		Muhammad rasuli
Kiongozi wa dini		Huwa safiaallah
Muhammad Swalawatullah

Mwendo wake walioubaini		Walisema huwa wa kunyatia
Visigino havikugusa chini		Na mchanga ili kuuridhia
Na sisi tulioamini		Hakika twazingatia
Utukufu wa Muhammad rasuli		Alijaliwa huwa safiaallah
Muhammad Swalawatullah

Khatimae wakawa miguuni		Wakifuata mwendo aendao
Ndipo walipobaini		Kufudhu mema yajayo
Aloahidiwa Muhammad rasuli		Kwa amali zao, huwa safiaallah
Muhammad Swalawatullah

**31. Karibuni Wageni**

Sherehe leo jama		Tunashangiria

Sherehe leo		Tunafurahia x2

1. Karibuni nyi wageni		Nyote mlohudhuria
   Mlo hapa uwanjani		Shukurani twawambia
   Mujihisi mu nyumbani		Kama mlikotokea

Hiyo hofu ondoweni    Mkae mkitulia x2

Kiitikio

2. Twaanza nao wazazi    Ndio waliowalea
Hawa wetu wanafunzi    Hadi hapa kufikia
Pia nao viongozi    Juhudi walichukua
Kuongoza wanafunzi    Ndio leo wanag’ara x2

Kiitikio

3. Twakuomba ya Rabana    Ilahi mola Jalia
Ukinyanyuwe kwa wima    Chuo chetu Faraghiya
Umpe nyingi neema    Mwalimun wetu Bihila
Kwa kusimamia vyema    Chuo chetu Faraghiya x2

Kiitikio

Kwa shangwe jama    Tunashangilia
Sherehe leo    Imetufikia

**32. Ngome adhimu**

1. Ngome iliyo adhimu    Wazazi wao hulinda
Huinza na mapema    Dhumuni lao kulenga
Awe wao msichana    Adabu mweye kutenda
Humpa mafunzo mema    Hasa kwa somo huenda
Na humuambia umekua    Unayotakiwa kufanya haya

2. Hufanya kila aina    Mwana asije kupinda

Hulinda yake heshima — Kwa kila anaporanda
Huipalilia vyema — Ipendeze yao shamba
Ili atokujavuna — Isije ikamshinda
Humsimamia, humfatilia — Asijepotea njia mbaya

3. Leo sasa twawaona — Wazazi wanavyotamba
Wamefurahika sana — Wamejifunga na kanga
Kazi waliyoifanya — Mwana kumuenga enga
4. Leo wanampa bwana — Mwenyewe alompenda

**33. Ile Siku Leo Imefika**

1. Maisha mazuri kuwajaalia — Na yote ya shari kuwaepushia
Kila la fakhari kuwamiminia — Na mwanga wa nuri kuwaangazia
Maneno ya shariyatawakimbia — Waishi vizuri pasi a ubaya
2. Kuondoka kwako ukatukimbia — Mazoea yako yakatupotea
Na haiba yako tuloizoea — Ya swauti yako yenye kuvutia
Kwetu sikitiko lisiloishia — Tukukumbukapo hwenda tukalia
3. Ila kwa sababu hii ni sharia — Twamuomba Rabu kukujaalia
Moyo wa dhahabu kukukunjulia — Madhila na tabu kupotea njia
Kwako umuhimu kwenda muombea — Iwe ni sababu neema kungia

**34. Dua njema**

Dua njema — Tunamtakia

Mtume mwema Khayrul-anbiya

1. Wote Maswahaba Walimswalia
   Wakajenga huba Na yeye nabia
   Na zao ghuluba Wakafikiria
   Na zao hisaba Wakajipatia
2. Kumswalia Nabia Agizo lake jalia
   Kitabuni kawambia Rehema humtakia
3. Tufanyeni twiba Swala za Nabia
   Iwe ndio twiba Katika dunia
   Na zote ukuba Kutuepushia
   Yetu matilaba Tutakubaliwa
4. Ya Rabi Mola Jalia Dua zetu zisikia
   Tufikishie Nabia Salamu na swala pia.

**35. Furaha ya Wazazi**

Leo nyoyo za wazazi zimefurahika sana
Kwa kutimu hii ndoa

1. Ngonme iliyo adhima Wazazi wao hulinda
   Huianza na mapema Dhumuni lao kulenga
   Awe wao msichana Adabu mwenye kutenda
   Humpa mafunzo mema Hasa kwa somo huenda
   Na humuambia kwamba Umekua, unayotakiwa kufanya haya

2. Hufanya kila aina | Mwana asije kupinda
Hulida yake heshima | Kwa kila anaporanda
Huipalilia vyema | Ipendeze yao shamba
Ili atokuja vuna | Isije ikamshinda
Humsimamia, humfatilia | Asijepotea kwenye njia mbaya

3. Leo sasa twawaona | Wazazi wanavyotamba
Wamefurahika sana | Wamejifunga na kanga
Kazi waliyoifanya | Mwana kumuenga enga
Leo wanampa bwana | mwenyewe alompenda
Wanafurahia, wanafamilia | Kwa kuwafikia harusi murua

**36. Mazazi ya kheri**

1. Mazazi ya kheri | Tunasimulia
Shafiin nnuri | Alipofikia
Rabiil-awal Jumatatu | Thani Ashiria
Ni alfajiri Saa njema | Alipozaliwa
Kote ardhini na mbinguni | Amepokelewa

2. Binti Wahabi | Wa Kikureish
Amina habibi | Ametuzalia
Yeye ni turabi | Dawa njema ametuletea
Meleta mpenzi l-azizi | Muombezi wa umma
Mungu akuenzi kwa uzazi | Wa Shafii mwema

3. Tumwa Muhammad | Tunakusifia

| | |
|---|---|
| Umetuahidi | Tatushufaiya |
| Swala alaa Sayyid | Muhammad tunakuswalia |
| Qauli latwifu mahabubu | Alotuachia |
| Zenye utukufu wa kuruba | Tumezipokea. |